**17 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 17 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

Katibu tuendelee.

**17 MEI, 2023**

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 347

**Mkakati wa kuwawezesha vijana wa skauti nchini**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha kimaendeleo vijana wa skauti nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa vijana wengine wote wa Tanzania wakiwemo vijana wa Skauti ambao wapo kati ya miaka 15 hadi 35, Serikali kwa kushirikiana na Chama cha Skauti Tanzania, imeendelea kutekeleza programu mbalimbali kama vile Klabu za Skauti katika shule za msingi na sekondari ambapo vijana hupatiwa mafunzo ya ujasiri, kutatua matatizo katika jamii, kujitolea na uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, vijana wa skauti ni miongoni mwa vijana ambao hunufaika na programu mbalimbali zinazosimamiwa na Serikali ikiwa ni pamoja na

fursa za mikopo yenye masharti nafuu ili kuanzisha miradi ya uzalishaji mali inayowawezesha kujiajiri pamoja na mafunzo ya fani mbalimbali kupitia programu ya kukuza ujuzi nchini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Serikali ina mpango gani wa kuwanyanyua vijana hawa wa skauti walioiva kimaadili na kizalendo, kuwatengea mgao maalum wa kupata ajira zinapotokea kama vile kwa Jeshi la Wananchi na taasisi nyingine?

Mheshimwia Mwenyekiti, swali la pili: Serikali ina mpango gani wa kutenga ruzuku malalum kwa ajili ya shughuli za Skauti Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa vijana walioiva kiuzalendo ambao wanatoka skauti, na mara nyingi tumekuwa tukiwaangalia sana kwenye suala la ajira, na ajira hizi pindi zinapotokea ziwe za Serikali na pia kwenye taasisi na vyombo vyetu vya usalama, imekuwa ni moja ya sifa ama kigezo, kama wale walioenda Mgambo na *JKT* kuangaliwa kama sifa ya ziada. Kwa hiyo, tumekuwa tukiwaingiza kwenye vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na pia katika majukumu mengine ambayo yanatokana, au ajira zinazotoka upande wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu ruzuku; Skauti Tanzania imeanzishwa kwa mujibu wa sheria, na bahati nzuri kabisa, Skauti Mkuu Tanzania ni Amiri Jeshi Mkuu ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo, katika utaratibu wa masuala ya kuwawezesha, kama jinsi sheria ya kuwaanzisha wao inavyoeleza, ndivyo hivyo hivyo wanaweza kupata pia fedha kupitia mifuko mbalimbali ambayo inasaidia kama sehemu ya chombo ambacho ni kama Jeshi, yaani inafanana na ile ambayo ipo katika Jeshi la Mgambo. Kwa hiyo, msaada, na pia iko fedha inayotoka Serikalini na kuna fedha ambazo ni kutoka kwa wadau mbalimbali huzitoa kupitia mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutazidi kuangalia kuweza kuboresha zaidi maslahi ya Skauti wetu kwa sababu wamekuwa wakifanya kazi kubwa na hasa kwenye masuala ya uokoaji pale yanapotokea majanga, sherehe za kitaifa na majukumu mengine, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Usonge.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia fursa hii. Kwa kweli vijana wetu wa skauti wametapakaa takribani nchi nzima; Bara na Visiwani. Kama Mheshimiwa Waziri alivyokiri kwamba wanafanya kazi kwenye maeneo mbalimbali. Je, Serikali haioni haja sasa kutenga mfuko maalum wa kibajeti kupitia Wilaya, Mkoa na Kitaifa zaidi ili wawe na uhakika wa fedha zao kwa ajili ya kuendesha programu zao pamoja na kufanya kazi zao kiujumla? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Usonge ambalo limefanana pia na jibu langu la msingi,

na hata swali alilouliza Mheshimiwa Asha kwenye suala la kibajeti, kwamba tayari wao wana sheria ambayo inaanzisha na inatoa taratibu ikiwa ni pamoja na masuala ya kifedha, lakini kwa sababu pia ni eneo ambao linaonekana pengine lina upungufu, tutauangalia na Serikali na kuweza kuona pale panapopelea tuweze kuwasaidia zaidi na kutengeneza mifumo ambayo itawasaidia kuweza kuratibu na kutekeleza majukumu yao kama ambavyo jinsi tunawatarajia, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Patrobass Katambi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa majibu hayo. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, aulize swali lake.

Na. 348

**Upungufu wa walimu katika shule za sekondari – Babati Vijijini**

**MHE. DANIEL B. SILLO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapunguza tatizo la upungufu wa walimu katika Shule za Sekondari Babati Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaanza kupunguza tatizo la upungufu wa Walimu u katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati ambapo katika mwaka wa

fedha wa 2021/2022, walimu 50 walipelekwa katika shule zilizopo Babati Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetangaza nafasi 13,390 za ajira kwa walimu ambapo baadhi ya walimu hao watapangiwa katika Shule zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuajiri walimu na kuwapeleka katika shule zote nchini hususan katika maeneo yenye uhitaji kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Baran Sillo.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa wako walimu wanaojitolea kwa muda mrefu katika Shule ya Sekondari ya Wilaya ya Babati: Je, katika ajira mpya, Serikali iko tayari kuwapa kipaumbele hao wanaojitolea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa kati ya shule 38, kuna shule sita ambazo zina mwalimu mmoja mmoja wa kike wa Shule za Sekondari ya Taraget, Burunge, Nar, Kameri, Ndeku na Endamanang'; je, Serikali iko tayari kuongeza walimu wa kike katika shule hizi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la kwanza la Mheshimiwa Sillo la wale ambao wanajitolea; katika ajira hizi ambazo nimezitaja, Serikali imetoa 13,390, tutakwenda kwa kuangalia vigezo, kwa sababu ajira hutolewa kwa usawa.

Hao wanaojitolewa kama wameomba ajira hizi na wanakidhi vigezo vilivyowekwa katika tangazo la ajira, basi nao pia watapata, lakini hakutakuwa na upendeleo maalum ambao utatolewa kwa wale tu wanaojitolea kwa sababu wanajitolea, ili kutoa fursa sawa kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali la pili la upungufu wa walimu wa kike katika shule ambazo Mheshimiwa Sillo amezitaja, hili agizo lilishatolewa kwa Makatibu Tawala wote wa Mikoa Tanzania kuhakikisha wanafanya msawazo wa walimu katika mikoa yao. Sasa katika ajira mpya hizi zinazokuja, kuna walimu wa kike nao wataajiriwa, wakifika mikoani kule wapangiwe katika shule zenye upungufu wa walimu wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena hapa kuelekeza Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara kuhakikisha anafanya msawazo katika shule ambazo amezitaja Mheshimiwa Sillo kupeleka walimu wa kike kutoka ndani ya Mkoa wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu nimekuona.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa walimu katika Shule za Msingi na Sekondari katika Mkoa wa Simiyu: Je, ni lini Serikali itatuletea walimu wa kutosha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nimeshasema kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali imetangaza ajira 13,390 na kipaumbele pale watakapokuwa wanapangiwa shule walimu hawa, ni kwa mikoa ile yenye upungufu mkubwa, ukiwemo Mkoa wa Simiyu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika ajira mpya ambazo zinaendelea sasa, Serikali ina mpango gani kupeleka walimu katika shule mpya sita; Shule ya Sekondari Kimusi, Nyagisya, Barata, Inchugu na Nyanungu pamoja na Kubiterere ili watoto wetu waweze kusoma, na shule hizi zimejengwa na nguvu ya wananchi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ajira mpya hizi ambazo Serikali imetoa, tutaangalia maeneo yenye upungufu ikiwemo shule hizi za Kimusi, Nyagisya, Nyamongo, zilizopo kule Tarime na Mkoa mzima wa Mara kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba tu kumwuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa sababu ni muda mrefu hapo nyuma ajira zilikuwa hazijatoka na kuna vijana wengi waliomaliza elimu zao toka mwaka 2014, 2015 mpaka sasa: Ni nini kauli ya Serikali kwamba baada ya kuwa mmetangaza ajira hizi 13,000 na kuwapa kipaumbele waliokuwa wame-*graduate* mapema zaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tangazo la ajira ambalo Serikali imetoa kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa walimu 13,390 imewekwa pale kwamba wale wa 2015 ndiyo

wataanza kuingia, watakuja wa 2016 wa 2017 ili wasikae muda mrefu baada ya kuwa wamemaliza masomo yao ya ualimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 349

**Kupandisha hadhi Zahanati ya Solwa**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaipandisha hadhi Zahanati ya Solwa kuwa Kituo cha Afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa kufanya ukaguzi na kutoa ushauri wa kitaalamu katika Zahanati ya Solwa ili kuona kama inakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pindi Mkoa utakapojiridhisha na miundombinu iliyopo, watawasilisha ombi hilo Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Afya kwa ajili ya hatua za kuipandisha hadhi Zahanati ya Solwa na kuwa Kituo cha Afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Kwa kutambua kwamba Solwa inahudumia watu karibia 31,000 na imebeba jina la Jimbo la Solwa; napenda kujua, Mganga Mkuu atatumia siku ngapi kumaliza ukaguzi huo? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga na sehemu nyingine wamekuwa wakijitolea kuongeza majengo ya zahanati ili yaweze kuwa vituo vya afya ili kukidhi huduma, sasa napenda kujua, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba zahanati zote ambazo zinakidhi na zimeshaongeza majengo, zitabadilishwa kuwa vituo vya afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ni siku ngapi zitachukuliwa kwa ajili ya ukaguzi huu wa Zahanati ya Solwa ambayo inahudumia watu 31,000 katika Jimbo la Solwa, nitoe agizo kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga kuhakikisha ndani ya mwezi mmoja, taarifa hii iwe imefika Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kuona zahanati hii inaanza mchakato wa kupandishwa hadhi na kuwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali la pili la Mheshimiwa Dkt. Mnzava kwamba wamejenga zahanati nyingi katika maeneo ya kimkakati, ni lengo la Serikali kuhakikisha kwamba zahanati hizi ambazo zimejengwa kwa nguvu ya wananchi kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu ya Tanzania, siyo Shinyanga peke yake kwamba zinapatiwa fedha na kuweza kuwa *upgraded* yale kwa yale

maeneo ya kimkakati, na Serikali itafanya hivyo kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Wananchi wa Kata Kilimilile wamejenga zahanati kwa nguvu ya wananchi na wafadhili na hiyo zahanati ina majengo ya wodi ambazo hazitumiki kwa sababu hadhi ya zahanati hairuhusiwi kulaza wagonjwa: Je, sasa ni lini Zahanati hiyo ya Kata ya Kilimilile itapandishwa hadhi ili iweze kutoa huduma katika Kata za Mabale na Kilimilile kwa wananchi hao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera kufika katika Zahanati ya Kilimilile katika Kata ya Kilimilile kufanya tathmini na kuona yale majengo ambayo yamejengwa kama yanakidhi vigezo vya kuweza kupandisha zahanati hii kuwa kituo cha afya na taarifa hii kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Naye nampatia mwezi mmoja ili iweze kuwa imefanyika tathmini hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kata ya Msaada kuna jengo ambalo lilikuwa likijengwa kwa mpango wa MAMM tangu mwaka 2008 mpaka leo halijakamilika. Naomba kujua, ni lini Serikali itamalizia jengo hilo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monni kuhusu Kata ya Msaada, Serikali itamalizia jengo la Msaada hapa kadri ya upatikanaji wa fedha. Tutaangalia katika mwaka wa fedha huu ambao umeshapitishwa na Bunge lako Tukufu, kuona kama kuna fedha imetengwa kwa ajili ya Msaada lakini kama haipo, basi tutatenga fedha kwenye mwaka wa fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

Na. 350

**Kuongeza posho kwa Madiwani**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaowaongezea posho Madiwani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliongeza posho za Madiwani ambapo mwaka 2012 posho hizo ziliongezwa kutoka shilingi 120,000 hadi shilingi 250,000 kwa mwezi sawa

na ongezeko la asilimia 108.3. Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali ilipandisha tena posho za Madiwani kupitia waraka wa mwaka 2014 kutoka shilingi 250,000 hadi shilingi 350,000 kwa mwezi sawa na ongezeko la asilimia 40 na shilingi 400,000 kwa Meya na Mwenyekiti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kubuni na kuimarisha vyanzo vya mapato pamoja na kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha kwa kutumia mifumo ya kieletroniki ya kukusanya na kutumia fedha katika kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja na matumizi mengineyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nilikuwa nataka niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza; kwa kuwa hawa Madiwani kwa muda mrefu sasa na hasa sisi wa Chama cha Mapinduzi wakati tunapokuwa kwenye kampeni za uchaguzi huwa tunasema kuna mafiga matatu kwa maana ya Madiwani, Wabunge na Rais na wao ndio wanaosimamia miradi ya Serikali. Sasa hatuoni kuna haja kwa kweli ya kuwaongeza kiasi fulani angalau kutoka kwenye eneo walipo ili kufika eneo wanalolitaka wao kwa sababu eneo ni kidogo sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; hawa Madiwani kwa muda mrefu sasa huko nyuma wengi wamechaguliwa na hawapati mafunzo ya Serikali. Lini sasa Serikali itaandaa mafunzo kwa Madiwani ili na wenyewe wawe na uelewa wa kusimamia miradi yetu katika maeneo yetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la kwanza la nyongeza la kuhusu kuongeza posho hizi za Madiwani, Serikali itafanya tathimini na kuangalia ni namna gani hili linaweza likatekelezeka kulingana na bajeti ambayo Serikali inayo. Kwa sbabu haya mambo yanahusisha ongezeko la matumizi kwa Serikali. Tayari kama ambavyo mnafahamu Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani kwamba mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilichukua jukumu kutoka kwenye halmashauri zote la kulipa hizi posho kwa mwezi zilienda Serikali Kuu. Kwa hiyo, tutaliangalia na lenyewe na kuona kama uwezo wa Serikali utauhusu kwenye bajeti zijazo tuweze kulichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye swali la pili la mafunzo kwa Madiwani; hili liko kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zenyewe. Kuna halmashauri ambazo zinatoa maunzo haya kwa kushirikisha Taasisi za *Uongozi Institute*, kwa kushirikisha Taasisi kama Chuo cha Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, niwatake wakurugenzi katika halmashauri mbalimbali nchini kuhakikisha wanatenga bajeti ya kutoa mafunzo kwa Madiwani wa halmashauri zao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Mtega.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa baadhi ya halmashauri malipo au stahiki za Madiwani zinapishana sana mathalani malipo ya simu kwa wenyeviti wa halmashauri na kadhalika, je, nini kauli ya Serikali katika hili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, aina za posho za Madiwani zimeainishwa ambazo ziko wazi. Posho ya kwanza, ni posho ile ya mwezi ambayo nimetoka kuitolea majibu katika swali la msingi. Posho ya pili, ni posho ya madaraka ambayo posho hii pia inatolewa kwa mujibu wa waraka wa viwango vya posho vya Serikali. Posho ya tatu ni posho ya kuhudhuria vikao na posho ya kujikimu na safari mbalimbali za ndani ya halmashauri husika na nje ya halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi posho za ndani zinategemeana na uwezo wa halmashauri husika. Kwa hiyo, hili tutaendelea kuwaasa wakurugenzi wa halmashauri mbalimbali nchini kuangalia walau wanatenga posho ya mawasiliano na kadhalika kulingana na uwezo wa mapato yao wenyewe ya ndani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya watu muhimu sana ni Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa; hawa ni watu ambao wanapata posho kama ni posho inakuwa ni ndogo sana. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha watu hawa ambao ni muhimu wanaongezewa posho kubwa itakayowasaidia utendaji wao wa kazi uwe mzuri katika halmashauri zetu, vitongoji na vijiji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwisha sema hapo

awali kwamba posho hizi zinategemeana na bajeti ya Serikali na uwezo wa makusanyo ya Serikali, lakini upo waraka maalum na Sheria katika Sheria ya Serikali za Mitaa ambayo inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kutenga fedha kwa ajili ya posho za Wenyeviti wa Vitongoiji, Wenyeviti wa Mitaa na Wenyeviti wa Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, nitumie tena nafasi hii mbele ya Bunge hili tukufu kuwataka Wakurugenzi wa Halmashauri kutenga posho hizi za Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa na Wenyeviti wa Vitongoji kwa mujibu wa Sheria ile ya Serikali za Mitaa, Sura 290.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera sasa aulize swali lake. Mheshimiwa nilikuwa nimemruka Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mkwakasaka.

Na. 351

**Hitaji la Vituo vya Afya – Jimbo la Tabora Mjini**

**MHE. VENANT D. PROTAS K.n.y. MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya ukosefu wa Vituo vya Afya katika Jimbo la Tabora Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 Serikali ilitenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Misha. Aidha, ujenzi wa Jengo la *OPD* na Maabara umekamilika na Kituo hicho tayari kimesajiliwa na kimeanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje, ujenzi wa Jengo la wazazi, jengo la upasuaji na jengo la *OPD* lenyewe upo hatua za ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya kwenye maeneo ya kimkakati ikiwemo vituo vya afya katika Jimbo la Tabora Mjini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant Daud, kwa niaba

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Tabora Mjini lina kata za mjini na vijini, lakini licha ya kuwa na Hospitali ya Rufaa ya Kitete na hospitali ya wilaya kumekuwa na mrundikano mkubwa wa wagonjwa. Je, nini mikakati ya Serikali kuzisaidia kata za vijijini kupata vituo vya afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Sera ya Serikali ni kujenga vituo vya afya kwa kila kata lakini mwaka 2021 Waziri wa TAMISEMI, wakati huo Mheshimiwa Ummy Mwalimu alituletea Wabunge kuandika kata za kimakakati ambazo katika Jimbo la Igalula tuliandika Kata ya Goeko, kizengi na Miswaki.

Je, ni lini mtatekeleza yale maagizo ya kata za kimkakati ili tuweze kujenga vituo vya afya na kusogeza huduma za wananchi katika maeneo hayo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali lake la kwanza la utofauti wa Mjini na vijijini katika Jimbo la Tabora Mjini na Serikali kusaidia. Serikali itaendelea kutenga fedha kadri ya bajeti ambavyo inaruhusu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikiwemo Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali la pili la nyongeza la Kata za Goeko, Kizengi na nyinginezo katika Jimbo la Igalula. Serikali itajenga vituo hivi vya afya vya kimkakati kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jimbo la Nkasi Kaskazini lina vituo vya afya vitatu na vinavyofanya kazi ni viwili kati ya kata 17. Ni lini Serikali itajenga vituo 13 vilivyobaki katika Jimbo la Nkasi Kaskazini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeweka kipaumbele katika kuboresha afya za watanzania na tayari Serikali inatenga fedha katika vituo vya afya kwenye kata za kimkakati pote hapa nchini, ikiwemo kata ambazo amezitaja Mheshimiwa Aida Khenani za kule Nkasi ambayo ina vituo vya afya vitatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutangalia katika mwaka wa fedha huu ambao unakwenda kuanza kuutekeleza mwezi Julai, kuona Nkasi imepangiwa vituo vya afya vingapi kwa

ajili ya utekelezaji. Kama bado itakuwa haijapangiwa basi Mheshimiwa Mbunge tutaangalia katika bajeti ya 2024/2025 ili tuweze kuwapangia wana Nkasi kupata huduma bora za afya kupitia vituo vya afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omari Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wananchi wa Wilaya ya Kilindi wanatambua jitihada za Serikali za kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya. Lakini tunazo kata tatu kwenye vituo vya afya vitatu kwenye Kata ya Jaila, Masagalu na kata ya Maswaki tunahitaji *at least* milioni mia, mia ili kuweza kumalziia vituo vya afya. Je, ni lini Serikali italeta fedha katika maeneo hayo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali kujenga vituo vya afya katika Mkakati ikiwemo kata za kwa Mheshimiwa Kigua kule Kilindi Kata hizi za Jaila, Masagalu na Mswaki na tutaangalia katika mwaka wa fedha kama zimetengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi vya afya na umaliziaji. Kama fedha hizo hazijatengwa nimhakikishie Mheshimiwa Kigua katika mwaka wa fedha 2024/2025 ili Jaila, Masagalu na Mswaki ziweze kupata fedha hizi kwa ajili ya umaliziaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kwa majibu hayo. Tunaendela na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 352

**Changamoto mpya za Muungano**

**Mhe. Angelina Adam Malembeka** aliuliza:-

Je, ni changamoto gani mpya za Muungano zimejitokeza?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa hakuna changamoto za Muungano zilizojitokeza. Sote tunafahamu kuwa Muungano wetu umeendelea kuimarika ambapo wananchi wa pande zote mbili wameendelea kunufaika kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya kutokuwa na changamoto mpya ni kutokana na jitihada za serikali zetu mbili za Muungano kuweka Muongozo mzuri wa kushughulikia changamoto kwa haraka zinapojitokeza katika hatua za awali. Lengo la Serikali zote mbili ikiwa ni kuhakikisha changamoto zote zinazopitiwa zinapatiwa ufumbuzi na kuendelea kuimarisha Muungano ili kuepusha changamoto mpya kujitokeza, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Angelina Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKO.:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya kutia moyo lakini pia nimpongeze Rais, Samia na Rais Mwinyi, kwa kutatua kero za Muungano hadi hadi kufikia 22 na kubakia kero nne. Swali langu ni kwamba kuna kauli gani ya Serikali juu ya kutatua hizo kero nne zilizo baki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Serikali imejipanga vipi kwa ajili ya utoaji elimu juu ya suala la Muungano kwa vizazi vijavyo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwanza zinaendeleza ushirikiano ama zitaendeleza ushirikiano wa kuhakikisha kwamba changamoto zote zinazogusa kwenye Muungano zinatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukasema kwamba ili kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto hizi, ziko Kamati ambazo zimeundwa au iko Kamati ya majadiliano ya pamoja ambayo ndio inayosimamia utatuzi wa changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba pamoja na kwamba zipo changamoto zilizobakia lakini kwa kushirikiana na kamati hii tunakwenda kumaliza changamoto zote ili Muungano wetu huu saa uwe imara na uweze kudumu kwa muda mrefu.  Kwa maana kwamba kuna Kamati za wataalam, Kamati za Makatibu Wakuu, Kamati za Mawaziri lakini kuna Kamati za Viongozi wakuu ambao hukaa kwa ajili ya kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nimwambie Mheshimiwa kwamba baada ya kuwa tumetatua

changamoto hizi, kinchofuata sasa ni kuwajulisha na kuwaeleza wananchi hatua tuliyofikia kama Serikali. Tumeanza na vyombo vya habari kuwaelimisha wananchi juu ya changamoto zilizokuwepo na zilizobakia. Kingine tumetoa tovuti maalumu *www.vpo.go.tz* wananchi wakienda hapo wanaweza kuona changamoto zilizotatuliwa na zile ambazo bado hazijatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya makongamano mbalimbali ambayo tumekuwa tukitoa elimu kuhusiana na masuala Muungano, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asya.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa maelezo ya Waziri kwamba hakuna changamoto mpya ni kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za zamani bado hazijakamilika. Ikiwemo hasa changamoto ya bandari na hili suala la bandari limekuwa linaleta kelele nyingi kwa wananchi na limekuwa kero kubwa. Kwa nini Serikali haioni haja ya kulichukulia jambo hili kwa udharura wake na kulitatua haraka iwezekanavyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge. Katika kikao chetu ambacho tulikaa mwezi wa sita tulikubaliana na tulitoa maelekezo. Kwa sababu vikao hivi huwa tunakaa na Wizara za pande zote mbili au pande zote mbili zinagusa Muungano. Tulitoa maelekezo na maelekezo haya yamekwisha anza kufanyiwa kazi kwamba, watu wa *TRA* na wengine wa Bandari wanaohusika waende wakakae washughulikia hili jambo,

tuweze kuambizana zipi zitakuwa zinalipiwa kama sehemu ya changamoto na zipi hazilipiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa kwa kuwa Kamati zinaendelea kukaa, hili jambo tunakwenda kuzimaliza ili kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa Mohammed.

**MHE. KHALIFA MOHAMMED ISSA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto ambazo bado hazijatatuliwa ni upelekaji wa sukari ya Zanzibar katika soko la Tanzania Bara. Ni lini kero hii ambayo ni ya muda mrefu itatatuliwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba moja ya miongoni mwa mambo ambayo Kamati zimo mbioni kuhakikisha kwamba tunaliweka sawa ili kuondosha hii kama ni sehemu ya changamoto ya Muungano ni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili ni jambo ambalo kama tulivyosema hapo awali kwamba jambo hili la utatuzi wa changamoto za Muungano limetengenezewa kamati maalumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe waheshimiwa Wabunge, ikiwa tumeweza kutoka tangu changamoto ya kwanza leo tumezipata changamoto 22 maana yake na hili

kupitia Kamati zinazohusika kwa mujibu wa taratibu zote linakwenda kutatuliwa ili kupunguza changamoto kubwa ambayo inakabili Muungano wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera aulize swali lake.

Na. 353

**Sheria ya Kodi na *VAT* kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo – Zanzibar**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza:-

Je, kwa nini Halmashauri ya Magharibi "A" imeweka Sheria ya Kodi na *VAT* kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Mfuko wa Jimbo hutolewa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Jimbo, Sura 96 ya mwaka 2009. Aidha, fedha hizi zinatumika kwa kuzingatia miongozo, kanuni na taratibu za usimamizi wa fedha za umma. Kila upande wa Serikali zetu mbili una utaratibu wa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itashirikiana na Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzizar kufuatilia utaratibu unaotumika na Halmashauri ya Magharibi "A" kwenye Mfuko wa Jimbo. Aidha, dhamira ya Serikali ni kuendelea kutoa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa pande zote mbili kwa ajili ya kuboresha huduma za jamii na kuwaletea wananchi maendeleo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zahor.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali kwa jibu. Pamoja na kwamba jibu hili limejibiwa kisiasa zaidi kuliko tatizo lilivyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini sasa Serikali au Wizara itakuwa *Serious* Kujibu matatizo yetu ambayo yanaongozwa na Sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; kwa sababu imeonekana Sheria hii inafanya kazi zaidi kwenye upande mmoja lakini kuwaathiri Wabunge wa Majimbo kwa upande wa Zanzibar. Je, Serikali sasa haioni iko haja ya kuwaandikia wenzetu wa Zanzibar ili waache kuvunja Sheria iliyotungwa na Bunge hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira tuko *serious* katika kufanya kazi zetu. Tupo *serious* kufanya kazi zetu kwa mujibu wa sheria na taratibu zote zilizowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inayafnya kazi kwa upande huu wa Mfuko wa Jimbo iko Sheria inayosimamia Mfuko wa Jimbo. Lakini ipo Sheria inaitwa *Zanzibar Revenue Administrative Act*. Sheria ambayo inasimamia na imetoa mamlaka kwa halmashauri na Mabaraza ya Miji kutoza ama

kukata kodi kutokana na sehemu ya fedha zinazoingia kwenye halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko *serious* na kutokana na u-serious tulionao tunakwenda kutatua changamoto zote ambazo zinakabili Mfuko wa Jimbo hasa katika Jimbo la Mwera na maeneo mengine yote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili, nimwambie Mheshimiwa kwamba tuko tayari kama ushauri wake alivyosema kwamba tuandike barua lakini nataka nimfahamishe tunavyo vikao vinavyohusika na kujadili changamoto hizi na majadiliano yote yanayohusiana na Mfuko wa Jimbo. Vikao ambavyo vinaanza katika ngazi nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tayari tumekwishaandaa kikao kazi ambacho tunakwenda kukaa viongozi wa halmashauri zote, viongozi wa mabaraza ya miji, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais ili lengo na madhumuni na Wabunge wote tuweze kuelezana hizi changamoto zinazogusa Mfuko wa Jimbo hasa kwa upande wa Zanzibar.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu Rais Muungano na Mazingira Mheshimiwa Hamza Hamis kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na sasa hakutokuwa na maswali ya nyongeza ya ziada. Mheshimiwa Daniel Tlemai, Mbunge wa Karatu, aulize swali lake; kwa niaba yake Mheshimiwa Zaytun.

Na. 354

**Ujenzi wa barabara ya Matala - Mwanhuzi – Lalago**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa Barabara ya Matala – Mwanhuzi – Lalago kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya barabara ya Matala – Mwanhuzi – Lalago yenye kilometa 148.4 ya kutoka Lalago – Mwanhuzi – Sibiti – Nyahaha imo kwenye mradi wa ujenzi wa Barabara ya Maswa – Lalago - Sibiti River – Haydom – Mbulu – Karatu yenye urefu wa kilometa 339 ambao utatekelezwa kwa utaratibu wa *Engineering, Procurement and Construction plus Financing (EPC+F)* ambao hadi sasa mkandarasi amepatikana na mkataba wa ujenzi utakuwa umesainiwa kabla ya mwishoni mwa mwezi Juni, 2023. Kwa sehemu ya Nyahaha kwenda Matala (kilometa 25) Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Swai kwa niaba ya Mheshimiwa Daniel, Mbunge wa Karatu.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kipande hiki kilichobaki ndio kinaunganisha mkoa wa simiyu na Mkoa wa Arusha na ni muhimu sana katika kufungua uchumi wa wananchi wa Karatu lakini wananchi wa Mkoa wa Arusha kwa ujumla wake.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa kuanza ujenzi wa kipande hiki cha Karatu-Orudeani Matara hadi Lalago kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Swai, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii ya Karatu-Odoyani hadi Mataralalago kujengwa kwa kiwango cha lami. Serikali imekwisha fanya tayari upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, na sasa kazi iliyobaki ni kutafuta fedha ili barabara hii ijengwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fredy Mwakibete, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta Mbunge wa Urambo, sasa aulize swali lake.

Na. 355

**Kuongeza majengo Chuo cha *VETA*-Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza: -

Je, ni lini majengo yataongezwa katika Chuo cha *VETA* Urambo ili kuongeza fani ambazo hazitolewi kwa sasa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Jimbo la Urambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuongeza baadhi ya majengo yanayokosekana katika Chuo cha *VETA* cha Urambo ili kuimarisha uwezo na ufanisi wa kutoa mafunzo kwa wananchi wa Urambo yatakayowawezesha kupata ujuzi na kutekeleza shughuli zao za kiuchumi kwa weledi na viwango stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* imetenga fedha kiasi cha shilingi 880,719,315.39 kwa ajili ya kukiimarisha Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Urambo. Fedha hizi zitatumika katika ujenzi wa miundombinu ya jiko, bwalo la chakula, madarasa na majengo mawili ya karakana. Aidha, ujenzi wa majengo hayo umeanza mwezi Mei, 2023.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, maswali ya nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa mwenyekiti ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Serikali alivyojibu; amejibu vizuri, ahsante.

Swali la kwanza; tuna uhaba wa walimu sita na katibu muhitasi mmoja na uhaba huu unasababisha kwamba mwalimu wa fani moja anapokuwa hayupo hakuna linaloendelea;

Je, Serikali ina mpango gani wa kutuongezea wafanyakazi saba ili shughuli za utoaji wa elimu ya ufundi ziendelee kama zilivyopangwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili jambo muhimu katika mafunzo ya ufundi ni utendaji, yaani *practical* sasa utendaji au elimu kwa vitendo unahitaji sana vifaa;

Je, Serikali yetu imejipangaje kuhusu upatikanaji wa vifaa ili kweli mafunzo ya ufundi ya vitendo yafanyike?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, Serikali ya Awamu ya Sita imejidhatiti kuhakikisha kwamba vyuo hivi ambavyo vilikuwa havina

miundombinu tunaenda kuongezea miundombinu. Na hatukufanya hivi tu kwa chuo hiki cha Urambo peke yake, kuna vyuo kadhaa ambavyo vilikuwa na upungufu wa miundombinu. Tunafahamu upungufu wa miundombinu kwa Mheshimiwa Mwijage kule Muleba, tumeshafanya kazi kule, Mheshimiwa Rais alitoa fedha kwa ajili ya ukarabati pamoja na ujenzi wa miundombinu mingine. Pia kwa Mheshimiwa Dugange kule Wanging'ombe tumefanya hivyo; kwa Mheshimiwa Mtanda Serikali imepeleka fedha vilevile lakini vilevile tumepeleka fedha kule Mikumi kwa Mheshimiwa Londo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hicho tu, katika swali lake la kwanza anataka kufahamu mkakati wa Serikali juu ya walimu. Nimuondoe wasiwasi, Mheshimiwa Rais alitoa kibali cha kuajiri wafanyakazi watumishi wakiwemo na hao walimu 571. Mpaka hivi sasa ninavyozungumza walimu 151 tayari wameshaajiriwa na wameshapelekwa kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo na kwenye baadhi ya hivi vyuo ambavyo vilikuwa tayari vinatoa huduma na vile vyuo vytu 25 vya wilaya na vinne vya mikoa. Kwa hiyo tunaendelea na mchakato huu kwa kukamilisha idadi hii ya waaalimu na watumishi 571 tunaamini na Urambo itafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vifaa naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa na Bunge lako tukufu, tumejidhatiti na kujipanga kwa dhati kabisa kuhakikisha kwamba tunapeleka vifaa kwenye vyuo hhivi vile vya zamani lakini na vile vipya ambavyo tunajenga hivi sasa. Katika bajeti yetu hii inayoendelea tuna *package* ya vifaa lakini vilevile na katika bajeti ambayo tumeanza kuisoma hapa kutakuwa na eneo la fedha ambayo tumetenga kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya vyuo hivi vya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 356

**Kuanzisha masomo ya kuibua vipaji kuanzia shule za msingi**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha masomo yatakayoibua vipaji vya watoto kuanzia shule za msingi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa masomo yanayoibua vipaji vya watoto kuanzia ngazi ya elimu ya msingi. Kwa kuliona hilo Wizara ilianzisha somo la sayansi na teknolojia kuanzia darasa la tatu; stadi za kazi pamoja na sanaa na michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masomo hayo mada mbalimbali zinazochochea vipaji zinafundishwa. Kwa mfano katika somo la stadi za kazi wanafunzi hujifunza muziki, uigizaji, ufinyanzi na ususi. Katika somo la michezo na sanaa wanafunzi hujifunza michezo sahili, michezo ya jadi, riadha na mpira. Aidha kwa upande wa somo la sayansi na teknolojia wanafunzi hujifunza matumizi ya nishati, majaribio ya kisayansi, mashine na kazi na kuelea na kuzama kwa vitu.

Aidha, Wizara imetoa mwongozo wa ubainishaji na utambuzi wa wanafunzi wenye vipawa na vipaji wa mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali kwa sasa inaendelea na mapitio ya mitaala ikiwemo Mtaala wa Elimu ya Msingi ambapo ushauri wa Mheshimiwa Mbunge utazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka swali la nyongeza

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka hapo awali tulikuwa na shule ambazo zilikuwa za wananfunzi wenye vipaji maalumu. Shule hizo zilikuwa Kilakala, Loreza, Tabora *Boys*, Mzumbe, Iliboru na kadhalika lakini hadi sasa hivi hatuzisikii hizo shule zikizungumziwa au tukipata taarifa kwamba *performance* yake ya vile vipaji vyao maalum vimetumikaje.

Je, Serikali ina mpango gani basi kuziimarisha hizo shule ilikusudi tuone kwamba huu mtaala ambao unatengenezwa sasa hivi wa mali utaweza pia kuwa na tija katika shule hizi maalum?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; tumeona nchi za wenzetu kama Japan na Uchina wanatilia sana mkazo kwenye kazi za stadi, na matokeo yake ni kwamba zile kazi zinazotengenezwa na wanafunzi zinauzwa wakati wakifanya mahafali ya shule na kuwaalika wazazi ili kusudi wanafunzi wale wapate morali kwamba kweli vile wanavyotengeneza vina maana na wawanye wengine wa

shule nyingine wapate moyo kwamba kumbe hizi shule za ufundi zina maana.

Je, Serikali ina mpango gani pia kuanzisha utaratibu ambao hivi vifaa vinavyotengenezwa na wanafunzi hawa wanaokwenda kwenye hizi shule za amali zitakuwa zenye thamani ya kuweza kuuzika ili ziongeze kipato kwenye shule hizi wanazofanyia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kaboyoka, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alichozungumza Mheshimiwa Mbunge. Nimuondoe wasiwasi, shule hizi bado zipo. Kwa upande wa wasichana ni kama alivyozitaja; tuna Shule ya Msalato hapa Dodoma tuna Kilakala ambayo ipo Morogoro. Pia tuna *Tabora Girls* ambayo ipo kule Tabora. Kwa upande wa wavulana tuna shule ya Kibaha Sekondari, tuna Mzumbe, tuna Ilboru pamoja *Tabora Boys.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani jambo kubwa alilolizungumza ni kwamba hazisikiki. Tunaomba tuchukue ushauri wa Mheshimiwa Mbunge twende tukaimarishe ufundishaji. Hizi ni shule zetu ambazo tunasema ni maalum kabisa kwa ajili ya kupokea watoto wenye vipaji na vipawa mbalimbali. Tunaendelea kuzihudumia na kuziimarisha, lakini tunaomba tuchukue fursa hii, tubebe ushauri wako ili twende tukaziimarishe zaidi ili ziweze kujitangaza kama ilivyokuwa zamani, zilikuwa zinavuma sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili amezingumzia suala la zile *study* mbalimbali. Kwa vile tumesema kwamba sasa hivi tunafanya mapitio ya mitaala, mapitio ya mitaala hii itakwenda kuongeza baadhi ya

masomo ambayo yatakwenda kufundisha sanasana stadi mbalimbali hasa kwenye *skills*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia suala la kuongeza ubora wa vile vitu ambavyo vitakuwa vinazalishwa ili viende vikapate soko, kwa maana ya tuvibiasharishe iwe kama kitega uchumi cha chuo. Tunaomba tubebe ushauri huo; na kwa vile tunapitia mitaala tutakwenda kuchopeka baadhi ya kozi ambazo tutakwenda kuzungumza au tutakwenda kushughulikia zaidi zile *study* za mikono na kazi za mikono ambazo tutakwenda kuzipeleka sokoni kwa ajili ya kukuza na kuongea vipato na iwe kama miradi kwenye shule zetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi Mbunge wa Malinyi, aulize swali lake.

Na. 357

**Hitaji la mawasiliano ya simu Malinyi**

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza: -

Je, ni lini serikali kupitia *UCSAF* itapeleka minara ya mawasiliano Wilaya ya Malinyi kwa kuwa maeneo mengi ya wilaya hiyo hayana usikivu wa mawasiliano na *data?*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari napenda kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Jimbo la Malinyi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka wa fedha 2015/2016 na 2020/2021 Kata za Biro, Sofi, Ngoheranga na eneo ilipo Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi zimenufaika na Miradi ya huduma za mawasiliano ya simu kupitia ruzuku ya Serikali. Aidha, ujenzi wa minara katika Kata ya Ngoheranga na eneo ilipo ofisi ya Mkurugenzi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia mradi wa Tanzania ya kidigitali imeainisha Kata za Igawa na Njiwa ambazo tayari zimepata mtoa huduma wa kuzifikishia huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa minara hii ikikamilika itatoa huduma za mawasiliano katika teknolojia ya *3G* na *4G*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Antipas.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, mpaka hivi ninavyozungumza Ofisi ya Halmashauri ya Malinyi bado hakuna mawasiliano na mkandarasi hajafika *site*. Hata hivyo ninafahamu kwamba mfuko wa mawasiliano kwa hiyo *(UCSAF)* walishatoa fedha ila *TTCL* ambao walipewa kazi hawajafanya mpaka sasa hivi;

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kuambatana na mimi *weekend* hii wewe au Mkurugenzi wa *TTCL* na *UCSAF* kwenda Malinyi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sehemu kubwa ya Jimbo la Malinyi hasa Kata ya Usangule, Sofi na Itete kwenye vijiji kama Dabadaba hakuna mawasiliano kabisa.

Je, ni lini Serikali itamaliza changamoto hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Antipas, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali iliingia mkataba wa bilioni 10.88 na Shirika la Mawasiliano Tanzania *TTCL,* ambapo katika fedha hizo zingine zinaenda katika Halmashauri ya Malinyi ambayo ni milioni 320 kwa ajili ya kujenga mnara wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kutoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano *TTCL* kuhakikisha kwamba, pamoja na Halmashauri ya Malinyi na halmashauri nyingine zote 33 ambazo tumeingia nao mkataba wahakikishe wanakamilisha miradi hii ndani ya wakati, kwani kwa kufanya hivyo tutawarahisishia halmashauri kukusanya mapato na vilevile wananchi wataweza kupata huduma ya mawasiliano bila kuwa na changamoto yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kipengele cha pili, kata ambazo Mheshimiwa amezitaja mimi nilifanya ziara na yeye tukiwa pamoja katika jimbo lake; Kata ya Itete katika eneo linaitwa Madabadaba na Usangule, Kilosa Mpepo, yote hayo yameepata watoa huduma katika mradi wetu wa Tanzania ya kidigitali. Kwa hiyo tunaamini kwamba kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambayo ameyatoa ni kwamba ni lazima mikataba hii ikatelezwe ndani ya muda ambao

tumekubaliana. Kwa hiyo tunaamini kwamba ndani ya miezi tisa mkataba huu ukikamilika wananchi wa eneo la Malinyi watapata huduma ya mawasiliano.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Andrea Mathew Kundo, kwa majibu hayo ya Ofisi ya Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, sasa aulize swali lake.

Na. 358

**Mpango wa kufufua zao la kahawa Wilayani Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua zao la kahawa Wilayani Lushoto?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya waziri wa kilimo ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaban Omari Shekilindi Mbunge wa Lushoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanzisha kitalu cha miche ya kahawa katika eneo la Jegestal ili kuwezesha upatikanaji wa miche kwa wakulima wa kahawa Wilayani Lushoto. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 jumla ya miche 227,905 imezalishwa na imeanza kusambazwa kwa wakulima mwezi Mei, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania imekiwezesha Chama Kikuu

cha Ushirika cha Usambara kuingia mkataba na Kampuni ya *Mambo Coffee Company Ltd* na kupata cheti cha kilimo hai *(Organic Certification)* kitakachowezesha chama hicho kuuza kahawa yake kwenye soko maalum. Hatua hizo ni sehemu ya jitihada za Serikali za kufufua na kuendeleza kilimo cha zao la kahawa katika Wilaya ya Lushoto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabani Omary Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Ni kweli kitalu kiko tayari na wakulima wanaendelea kupata miche ya kahawa. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa zao la kahawa ni zao ambalo linaingiza fedha nyingi za kigeni:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha zaidi zao hili la kahawa hapa nchini?

(b) Je, ni lini Serikali itaruhusu bei ya zao la kahawa kuamuriwa na nguvu ya soko?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la kwanza la kuboresha na kuhakikisha kwamba tunatafuta masoko ya uhakika. Ni dhamira ya serikali ya awamu ya sita kuhakikisha kwamba zao la kahawa linaendelea kuwa na mchango mkubwa katika kuingiza fedha za kigeni na kubadilisha maisha ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunaendelea na kuitangaza kahawa yetu nje ya mipaka ya Tanzania kwa sababu wanunuzi wakubwa wanatoka nje ya mipaka ya Tanzania. Tunashirikiana na Balozi zetu mbalimbali na kupitia matamasha na maonesho mbalimbali tumekuwa tukiitangaza kahawa yetu na jambo hili limetuletea tija kubwa sana. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu wezeshi ili zao hili liweze kupata soko la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili la kuhusu bei ya kahawa kuamuliwa na nguvu na soko. Mwenendo wa masoko rejea ya kahawa duniani ndiyo ambayo huwa yanaamua bei ya kahawa. Masoko haya ni masoko ya New York kwa kahawa ya *arabika* na *Eurone*x Uingereza kwa ajili ya *robusta*. Sisi kama Serikali tumehakikisha kwamba mara zote tunahakikisha wakulima wetu kupitia taarifa hizi wanapata taarifa sahihi na mwisho wa siku waweze kupata bei ambayo itamnufaisha. Kwa hiyo kama Serikali tumeacha nguvu hiyo ya soko iamue, lakini tunawasaidia wakulima wetu kuzalisha kahawa bora ambayo itasaidia pia kuongeza tija katika Soko hilo la Kimataifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri Wizara ya Kilimo kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, Mbunge wa Chwaka, aulize swali lake.

Na. 359

**Warithi wa Askari E2152 kulipwa mafao yao**

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE** aliuliza:-

Je, lini warithi wa Askari E2152 aliyekuwa mtumishi wa Jeshi la Polisi watapewa mafao yao?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimwa Haji Makame Mlenge, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafao ya warithi wa Askari Polisi E.2152 *PC* Makame Haji Kheir yameshashughulikiwa na Kamisheni ya Polisi Zanzibar, pamoja na Kamisheni ya Utawala wa Jeshi la Polisi, Makao Makuu Dodoma. Mnamo tarehe 8 Machi, 2023, maombi hayo yaliwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango baada ya kukamilika kwa nyaraka zote muhimu zilizokuwa zikihitajika kwa ajili ya malipo ambapo taratibu za uandaaji wa malipo hayo zinaendelea na yanatarajiwa kukamilika ndani ya Mwezi huu Mei ambapo warithi wa Askari huyo watalipwa stahiki zao kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, swali la nyongeza.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali kwa kufikia hatua hii ya kusema Mei, mwezi huu watalipwa warithi wa Marehemu Makame Haji Kheir aliyefariki toka mwaka 2003 lakini kwa sababu ni muda sasa na mwezi Mei ukiisha hajalipwa, ikifika mwezi Agosti nitauliza tena swali hili ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msingi, kwa kuwa tatizo hili naamini kwamba liko kwa wingi sana Nchini Tanzania. Je, Serikali ina mkakati gani au inawaambia nini Watanzania wenye tatizo kama hili la mirathi ambao hawajalipwa mpaka leo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YANDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ambayo tumempa Mheshimiwa Mlenge ndio majibu ambayo tunakwenda kuyafanyia kazi. Kwa maana ya kwamba huu mwezi Mei huyu mtu ambaye anadai mafao yake kupitia warithi, atapata mafao yake kwa sababu kila kitu kipo na vielelezo vimekamilika na fedha zimeshatengwa na zipo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto pamoja na kwamba tunachowaambia Watanzania kwamba madai yote na hiki tunataka tuwaambie, itakapofika Oktoba mwaka huu tutahakikisha kwamba warithi wote wameshapatiwa mafao yao ili lengo na madhumuni sasa changamoto hizi zisiendelee kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyojitokeza na ndiyo maana tunachukua muda mrefu halafu wananchi wanailaumu Serikali ni kwa sababu ya kuchelewa kuleta vielelezo vitakavyotupa sisi uhalali wa kuweza kuwapatia wananchi ile stahiki. Kwa hiyo niwaombe tu wananchi kwamba likishatokea hili walete vielelezo haraka iwezekanavyo ili na sisi tuweze kuwafanyia haraka waweze kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Swali la Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke litauliza kwa niaba na Mheshimiwa Janejelly James.

Na. 360

**Tamko kuhusu Kitambulisho cha Taifa kuwekwa ukomo wa kutumika**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE K.n.y. MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza:-

Je, nini tamko la Serikali kuhusu Kitambulisho cha Taifa kuwekwa ukomo wa kutumika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vitambulisho vya Taifa vilivyotolewa hadi mwaka 2022 vilikuwa na tarehe ya ukomo wa kutumika. Serikali imefanya marekebisho ya Kanuni za Usajili na Utambuzi wa Watu za mwaka 2014 ikiwemo Kanuni ya 7(3)(a) ambayo inaainisha taarifa zilizopo katika uso wa Kitambulisho cha Taifa zinazohusiana na tarehe ya ukomo wa muda wa matumizi ya Kitambulisho cha Taifa. Ili kuondoa ukomo wa matumizi, marekebisho hayo yalitangazwa rasmi katika Tangazo la Serikali *(GN)* Na. 96 la tarehe 17 Februari, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kwamba, Vitambulisho vya Taifa kwa raia ili kuwezesha Vitambulisho

vinavyofikia ukomo wake baada ya kipindi cha miaka kumi vitaendelea kutumika baada ya muda huo. Napenda kufafanua zaidi kwamba Namba za Utambulisho *(NIN)* zilizopo katika vitambulisho hivyo, hazina ukomo wa muda wa matumizi. Aidha, marekebisho hayo hayatahusu muda wa matumizi ya Vitambulisho vya Taifa kwa Wageni Wakaazi *(Legal Residents)* na Wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa watoa huduma wanaotumia vitambulisho vya Taifa kuwatambua wateja wao, kuendelea kutambua vitambulisho vyenye tarehe za ukomo, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janejelly James.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, wale ambao walipewa namba za *NIDA* kabla ya tarehe ya *GN* Namba 96 ya Mwaka 2023, vitambulisho vyao vitatoka vikiwa na ukomo au vitakuwa havina ukomo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali imejipangaje kuleta uelewa kwa wananchi ili wajue kwamba vitambulisho vyao ambavyo vimekaribia kuwa na ukomo na ambavyo vina ukomo havitawaathiri ili kupunguza taharuki iliyo kwa wananchi sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho ambavyo vitakuja baada ya tangazo hili havitakuwa na ukomo lakini

hata vile vitambulisho ambavyo vimekuja kabla ya tangazo wataendelea. Kwa sababu lengo la Serikali hii ni kuhakikisha kwamba vitambulisho haviwezi kuwafanya watu wakakosa huduma zao muhimu. Kwa hiyo ndio maana tukasema kwamba vitambulisho ambavyo vitakuja baada ya tangazo hili havitakuwa na ukomo, lakini hata vile ambavyo tunasema vimeshakwisha muda navyo vilevile vitaendelea kutumika kuwapatia wananchi huduma mpaka pale Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itakapotoa maelekezo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipi wananchi watafikiwa na taaluma hiyo. Kwanza kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Waziri ameshatoa tangazo kupitia vyombo vya habari kama vile televisheni, redio na magazeti. Nadhani wengi ambao wanakwenda kwenye mitandao huko wameona, lakini kikubwa tumeshatoa maelekezo na tupo tayari muda wowote tunaweza tukaanza mafunzo kwa watendaji wote wa *NIDA* kuwapa maelekezo na mafunzo ili sasa waanze kuwafundisha wananchi ili wananchi waweze kujua huu mchanganuo wa kipi kimekwisha ukomo na kipi hakitakwisha ukomo na kipi kitatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hamza Khamisi kwa majibu hayo ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Waheshimiwa Wabunge, Wizara yetu ya mwisho kwa leo ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 361

**Wataalam wa maendeleo ya jamii kuwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawahamisha wataalam wa maendeleo ya jamii kuwa chini ya Wizara?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Dkt. Dorothy Gwajima.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inatekeleza Tamko la Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwa wananchi kwa kushusha madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kusogeza huduma na utalaam karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kufuatia kuundwa kwa Wizara hii ya Maendeleleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambapo kada za msingi za kitaalam ni Maafisa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii, Serikali inaendelea na hatua za kuimarisha mifumo ya uratibu ngazi ya Sekratarieti ya Mikoa na Halmashauri ili kujibu mahitaji ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii mpya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini hata hivyo swali hili naona halipaswi kujibiwa na Wizara hii. lakini nitauliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa kuna baadhi ya Wizara kama vile Wizara ya Ardhi na Wizara ya Afya imeweza kuhamisha wataalam wa kada zinazoendana na Wizara zile kutoka halmashauri kwenda kwenye Wizara mama zao. Je, Serikali haioni haja sasa ya kufanya tathmini ya kina ya Sera hii ya Ugatuaji ili kuendana na mahitaji halisi ya sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu namba mbili; kwa kuwa sasa kumekuwa na wimbi kubwa la upotofu wa maadili nchini, kama vile ukatili wa watoto na wanawake. Je, Serikali haioni haja katika Ofisi ya Sekretarieti ya Mkoa *(RAS)* kuwepo na *RAS* Msaidizi kwa ajili ya maendeleo ya jamii? Kwa sababu mpaka sasa hivi ofisi zote za mkoa hakuna *RAS* Mmsaidizi kwa ajili ya *issues* za maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu langu la msingi kama nilivyosema kwamba Serikali sasa baada ya kuundwa kwa Wizara hii mpya inaendelea kuangalia utaratibu gani mzuri utaweza kuimarisha uratibu au mfumo wa ngazi ya mkoa mpaka kwenda kwenye halmashauri ili Wizara hii ambayo sasa hivi inakabiliwa na changamoto nyingi za kijamii iweze kufanya kazi kwa uharaka na ufanisi kwa kuwatumia wale wataalam wake. Hivyo basi niseme kwamba nimepokea mchango wake na tunapoendelea na majadiliano haya ya kuimarisha hii mifumo tutawasilisha ili Serikali kwa ukubwa wake na upana wake iweze kuangalia.

Lengo letu ni kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa kule na wataalam hawa ziko vizuri wakati wote na za haraka na jamii inabadilishwa fikra zao ili kupokea maelekezo na matakwa ya utekelezaji wa sera zingine zote. Naweza nikaweka hivi kwa ujumla wake.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali ndio umefikia ukomo wake na sasa ni matangazo, nitaanza na matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii:-

Kuna wageni ambao wapo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, wageni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia; kuna Mheshimiwa Khamis Maiga, Mkuu wa Wilaya ya Rombo; Ndugu Antony Tesha, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Rombo; Ndugu Mary Sulley, Katibu wa CCM Wilaya ya Rombo; Ndugu Gilbert Tarimo, Mwenyekiti wa Halmashauri Rombo. Pia kuna Ndugu Mboka Mwanitu, Mkurugenzi kutoka *World Food Program,* Dodoma, karibuni sana wageni wetu ambao mpo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni nane wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza, ambao ni wadau wa elimu kutoka Mikoa mbalimbali ya Tanzania. Wageni wa Mheshimiwa Rweikiza, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Khalifa Salum Suleiman ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Tunguu, Kusini Zanzibar, karibuni sana Madiwani kutoka Kusini Zanzibar. *(Makofi)*

Tuna wageni tisa wa Mheshimiwa Hassan Mtenga, viongozi wa Chama cha Wazalishaji Chumvi kutoka Mikoa ya

Mtwara, Tanga na Lindi, karibuni sana wageni wetu kutoka Mtwara, Tanga na Lindi. *(Makofi)*

Pia tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 116 wa darasa la nne na walimu sita kutoka Shule ya Msingi *Saint Gaspar* ya Jijini Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wanafunzi 35 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wanachama 26 kutoka *Muungano Jogging Sports Club* ya Jijini Dodoma, karibuni sana wanachama hao. *(Makofi)*

Wanafunzi 100 kutoka Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi, Tawi la Chuo Kikuu cha Jordan cha Mkoa wa Morogoro, karibuni sana Umoja huo wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi kutoka huko Jordan, Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia kuna tangazo hapa ambalo mnaomba mkumbushwe kwamba Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itaendesha semina kuhusu utendaji wa kazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzani *(TPA)* ambapo semina hiyo itafanyika leo siku ja Jumatano tarehe 17 Mei, 2023, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribisha kuhudhuria semina hii muhimu.

Katibu tuendelee.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko na Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi wajiandae.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukrani nyingi sana kwa kupewa nafasi hii ya kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Elimu, Profesa Adolf Mkenda, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa hotuba nzuri ya bajeti ya suala ambalo ni muhimu sana ambalo ni elimu na maarifa, sayansi na teknolojia kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuliendeleza gurudumu hili la mapitio ya uboreshaji wa Sera ya Elimu na Mitaala katika nchi yetu. Serikali ya Awamu ya Sita imefanya jambo kubwa sana kukamilisha sera hii na sasa kuileta kwa wananchi ili wananchi waweze kuijadili na kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu ni muhimu sana. Serikali ya Awamu ya Sita na zilizopita zimewekeza sana katika miundombinu *(hardware)*. Yawe ni majengo, ziwe ni maabara na sasa inajikita katika eneo muhimu sana la

kuwekeza katika *software* na *software* ya elimu ni sera na mitaala. Hili ni zoezi muhimu na ni vyema niiombe Wizara makongamano na mijadala hii ambayo tumeiona iendelee katika maeneo mbalimbali ya Tanzania ili wananchi watoe maoni yao katika jambo hili muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo napongeza sana katika mwelekeo mpya wa sera ni sasa kuitoa elimu ya lazima kutoka darasa la saba na sasa kwenda kidato cha nne. Takribani sasa miaka 58 toka elimu ya lazima ilipotolewa darasa la nne kwenda darasa la saba na maamuzi yale ya kijasiri yaliyofanywa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1968 kutoa elimu ya lazima toka darasa la nne kwenda darasa la saba. Katika kipindi cha mpito kuanzisha shule ambazo ziliitwa *extended primary school,* yaani zile shule za darasa la nne zikaongezewa darasa la tano, la sita na la saba na wale wanafunzi walipofika darasa la saba wakafanya mtihani mmoja na wanafunzi wa darasa la nane *middle school* na ndiyo ikawa mwisho wa *middle school.* Kwa hiyo mambo haya yanayofanyika ni mambo makubwa takribani miaka 58 baada ya kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naunga mkono suala la kuwa na elimu ya msingi ya miaka sita ikifuatiwa na elimu ya sekondari ya miaka minne. Jambo hili pia siyo jipya sana, wale waliosoma miaka ya 1920, 1930 na 1940 palikuwa na aina mbili ya shule wakati ule, mmoja wa hao waliosoma ni Baba yangu. Palikuwa na *District Schools* na kwenye *District Schools* wanafunzi walisoma darasa la kwanza mpaka darasa la sita na baada ya hapo wakaenda kwenye *central schools.* Kwenye *central schools* walisoma miaka miwili, darasa la saba na la nane na baadaye wengine walikwenda kwenye taaluma kama vile Ualimu kwa miaka mitatu na wengine waliendelea darasa la tisa na darasa la kumi ili kupata sifa ya kwenda kusoma *diploma* ya elimu Makerere. Tutakapopata

muda wa kuchangia haya tutayachangia zaidi ili kuzidi kuboresha hili jambo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba nichangie katika maeneo mawili au matatu kama muda utaruhusu. Eneo la kwanza ni *FDC,* Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na eneo la pili elimu ya watu wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katikati palitokea upotoshaji kwamba Vyuo vya Wananchi - *FDC* ni vyuo vya CCM, siyo kweli. Vyuo vya Wananchi -*FDC* vilivyoanzishwa mwaka 1975 vilikuwa ni wazo la Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere baada ya kutembelea nchi za *Nordic* na hasa Sweden alipokuta kule wana aina hii ya vyuo na vyuo hivyo ndiyo vikaanzishwa mwaka 1975 na kwa miaka mingi sana vilikuwa vina hisaniwa na Shirika la Fedha la *SIDA* la Sweden na lilipojitoa watu waliona labda vyuo hivi vitakufa lakini nashukuru vinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wizara ya Elimu sasa iwekeze kwa kiasi kikubwa sana katika hivi Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na ikiwezekana Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi viwe katika kila Kata ya nchi yetu. Kwanini nasema hivyo? Bado tuna kundi kubwa la wanafunzi waliomaliza darasa la saba hawakufaulu kwenda sekondari. Bado tuna kundi tena la wanafunzi waliomaliza Kidato cha Nne lakini hawakufanikiwa kupata taaluma. Pia tuna kundi la wanafunzi ambao wamesomea fani mbalimbali hata Vyuo Vikuu lakini hawana cha kufanya katika maeneo wanayoishi kutokana na kukosa stadi mbalimbali katika kilimo, ufugaji, ujasiriamali na ili waweze kujitegemea ninaona vyuo vya kufanya kazi hiyo ni Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mabadiliko haya ya Sera na Mitaala, kijana atakayemaliza Kidato cha Nne na sasa anaamua haendelei anakwenda kijijini au anakwenda

kujiajiri bado atahitaji kuwa na mafunzo ya *orientation*. Mafunzo ya kumuandaa kwenda kwenye jamii, mafunzo ya kumuandaa kwenda kufanya anachokitaka kukifanya na chuo cha kufanya kazi hiyo mimi naona ni Chuo cha Maendeleo ya Wananchi - *FDC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wale ambao tayari watakuwa wamejiajiri wana fani mbalimbali, wana taaluma mbalimbali, wana kazi mbalimbali, kila mara watahitaji kupata mafunzo ya maeneo mapya yanayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliusikiliza kwa makini sana mchango wa Mheshimiwa Jumanne Kishimba katika kongamano lile la sera mpya ya elimu na mitaala mipya ya elimu. Alipoeleza kwamba leo kuna uhitaji mkubwa sana wa mafundi wa simu, leo kuna uhitaji mkubwa sana wa mafundi wa pikipiki. Sasa ili kufanya mambo haya hatuwezi kuitegemea *VETA* ifanye hivyo. Mimi naona vyuo vya kufanya kazi hiyo vitakuwa ni Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa sababu vyenyewe vinaweza kuwa na mafunzo ya muda mfupi lakini pia kuwa na mafunzo ya *outreach program* kuwafikia vijana na kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuweke umuhimu sana katika vyuo hivi na sasa tuwekeze zaidi, na mimi niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutoa shilingi 645,764,808 kukarabati Chuo cha Kilosa cha Maendeleo ya Wananchi pale Ilonga. Chuo kile sasa kina mandhari nzuri, kina kazi nzuri lakini kinapungukiwa na vifaa, kinapungukiwa pia na wakufunzi. Kwenye suala la wakufunzi ningependa katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi tuwe na aina mbili ya wakufunzi. Tuwe na wakufunzi wa kudumu ambao ni *permanent* lakini pia tuwe na wakufunzi wa kujitoela katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili nalitilia umuhimu sana kwa sababu nchi hii inahitaji aina hii ya vyuo ili

kuwawezesha vijana wetu na wananchi wote kila wakati kunoa maendeleo yao na kuendelea kuwa muhimu katika jamii zao. Kwa hiyo, tuviongezee fedha vyuo hivi. Tuviongezee rasilimali vyuo hivi, tuviongezee wataalam vyuo hivi, lakini ningependa pia nimuombe Waziri wa Elimu, suala hili la *FDC* sasa pia liingie ndani ya sera ya elimu ambayo tunaifanyia mapitio na maboresho sasa ili iwe ni sehemu ya mfumo wa elimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ningependa kulichangia ni elimu ya watu wazima. Mara baada ya kupata uhuru, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitangaza maadui watatu ambao ni ujinga, umaskini na maradhi. Kwenye ujinga tulikuja na suala la elimu ya watu wazima na tumefanya vizuri sana, mkazo wa elimu ya watu wazima wakati ule ilikuwa ni katika eneo la kusoma, kuandika na kuhesabu. Katika kusoma, kuandika na kuhesabu tumefanya jitihada kubwa sana lakini wakati umefika sasa na hili pia ningependa liingie katika sera ya elimu, tuje na mtazamo mpya kuhusu elimu ya watu wazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya watu wazima siyo tu kwa wale ambao hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu. Elimu ya watu wazima inahitajika na watu wote hata wenye *Phd* kama mimi. Hata mimi pia nahitaji elimu ya watu wazima, maana yake tuwe na mtazamo mpya sasa wa elimu ya watu wazima ambayo itawagusa watu wote wa rika zote, wa elimu zote, wa mahitaji yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kutokana na uzoefu. Katika miaka ya 1990 na miaka ya mwanzo ya 2000 ilionekana kuna umuhimu sasa wa kutunga Sheria za Mazingira na kuwafanya Majaji na Mahakimu wetu wazimudu sheria mpya za mazingira na wawe na elimu ya mazingira, mimi ni mmoja wa watu ambao Umoja wa Mataifa ulinichukua niwe mmoja wa wataalam waelekezi wa

kuandaa mitaala ya kuwasaidia Majaji na Mahakimu kujua elimu ya watu wazima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya jambo hilo niliona umuhimu wa kujifunza elimu ya watu wazima kwa ngazi zote. Kwa hiyo, nisisitize sana umuhimu wa elimu ya watu wazima katika nyanja zote na sera iliangalie hilo katika upana wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mengine ya kuchangia katika suala la sayansi na teknolojia, tuwekeze katika maeneo mapya lakini hilo nitatoa mchango wangu kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikujua kwamba muda ni mfupi lakini nashukuru sana. Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Elimu ya Watu Wazima iingie katika sera ya sasa ya elimu ili tuweze kusonga mbele kama Taifa jipya linalojitambu na kujifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, pamoja na wageni ambao niliwataja wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda Waziri wetu wa Elimu pia tuna Wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Rombo. Naomba tutambue uwepo wao. Karibuni sana Wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Rombo, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi na Mheshimiwa Injinia Dkt. Leonard Chamuriho wajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa na mimi kuweka mchango

wangu kwenye bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu naomba nitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali. Kuipongeza Serikali kwa sababu yapo mambo mengi ambayo tumekuwa tukisimama mbele ya Bunge lako Tukufu tunashauri Serikali namna ya kuboresha elimu ya Tanzania, tumeshuhudia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini tumeshuhudia kwenye mijadala mbalimbali ya Mheshimiwa Waziri na Kamati ya Kudumu ya Bunge, yameendelea kutekelezwa na yanaonesha kuleta tija kubwa katika mabadiliko ya elimu nchini, ninapongeza sana kwa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi, binafsi tangu nimeingia kwenye Bunge hili pamekuwa na mjadala mkubwa wa uhitaji wa mabadiliko ya elimu Tanzania. Watu wamekuwa na kiu ya kuona elimu ya Tanzania inatolewa kwa kuleta mabadiliko ya mtu mmoja mmoja baada ya kuhitimu. Tumekuwa na uhitaji wa kushuhudia elimu ya Tanzania inamsaidia kijana wa Tanzania kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mkakati huu wa kutekeleza maombi na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge hili kwa kuamua kuleta mtaala mpya wa elimu, hii ni dhahiri kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu, ni dhahiri kwamba Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeamua kusikiliza mawazo na kutekeleza kadri ambavyo imeweza. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hili la kubadilisha mitaala liliafikiwa na Rais wetu kipenzi, Mama Samia Suluhu Hassan na alilitolea maelekezo Madhubuti, na yeye kama Mama, kama Kiongozi alishagundua yapo maeneo ambayo yana mapungufu na yanahitaji kufanyiwa kazi ili elimu yetu iweze kuwa bora. Mimi nataka niseme pamoja na mambo

mengi mazuri ambayo yamewekwa kwenye mitaala mipya, lakini jambo la kuweka *internship* kwa walimu, jambo la kuhakikisha kwamba mwalimu kabla hajaajiriwa anajitolea kwa mwaka mzima kwenda kufanya *internship* kazini kuimarisha ujuzi wake, ni jambo kubwa ni mabadiliko makubwa na ni jambo ambalo litaboresha sana elimu ya Tanzania. Niendelee kupongeza kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze kuchangia. Kama mtakumbuka vizuri kwenye mchango wangu juu ya Wizara, wakati nachangia Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, niliishauri na niliiomba Serikali ije na mkakati wa maksudi wa kupunguza upungufu wa walimu kwenye mashule yetu. Nilikuja na takwimu, nilionyesha namna ambavyo kuna pengo kubwa kutoka kwa walimu wanaohitimu, walimu walioko mtaani na walimu ambao wanaajiriwa kila mwaka, nikashauri kwamba inawezekana kupunguza hili wimbi au pengo la upungufu wa walimu mashuleni kwa kutengeneza utaratibu wa kuajiri kwa mkataba au kuajiri kwa muda, kuleta ajira za muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge litakuwa limerekodi kwenye *Hansard*. Majibu yaliyotolewa na Serikali ilikuwa ni kwamba Serikali haina mwongozo, hakuna utaratibu wa walimu kujitolea lakini walimu wengi wapo mashuleni wanajitolea, nataka niseme jambo moja, tunapozungumza sasa katika ngazi ya awali tunahitaji kuwa na walimu 61,487. Walimu waliopo mashuleni ni 8,619, upungufu wa walimu kwa ngazi ya awali pekeyake ni walimu 52,868. Huu upungufu ni mkubwa sana, upungufu ni mkubwa lakini walimu wapo mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda sekondari vivyo hivyo, tuna uhitaji wa walimu laki tatu na zaidi lakini walimu walioko shuleni ni laki moja na kidogo. Kwa hiyo tuna upungufu wa zaidi ya walimu 100,000. Ukienda kwenye shule za msingi ni

hivyo hivyo na inapelekea kama nchi sasa kuwa na zaidi ya upungufu wa walimu 300,000 kwenye mashule yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nilizonazo Mama yetu, kipenzi chetu Mheshimiwa Rais ametangaza ajira za walimu hivi karibuni. Ajira ni kama 29,000 kama nakumbuka vizuri lakini walioomba ni zaidi ya walimu 300,000. *Imagine* tatizo ni kubwa namna gani? Tunawezaje kwenda kulitatua tatizo hili kwa kufikiria kwamba hatuwezi kuwa-*consider* wale ambao wanajitolea kwa sababu hatuna mwongozo. Hii siyo sawa na hii siyo sahihi. Niendelee kusisitiza na kuiomba Serikali tuleteeni mwongozo, walimu waliohitimu vyuo vya ualimu wapate nafasi ya kwenda kujitolea. Wanapojitolea mambo mawili yanatokea kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni wao kuimarisha ujuzi wao na kujikumbushia yale *material* yasiweze kupotea, lakini jambo la pili wanatupunguzia upungufu *gap* ya walimu kwenye mashule yetu. Watoto watapata nafasi ya kusoma. Hili hatuwezi kuliacha pembeni kwa majibu kwamba hatuna mwongozo. Majibu hayo hayatoshi, hayatoshelezi. Kwa hiyo tunaiomba sana Serikali ifikirie namna nyingine ya kuleta mfumo au mwongozo ili tuweze kuajiri walimu wengi zaidi kwa mkataba kwa sababu sisi wote ni Watanzania, tunajua hali ya nchi yetu hatuna uwezo wa kutoa ajira kwa walimu 300,000 kwa pamoja lakini basi walau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafanya ujasiriamali. Huko kwenye m-pesa tumeajiri walimu wenye *certificate,* wenye *diploma,* wenye *degree*. Unamlipa mwalimu shilingi 100,000 kwa mwezi na anafanya hiyo kazi. Anafanya shughuli ambazo wala hajazisomea lakini yuko pale kwa ajili ya kutafuta angalau tonge la kila siku. Sasa kama Serikali itaamua kuajiri kwa mkataba au kutengeneza utaratibu wa walimu kujitolea maana yake ni kwamba bajeti inaweza kutumika ndogo lakini ikawa imetatua matatizo mawili kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu wadhibiti ubora elimu. Ukizungumzia ubora wa elimu hawa wadhibiti ni kama tunavyochukulia nafasi ya CAG kwenye Hesabu za Serikali. Wao ndiyo wanaangali utaratibu, utekelezaji na namna ambavyo elimu inaendelezwa katika maeneo yetu, katika shule zetu na kadhalika. Nilizungumza mwaka jana katika bajeti iliyopita nikaiomba Serikali, hawa kwa nia njema kabisa huko nyuma Serikali iliamua kuwabadilishia muundo kuwatoa kwenye watumishi wa kawaida kuwapeleka kweye watumishi viongozi ili walau maslahi yao yaweze kuongezeka na mwisho wa siku kazi zao ziweze kufanyika kwa ufanisi. Niiombe Serikali na nimuombe Mheshimiwa Mkenda, Mheshimiwa Mkenda wewe ni Mwalimu na tunafahamu uwezo wako na sasa hivi una mama mmoja jembe sana, Profesa Carolyne Nombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, Katibu Mkuu tuliye naye Wizara ya Elimu sasa ni Katibu Mkuu mwenye weledi mkubwa. Mimi nimefanya kazi katika Kamati hii na nimeshirikiana na Wizara hii ya Elimu tangu nimeingia hapa Bungeni, na nimeshapita na Makatibu Wakuu zaidi ya watatu lakini Katibu Mkuu tuliyenaye sasa ni Katibu Mkuu kweli kweli. Anatoa ushirikiano, anajibu hoja za Wabunge, anakerwa na yale ambayo sisi Wabunge tuna kerwa nayo. Hongera sana Mheshimiwa Waziri, hongera sana Mheshimiwa Nombo, lakini mwisho wa siku tunachoomba, yale ambayo tunayashauri kama wawakilishi wa wananchi basi yachukuliwe hatua ili wananchi ambao tunawawakilisha nao waone kwamba tumefanya kazi yetu vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Husna Sekiboko kengele ya pili imelia.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Profesa Patrick Ndakidemi, Mheshimiwa Injinia Leonard Chamuriho na Mheshimiwa Mwita Waitara wajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru kwa kunipa fursa na nianze kwa kumpongeza sana Waziri wetu Profesa Adolf Mkenda, Naibu wake Omari Kipanga na Katibu Mkuu Profesa Carolyne Nombo na Wakuu wote wa taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanzia pale alipomalizia mwenzangu, nimpongeze sana Rais kwa kuboresha shughuli za elimu katika nchi yetu kwa sababu anajaribu ku-*address,* kutatua kero kubwa ambazo ni ujinga, umaskini na magonjwa na Wizara hii inahusika moja kwa moja kwenye kupambana na hivi vitu. Ninaanzia pale Mheshimiwa Sekiboko aliposema kwamba ubora na mimi nitaongelea ubora wa vyuo vikuu. Nataka tulinganishe vyuo vyetu vikuu vya Tanzania na vyuo vya Afrika na duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania na Afrika Mashariki, Tanzania tunakweda vizuri. Nchi yetu inakua vizuri sana na sisi kama nchi Taifa letu lina miundombinu bora sana ya elimu. Tunatoa elimu bure kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha sita na tunatoa mikopo kwa vijana wetu waweze kusoma. Kwa hiyo suala la kusoma hapa nchini siyo shida. Nchi yetu inajitahidi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilisikiliza taarifa ya habari ya *BBC,* wakasema kwamba kule Afrika Kusini kati ya watoto 10, nane hawajui kusoma vizuri na kuandika, lakini nchi ya Afrika Kusini katika Bara letu la Afrika ndiyo nchi yenye vyuo bora kuliko nchi zote kwenye Bara la Afrika. Sasa hapa kwetu Tanzania kwenye ubora wa vyuo vikuu tuko vibaya sana, hatuko vizuri. Ni kwa nini, ni nini kinatokea kwamba hata wale

ambao asilimia kubwa hawajui kusoma na kuandika wanatupita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *ranking* iliyofanyika kuangalia vyuo vikuu bora 200 duniani, Afrika Kusini nafasi ya kwanza mpaka ya tano ilichukuliwa na Afrika Kusini. Chuo Kikuu cha Nairobi kilikuwa cha sita, Chuo Kikuu cha Makerere Uganda kilikuwa cha 16. Chuo Kikuu cha Kenyatta kilikuwa cha 24. Chuo chetu Kikuu cha Dar es Salaam kilikuja cha 34, Chuo Kikuu cha *SUA* kikawa cha 67, Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili cha 94, *State University of Zanzibar* cha 163 na *UDOM* ikawa ya 184. Tunawashukuru hivi vyuo angalau vimetupeleka juu kidogo lakini bado kuna kitu hakiko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini *South Africa* wanatushinda na ukiangalia kwa ujumla wake katika hii *ranking,* vyuo vya Kenya na Uganda vimetupita vibaya sana. Sisi tuko chini kusema ukweli kwenye hii *aspect*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wenzetu wamefanikiwa sana kwa sababu wamewekeza kikamilifu kwenye sekta ya elimu na hapa sawa tunakwenda vizuri lakini bado kuna haja ya kuendelea kuwekeza pesa za kutosha kwenye sekta ya elimu ili vyuo vyetu navyo vionekane vizuri kwenye uso wa Kimataifa. Vigezo vinavyotumika kwenye ku-*rank* hivi vyuo ni vitu vya kwenye mtandao tu, mambo ya kwenye mtandao na sisi kama nchi Tanzania iko vizuri sana kwenye mambo ya mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wanaangalia kwenye mtandao kama kuna machapisho ya kisayansi yaliyofanywa na wasomi wetu. Kitu cha pili wanachoangalia ni shughuli za kitafiti kwenye mitandao ya vyuo vyetu. Je, kuna shughuli zinazoendelea za kitafiti? Je, chuo kimesajiliwa na mamlaka husika kama *TCU?* Je, chuo kinatoa *degree* za kwanza, *Master* na *Ph.D?* Hiyo tunafanya. Je, vyuo vinatoa elimu kwa

kuwasiliana, wananfunzi wanakaa darasani na kusoma? Vyote hivyo tunafanya lakini bado hatuonekani kwamba tunafanya vizuri kama vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili wanachoangalia ni shughuli za kitafiti kwenye mitandao ya vyuo vyetu. Je, kuna shughuli zinazoendelea za kitafiti? Je, Chuo kimesajiliwa na mamlaka husika kama *TCU*? Je, Chuo kinatoa degree ya kwanza, masters na *Ph.D*? Je, vyuo vinatoa elimu kwa kuwasiliana, na wanafunzi wanakaa darasani na kusoma? Yote hiyo tunafanya,a lakini bado hatuonekana kwamba tunafanya vizuri kama vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya huku vibaya kunasababishwa na viongozi wetu wa vyuo kukosa ubunifu kuonesha vitu vizuri ambavyo wamefanya. Ubunifu hamna, hiyo ndiyo sababu yangu ya kwanza. Sababu ya pili ni uvivu wa wanasayansi wetu wa Kitanzania kuchapisha, kuandika kwenye majarida ya Kimataifa ili sisi kama Taifa tuweze pia kutamba na kwenda kifua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya tatu ni tovuti zetu za vyuo vikuu haziweki vitu, hazina taarifa ya vyuo vyetu vikuu. Hakuna taarifa za mambo mazuri tunayofanya. Matokeo mengi ya utafiti ambayo wenzetu wanafanya, yanabakia kwenye makabati na kwenye kuta nne za vyuo vikuu, hayatoki nje ya pale. Hizi ni sababu kubwa ambazo zinatufanya tusionekane tuko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini athari za kupata *low rank* ya *Universities* zetu? Athari ya kwanza ni heshima hakuna. Tunakosa heshimia tukijilinganisha na wenzetu wa nchi nyingine. Athari ya pili, ni umaarufu wa Maprofesa wetu na Wahadhiri wetu. Huwezi kujilinganisha kwamba na wewe ni Profesa ukatamba kabisa kama chuo chako hakipo pale, yaani *your nowhere,* huwezi kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakosa nafasi ya kupata washirika wa kusaidiana nao kufanya utafiti. Huwezi kwenda kwa watu ambao labda ni vilaza ukafanya nao kazi, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kwamba wasomi wetu wanakosa nafasi. Kama hatuko vizuri, tunakosa nafasi kwenye masoko ya Kimataifa. Ushauri wangu nini kifanyike? Cha kwanza namwomba Mheshimiwa Waziri asimamie hili, Wahadhiri wote na wanafunzi wanaofanya *Masters* na *Ph.D* wajisajili kwenye *Google Scholar,* kwani mchakato wa kupata vyuo bora unatokea kwenye *Google Scholar. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili, watafiti wetu wachapishe kwenye majarida ya kimataifa, tusiende kwenye zile *journal* za ajabu ajabu ambazo hata hazipo kwenye mifumo. Twende kwenye majarida ya kimataifa kama wanaume na wanawake wenye nguvu pia. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Naam!

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia tuwe na sera ya kuweka machapisho yetu kwenye *depository* vyuo vyote, kwenye *library* zetu ziweze kuonekana *online*. Cha nne, tuoneshe *abstract,* hata tukishindwa kuonesha zile *Ph.D* na *Masters* ambazo vijana wetu wameandika, tuziweke *online* ili wanapochakata na sisi tuonekane tupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha tano, matukio yanayotokea kwenye vyuo vyetu kama mikutano, tukienda kwenye makongamano, wanaangalia vitu vyote hivi viwekwe *online* ili wanapochakata na sisi tuonekane kwamba huwa tunashiriki kwenye hivyo vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, pia tukienda kufanya *presentations* kwenye Mikutano ya Kimataifa tuyaweke kwenye mitandao ya vyuo vyetu. La muhimu hapa niwaombe Wakuu wa Vyuo na Wakuu wa Mabaraza ya Vyuo wasimamie hili kwa sababu kabisa sioni sababu ya sisi kuwa na *low ranking*. Nchi yetu inawekeza pesa nyingi sana kwenye elimu lakini kweli kabisa hatuko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mimi najua nilitoa mchango wangu na ndiyo sababu nimesimama hapa kwa nguvu kabisa, siogopi kuchangia kwamba tukaze viatu, tukaze uzi, twende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe kwa kusema kwamba hili suala la kuwa na nafasi za chini kwa vyuo vyetu siyo kitu chema, inatupunguzia heshima ya nchi yetu. Namwomba Waziri achukue hatua makini kabisa mapema kukabiliana na tatizo hili ambalo tukishakabiliana nalo mtatujengea heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Patrick Ndakidemi. Nilimtaja *Eng.* Leonard Chamuriho na Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Suma Fyandomo ajiandae.

**MHE. ENG. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika bajeti hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Napenda kukupongeza wewe unavyoongoza Bunge pamoja na Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wenzako kwa kazi nzuri mnayofanya katika kuendesha Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vile vile kutumia fursa hii kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwa maendeleo ya nchi hii. Tumeshuhudia kwamba anaweka utendaji mkubwa sana wa mara moja katika sekta hii ya elimu na hili ni jambo kubwa ambalo sasa tunaanza kuona matokeo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechungulia bajeti ya elimu, katika miaka mitatu kama ilivyo katika vitabu vyetu, inaongezeka kila mwaka, na hii ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Rais ana dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba elimu inakuwa bora katika nchi hii. Vilevile nampongeza Waziri Profesa Adolf Mkenda pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Omari Kipanga kwa kazi nzuri wanayoifanya, vilevile na wataalam wao, Katibu Mkuu, Profesa Nombo na Manaibu Katibu Wakuu wawili, Makamishna wote nakadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imesheheni wabobezi na tunaona kweli kazi inakwenda vizuri, tunawapongeza sana. Uwekezaji huu mkubwa ambao umewekwa na Mheshimiwa Rais katika miundombinu ya elimu unahitaji kulindwa na vilevile kupatiwa viwezeshaji. Ulinzi wa miundombinu utawezeshwa katika matengenezo ya mara kwa mara kuhakikisha kwamba miundombinu hiyo inadumu, lakini katika huduma zake viwezeshi kuhakikisha kwamba walimu na vifaa vinapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita zaidi katika elimu ya juu ambayo katika hayo mawili nitaangalia utafiti pamoja na utayarishaji wa walimu. Walimu wa Elimu ya Juu hawana chuo maalum cha kuwafundisha kama ambavyo tunafahamu vyuo vingine vya walimu hapa kwamba kuna chuo kinachofundisha walimu, lakini kwa elimu ya juu ni vyuo vyenyewe ndiyo hutengeneza walimu wake kulingana na hadhi ya chuo. Kwa hiyo, chuo kinaandaa walimu wake na ubora wake unategemea na jinsi ambavyo itapanga yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeangalia ukurasa wa 34, kwenye utakelezaji wa bajeti iliyopita, nikaona kwamba ndiyo, ameshughulikia mambo ya udahili vizuri, ameshughulikia vilevile na elimu ya wadahiliwa, lakini nilivyoangalia jinsi anavyoshughulikia walimu wa walimu, nikaona hapo kuna ombwe. Nilipoangalia vilevile katika ukurasa wa 76, nikaona mapendekezo ya bajeti hii anayoiomba, nikaona vilevile kwamba ameweka utafiti, ameupa kipaumbele. Kwa hilo nampongeza sana, kwani hilo ndilo ambalo linawezesha ufundishaji wa hao walimu wa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba bajeti hii haijaweka wazi jinsi wataalam hao, walimu wa walimu wanavyotengenezwa, kwa sababu kama nilivyosema mwanzoni, hakuna vyuo vya kuwaandaa walimu wa walimu. Hivyo, vyuo vinakuwa huru kutengeneza hayo matokeo ya walimu wanaowatengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi kwa sababu walimu hao wanakuwa wana shahada, vilevile ni zao la vyuo vikuu; na kuondoa huu utaratibu wa mwalimu kusoma hapo hapo na kufundisha hapo hapo, ambapo kitaalam wanaita *inbreeding,* vyuo vingi huhitaji kufundisha walimu katika vyuo vingine, na hapa ndipo changamoto inapoanza, kwa sababu inahitaji aidha watengewe fedha au wapate ufadhili. Sasa hapa kwenye ufadhili, ndipo changamoto inapokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna methali ile inayosema kwamba "anayemlipa mpiga zumari ndiye anayechagua wimbo." Sasa katika hili, wafadhili wengi huchagua kufadhili fani ambazo wanazipendelea wao, siyo fani ambazo chuo kinazihitaji. Kwa hiyo, hapo ndipo changamoto inapoanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta kwamba fani ambazo hazina mvuto kwa wafadhili zinaathirika katika vyuo vyetu. Unakuta vyuo vinapata wafadhili, lakini walimu wanaokwenda kufundishwa wanalundikana katika fani ambazo ni fani pendwa za hao wafadhili. Kwa hiyo, unakuta kwamba kweli ukihesabu idadi ya Shahada za Uzamivu ni nyingi lakini mchanganuo wa fani katika hiyo fani inakuwa kidogo kuna changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na vitu viwili. Moja, kuna fani nyingine unaweza kuziona kama ni fani ngumu, ambazo hazina mvuto kwanza kwa wanafunzi wenyewe. Pili, ni fani ambazo ni ghali kuzifundisha. Kuna fani nyingine ambazo kumfundisha mwalimu mmoja au mhitimu mmoja, unaweza ukafundisha wengine watatu. Kwa hiyo, hiyo haivutii wafadhili katika kuwekeza huko. Matokeo yake inakuwa ni nini sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta kwamba katika idara mbalimbali fani ambazo hazina mvuto zinapungua miaka hadi miaka, lakini matokeo tunapata. Wahitimu wanazidi kutoka lakini wamehitimishwa na nani? Wamehitimishwa na walimu ambao, fani zile ambazo hazipo, vilevile zinakuwa vichwani mwao hazipo, na matokeo yake unakuta baadhi ya kozi nyingine zinaahirishwa, kwa sababu wataalam hawa hawapo. Vilevile wanafunzi wa wauzamivu na wa uzamili wanaathirika kwa sababu wanakosa hiyo huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kushauri Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwamba, moja, vyuo vya elimu ya juu vianishe hizi kozi au utaalam ambao hauna mvuto kwa wafadhili. Baada ya kupata orodha hiyo ya fani ambazo hazina mvuto kwa wafadhili, basi Serikali itenge fedha kwa ajili ya fani hizo, kwani ni muhimu kwa Taifa lakini hazina wa kuzifadhili. Kwa hiyo, hiyo itatuwezesha kuhakikisha kwamba mazao ya chuo yanapotoka, pamoja na hiyo *degree* kubwa, lakini vilevile fani ambayo iko

kichwani kwao imekamilika kama ambavyo tunaitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa muda mfupi, Serikali iruhusu vyuo viendelee na utaratibu wao wa kutengeneza walimu wao wenyewe bila kuviingilia kwa sababu hilo ndiLo litakaofanya waweze kuainisha hizo fani na kuzitafuta na kuzitengeneza jinsi wanavyoweza. Hii ni pamoja na kuruhusu watoe mikataba kwa watu ambao wanadhani wanaweza kuwa na fani hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa utafiti umetajwa mle ndani, vilevile tuondoe hii dhana kwamba fedha za utafiti katika vyuo ni fedha za kuliwa na hawa walimu. Ni fedha muhimu sana ambazo ndiyo chanzo cha kutengeneza utafiti na utafiti huo ndiyo unaofanya kutoa hao walimu bora; walimu wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda wangu unakwisha. Natoa shukurani kwako na kwa hili, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng.* Leonard Chamuriho.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tutambue uwepo wa Profesa Yunus Mgaya, Rais wa *Tanzania Academy of Science* ambaye yuko pale kwenye *Gallery* ya Spika. Karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Suma Fyandomo na Mheshimiwa Hawa Chakoma, ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupeleka fedha kujenga *VETA*

Tarime, shilingi bilioni 1.4. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kulipa baadhi ya madai ya watumishi wakiwemo walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kupeleka vishikwambi ambavyo vimesaidia pia kupeleka teknolojia na kurahisisha mawasiliano. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa jambo kubwa hili ambalo ameruhusu tufanye mjadala wa kupitia mitaala ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika eneo hili, hili ni jambo muhimu sana, tunazungumzia Watanzania wa leo na kesho na vizazi vijavyo, tujipe muda wa kutosha wa kutafakari jambo hili. Tunahitaji kupata muda wa kujadiliana. Yako maswali yanahitaji kuwa na majibu. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri amesema, Januari mwakani 2024 wanaweza wakaanza utekelezaji. Tungependa Mheshimiwa Adolf Mkenda atuambie mkakati wa utekelezaji huu ukoje? Zile shule za zamani za ufundi wamekarabati lini? Vitendea kazi vya kisasa umepeleka lini, kwa maana ya ukarabati wa karakana na kadhalika? Vyuo vya ufundi vimesimama kwa muda mrefu. Walimu wabobevu wenye taaluma hiyo wameandaliwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mambo ni muhimu. Unaona watu wanauliza, Zanzibar kule Darasa la Kwanza mpaka la Saba hapa mnapendekeza Tanzania Bara, Darasa la Kwanza mpaka la Sita. Tumetajiwa mifano ya nchi nyingine ambazo zimefanikiwa, mnafanya *reference* wapi? Mambo haya yote yanapaswa kujadiliwa kwa kina ili tupate kitu cha maana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamependekeza hapa pia, ni vizuri tukapitia Sheria ya Elimu, twende kwenye sera, twende kwenye mitaala na tutengeneze kitu ambacho kitadumu kwa miaka 100 ijayo, tutengeneze Tanzania ambayo inaonekana

kwa macho tuchore *roadmap* ya nchi yetu kwa upande wa taaluma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile watu wanahoji hata lugha ya mawasiliano. Hili ni muhimu pia tutakubaliana kama Taifa, tunatoka hapa tunaenda wapi? Kila mtu aweze kuridhika na tuweze kwenda mbele. Pia maeneo yetu kwa mfano, mimi maeneo yetu watu ni wakulima kule, mitaala ambayo inatengenezwa, tungetarajia kuwe na fani ya uchimbaji, kuanzia *level* ya chini kabisa. Mahali ambapo kuna kilimo, kuwe na fani ya kilimo *proper* na vifaa viende vya kisasa. Mahali ambapo kuna uvuvi, kwenye maziwa na Bahari, lazima mitaala ya kisasa ya kuvua iwepo ili tukimaliza jambo hili, tuwe tumefanya *once and for all* na watu waweze kunufaika tupunguze shida kubwa ya ajira katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni ubora wa elimu. Nimeangalia matokeo ya Kidato cha Nne, ni kwa miaka mitatu. Kwa mfano, 2020 waliopata *Division One* mpaka *Division Three* walikuwa 152,909. *Division Four* mpaka *Zero* ni 318,148. Hao waliofeli ni asilimia 65. Mwaka 2021 waliofanya *Form Four,* waliopata *Division One* mpaka *Three* ni 173,422; *Division Four* mpaka *Zero* 310,398. Asilimia 62 hawa walifeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022 waliofanya mitihani darasa la kwanza mpaka la tatu ni 192,348, lakini daraja la nne na *zero* 328,000, kwa ujumla wake, kwa miaka mitatu hii. Maana yake waliopata *Division One* mpaka *Four* ni asilimia 34, zilizobaki walifeli kwa lugha nyingine. Hawa wako mtaani. Hii nime-*sight* miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sura moja nimeona hapa, mwaka huu wa 2022 kwa mfano, *division one* walipata wawili, *division two* wakapata sijui sita, wengine wote katika

watoto 200 walipata *four* na *zero*. Hii maana yake ni dalili mbaya kwenye ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kinachangia hapo? Mimi nazungumza kama mwalimu na Mbunge wa Vijijini. Tusijifiche ukaweka kichwa chini kwenye katani, halafu huku nje ukasema umejificha, lazima tuambiane ukweli. Tuna upungufu mkubwa kwa mahitaji ya elimu kwa walimu wenyewe. Ukiacha upungufu kwa maana ya idadi, hawa walimu wanaweza kufundisha? Unaposema anafundisha hesabu, anaijua? Kiingereza anafundisha anakijua? Kiswahili hicho anakijua? Kifaransa anakijua? Au ni walimu ambao wanafundisha Kiswa-Kinge shuleni! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna shida, Mheshimiwa Profesa Mkenda kuna kazi ya kufanya ya ziada. Hawa walimu wetu, hii *performance* ndiyo maana unakuta kuna ukinzani kati ya shule za watu binafsi na shule za Serikali. Hawa watu binafsi wana walimu wa kutosha kila somo. Shule za Serikali hakuna walimu wa kutosha. Shule za *private* kuna wanafunzi idadi ndogo darasani, shule zetu kuna 100,000 mpaka 200,000 kwenye darasa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa *private* wana motisha A moja kwa shilingi 100,000, hawa wa Serikali hawana motisha. Hawa wa *private* wana usafiri, wana chakula shuleni, wa Serikali hatuna. Hawa walimu wetu vijijini hawana nyumba. Leo tunazungumza matundu ya vyoo hayatoshi, lazima tukae kama Wabunge tuzungumze hali halisi. Hii imesababisha Profesa kwa kweli katika sehemu ambayo mimi mlinikwaza sana Wizara ya Elimu ni kitendo cha kundoa *ranking*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani shule tunajua kabisa kwamba kama mwalimu analipwa vizuri, kama mwalimu ana usafiri, maeneo mengine wana ratiba ya chakula, halafu ana wanafunzi wachache, anaweza akamfuatilia mwanafunzi mmoja mmoja, *obvious performance* ya huyu wa wanafunzi

wachache itatofautina na *performance* ya mwalimu ambaye ana wanafunzi wengi na hana sehemu ya kufikia na ana madeni na mshahara ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo lazima tulizungumze. Unapotaja shule imefanya vizuri, hivyo ni vigezo. Tunazo maabara ambazo ni mbovu hazijakamilika. Wenzetu wana maabara na vifaa. Tuna walimu wachache wa hesabu. Hivi kama una shule ambayo ni *form one* mpaka *form four,* hakuna mwalimu wa hesabu, mnatarajia apate A kwenye mtihani? Hiyo miujiza inatokea wapi? Sasa Profesa ungetuonesha mpango wa Serikali kupata walimu wa hesabu wa kutosha nchi hii, mpango wa Serikali wa kuleta walimu wa sayansi wa kutosha, mpango wa kuajiri walimu wa Tanzania ambao wako mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako, Profesa sasa hivi vijana wetu wamekata tamaa kwenda kusoma masomo ya ualimu. Wanaona kama ni fani ambayo hawapati ajira huko mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako Profesa sasa hivi vijana wetu wamekata tamaa kwenda kusoma masomo ya ualimu, wanaona kama ni fani ambayo hawapati ajira huko mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe jambo hili pia liangaliwe upya, tupeleke walimu, tuboreshe mazingira ya kazi watoto wetu wasome vinginevyo kuzuia *ranking* eti wanafanyabiashara unajidanganya tu. Walimu wana magrupu, wanafunzi wana magrupu, wazazi wana magrupu, wanafunzi tunawasiliana na ukweli hata mimi watoto wangu wanasoma *private*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wangu wa *form two* anaweza akamshinda mwanafunzi wa kawaida wa *form four* mimi naangalia mimi ni mwalimu naangalia hata wanacho

kifundisha, mazingira ya kufundishia na kujifunzia lazima yaboreshwe. Kwa hiyo, hilo lifanyike vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mimi ni Mbunge wa Tarime Vijijini jirani na Kenya. Kenya walimu wa Serikali ndiyo wanalipwa vizuri zaidi kuliko *private,* nenda ufanye *research*. Kwa hiyo, inamaana Kenya unapoenda kuomba kazi walikosa kazi za Serikalini ndiyo wanaenda *private,* kwanini? Wanalipwa vizuri zaidi na motisha ni kubwa. Tunaweza kuiga jambo zuri si vibaya tukaiga na kwa maana ya kuanza kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muingiliano na usimamizi wa elimu ni kweli kuna mapungufu kwenye *private*, wana michango mingi, wana masharti mengi lakini tuwe na chombo huru cha kuwasimamia. Hivi nimeamua kupeleka mtoto wangu *private* kwa kipato changu alafu unakuja kuniwekea masharti, tuboreshe shule za Serikali ambazo wananchi wengi masikini wanapeleka watoto wao. Watu walipeka Kenya, walipeleka Uganda, walikuwa wamerudisha, kwa mtindo wa sasa hivi tena watu wameanza kwenda Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuboreshe shule za Serikali, tuajiri walimu, tujenge maabara, tuboreshe huduma motisha alafu tushindane. Ila kwenye *level* ile ya chuo kikuu mimi natofautiana na wenzangu, kwamba mtoto wa waziri akope sawa sawa na mkulima kule Kangeliani, kule Nyabitucho, mimi nadhani tuliangalie. Vigezo vya mikopo ya elimu ya juu vinaweza kuangaliwa visiwe *fixed*. Mtu alikuwa ni mtumishi angeweza kusomesha mtoto, sasa amestaafu awe anaumwa, au mtu siyo Mbunge tuangalie vigezo hali halisi ya maisha ikoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusikalili mambo, maombi yangu Mheshimiwa Waziri nina shule zangu sita nguvu za wananchi, shule ya Kubiterere, Kimusi, Nyagisya, Barata

halafu Inchugu, Nyanungu hizi shule mpeleke wakaguzi kule zifunguliwe. Wananchi wangu wamechanga pesa wenyewe, wamejenga shule, wanataka watoto wao wasome ili tushindane na watu, kwetu tulichelewa sana kwenda shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba hiyo Mheshimiwa Waziri hilo lifanyiwe kazi lakini wale wakaguzi wa udhibiti ubora wale hawana hata magari, posho zenyewe wanaenda kukagua huku awajalipwa wamekopwa, wanatangulia kazini halafu unataka akakague shule nzuri aridhike. Unakuta wanaficha ficha hata wamepokelewa wakapewa tu chakula, akapewa sehemu ya kulala, akahifadhiwa wanakaguaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *equip* hiyo *department* ya udhibiti ubora watu wawe *fame* wawe sawa sawa wakague na vigezo tuvijue na kusiwe na *meanders.* Hata mkifungia shule kwenye matokeo, watoto wanaumia sana. Watoto wametoa hela mamilioni unafuta matokeo, unaadhibu watoto na wazazi, adhibu shule, adhibu wale wataalamu wetu msiumize wazazi wanaumia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, mwalimu wangu nilitaka niwaombe Waheshimiwa Wabunge. Mkiangalia kwenye uchaguzi ukitaka kujua anachozungumza Mheshimiwa Profesa Palamagamba ni kwamba wakati wa uchaguzi hivi ni wananchi wangapi ambao walishindwa kupiga kura? wanaandikiwa ni wazi kwamba ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupeleke mfumo elimu ya watu wazima kwa kila kijiji wale ambao wapo tayari kusoma, wasome kuna wengine hawasomi kwa sababu hawana nafasi, kuna wengine wamesoma hakusoma sana malezi, tutoe fursa kwa wote kama ambavyo tumetoa fursa kwa wale ambao wamepata ujauzito na changamoto mbalimbali ya kurudi shuleni basi na hawa ambao hawakusoma vijijini

wasome kwa hiyari na walimu wapo na vijana wetu wawepo. Pendekezo muhimu la mwisho kwenye ualimu… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita, ahsante sana. Kengele yako imelia.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja ni muhimu niunge mkono kwa nguvu zote tupate mjadala wa kutosha kwenye mitaala ya elimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Suma Fyandomo, Mheshimiwa Hawa Chakoma na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya wajiandae.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hii Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo amenipa afya njema nimeweza kupata nguvu ya kusimama, kuchangia wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo inafanya kazi vizuri ya kuboresha mambo ya elimu kwenye nchi yetu hii ya Tanzania. Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, anafanya kazi nzuri amekuwa akitenga fedha nyingi sana kwa ajili ya elimu na mambo mengine mbali mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ninaomba kabla sijaanza kuchangia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Mkenda pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote, wanafanya vizuri sana kusimamia elimu kuhakikisha inakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa sana kwenye shule za msingi. Shule za msingi zipo lakini ni kama tumezisahau kidogo, shule za msingi madarasa yamekuwa ni

machachakavu kwelikweli. Madarasa ni machakavu halafu wakati huo huo wanaweza yakawa hayatoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano pale Wilaya ya Rungwe, Kiwila kuna shule ya Mpandapanda ile shule ina wanafunzi jumla ya 1,380 ina vyumba vya madarasa saba kiasi kwamba darasa moja wanakaa wanafunzi 197 hiyo inapelekea shida kweli kweli namna gani ya kukaa wakiwa madarasani ili watoto waweze kuelewa wanavyofundishwa na walimu. Msongamano huo ni mkubwa sana, wakati huo huo kuna shule ambazo zina hali mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Wilaya ya Kyela kuna shule moja ya msingi inaitwa Makwale ina hali mbaya sana. Lakini wakati fulani hata ofisi zinakosena, wanachukua darasa wanaweka kama ndiyo ofisi, ambapo inaendelea kupungu zaidi idadi ya madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali, naomba itizame kwa upya, maana elimu ya msingi ina *matter* sana kwa sababu bila msingi hawajafika watoto sekondari, hawajafika chuo, hawajafika maprofesa wanakuwa hawapo wala madaktari bila shule ya msingi. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kushauri Serikali shule za msingi hizi tuzitazame ziboreshwe, ziwe mkazo wa kuboreshwa kwa sababu elimu yote inaanzia huku chini ndipo madarasa na vidatu vingine vinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nishauri Serikali pia, nishauri Serikali kwa upande wa wahasibu. Ninaipongeza Serikali imeweka wahasibu lakini kwenye shule zile kongwe Sekondari ya Rungwe, Iyunga Sekondari, Loleza kuna wahasibu kule na zingine nyingi tu ambazo zina wahasibu. Hizi shule zetu za kata za sekondari zilizo nyingi hazina wahasibu, anateuliwa mmoja wa walimu kwa ajili ya kwenda kufuatilia fedha kwenye halmashauri na mifumo inakuwa inasumbua, anaweza akaenda kwa siku nne

mfululizo na mwalimu yule ana vipindi darasani anatakiwa afundishe kwa hiyo, watoto wanakosa vipindi. Kwa sababu mwalimu anaenda kufatilizia mambo ya kiuhasibu kwenye halmashauri na si kwamba halmashauri wanafanya makusudi, hapana ni kwa sababu mifumo inakuwa inasumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi nilikuwa natamani serikali kama itaona inafaa basi watafutwe ama waajiriwe wahasibu siyo kwa kila shule, anaweza akawa muhasibu mmoja, ambaye anaweza akawa ana shughulikia shule tano mambo ya kifedha nadhani hilo litatusaidia kuiweka elimu yetu katika utaratibu mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano ipo hai kabisa, mtu anatoka Kata ya Nzovwe kule Mbeya Jiji au Iziwa nauli ni zaidi ya shilingi 5,000 anakwenda mjini Mbeya Jiji pale kwa ajili ya huduma. Mfumo umegoma basi anarudi kama alivyo kesho hivyo hivyo lakini bado mambo yanakwama kwa sababu vipindi ambavyo alitakiwa afundishe watoto wale wanakwama kupata masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchangia kwenye upande wa vyuo. Serikali inafanya vizuri sana kule Mbeya, Wilaya Rugwe tumebarikiwa, tuna vyuo viwili vya walimu, kuna chuo cha Mpuguso. Chuo cha Mpuguso Serikali imekitizama kwa jicho zuri, imefanya vizuri kwa maana imeboresha majengo lakini pia imeongeza mabweni lakini iliweka lami pia japo kwa sehemu lakini kuna changamoto. Chuo cha Mpuguso cha Ualimu kina wanachuo 670, wapishi wapo wawili, kiuhalisia walitakiwa wapishi wawe watano mpaka sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho ni chuo cha Mpuguso nakisema kwa mfano halisia si mfano ni halisia ya hao watumishi hawapo ila na vyuo vingine yamkini vina mapungufu kama haya. Kwa hiyo, nilitamani sana kuhusu

upande wa vyuo Serikali itizame watumishi namna ambavyo wapo na wanatakiwa kufanyaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia chuo hicho kina wakufunzi wa sayansi wawili tu. Kiuhalisia walitakiwa wakufunzi wawe wanne kwa hivyo chuo kina upungufu wa wawakufunzi hao ninaomba sana Serikali itizame upungufu huo wa wawakufunzi kwenye vyuo, ili iweke uhalisia na mambo mengine yaweze kwenda sawa sawa na vile mpango unavyoenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri Serikali inavyofanya uchakavu wa nyumba za watumishi. Kuna nyumba za watumishi lakini ni chakavu sana. Hivyo basi, nilikuwa naomba sana Serikali itazame hili namna ya kuboresha, kufanyia ukarabati nyumba za watumishi. Lakini pia bado azitoshelezi kuna uhaba, kuna uhaba wa nyumba za watumishi pale Chuo cha Walimu Mpuguso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali namna ambavyo imeweka vyuo vya *VETA*. Haijatusahau hata pale Iyunga kuna chuo cha *VETA* lakini pia kuna Sekondari ya Iyunga, Sekondari ya Iyunga ni sekondari ya muda mrefu sana ni ya tangu mwaka 1925 lakini miundombinu yake si rafiki sana kwa sababu haijafanyiwa ukarabati. Najua hili ninaweza kwenda moja kwa moja TAMISEMI lakini kwa sababu tunaongelea mambo ya elimu na pale ni elimu inapatikana ya sekondari. Ninaomba sana, sana muiangalie shule ya sekondari ya Iyunga ambayo ni shule bora sana kati ya shule nyingi ambazo ziko vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Suma, kengele imeisha lia.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante kwa kunipa nafasi ya kuongea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Hawa Chakoma, Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ajiandae.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Hotuba ya Wizara ya Elimu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwani wizara hii tayari imeishapokea asilimia 70.2 ya bajeti kufanya kubakia asilimia 29.8 ambapo kimsingi tunaamini mpaka mwisho wa bajeti hii tunayoenda nayo mtakuwa mmeishakamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwani bajeti ya sekta ya elimu imeongezeka kwa asilimia 18 sisi wote tumekuwa mashuhuda fedha takribani bilioni 300 ambazo zimeenda kwenye miundombinu ya ujenzi wa madarasa ya UVIKO hivyo kufanya kupata madarasa 12,000 tunawapongeza sana kwa kazi kubwa na nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia ubora wa elimu na tunapozungumzia ubora wa elimu Mheshimiwa Waziri penda usipende, taka usitake lazima tutalizungumzia ama utalisikia suala zima la upungufu wa walimu katika shule za msingi na sekondari ambayo takribani ni 160,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Husna, amesema hapa kwamba suala zima la walimu wa kujitolea kwamba majibu ambayo umetujibu ndani ya Bunge ni kwamba hakuna miongozo. Swali lingine ambalo Mheshimiwa Waziri, nikuulize inatohali nini? Au inatutaka nini kuweza kupata hii miongozo kama suala la miongozo tunaamini kwamba walimu wa kujitolea ni kweli linasaidia watoto wetu, linasaidia

wanafunzi wetu sasa kwa nini msilete hiyo miongozo? Ama kwanini msitoe hiyo miongozo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Waziri hapa ulipokaa unafahamu kwamba kwenye shule zetu walimu wa kujitolea wapo, wanapeleka maombi, walimu wakuu wanawapokea na wanalipwa posho na inategemea Serikali za vijiji. Serikali za vijiji ambazo zina mapato mazuri ndiyo hawa wanatoa fedha kulipa posho walimu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati tunasubiri mpango wa muda mrefu kuhakikisha walimu laki tatu wote tuweze kuajiri siyo jambo la miaka miwili, miaka mitatu inatuchukua hata miaka mitano hata miaka sita. Kwa hiyo, wakati tunasubiri kwenda kwenye jambo la muda mrefu, embu tuje namkakati wa muda mfupi, tuje na jambo la muda mfupi kama tutafanya ile ya kuingia mikataba sawa, kama tutaendelea hili la kusema kwamba Serikali za vijiji lakini mwisho wa siku ni vijiji vingapi vyenye uwezo? Hili kama tunalibariki bado linatakiwa kuja huko wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, kama sote tunakubali walimu wanaojitolea ni msaada kwa wanafunzi wetu. Kwa hiyo, hatuwezi kuzungumzia ubora wa elimu kama hatuna walimu, hatuna madarasa, hatuna matundu ya vyoo, hatuna madawati, hatuna nyumba za walimu. Kwa hiyo, suala zima la ubora wa elimu ni lazima tuangalie miundombinu lakini pamoja na walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mbali na hilo suala zima la elimu msingi ni lazima Sera itamke wazi wazi kwamba elimu ya msingi ianzie elimu ya awali. Suala hilo Mheshimiwa Waziri, nakusikiliza na nakufatilia sana huwa unalitamka kwamba elimu ya awali na yenyewe ni elimu msingi. Lakini tukija kwenye Sera aijitabanaishi, haijasemwa popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, elimu ya awali ni iwe elimu ya lazima. Kwa sababu hali ilivyo sasa ni kwamba wengine wanaona ni lazima lakini wengine wanafanya hiyari, na ndiyo hii sasa unakuta katika shule zetu masomo ya kujifunza wakati kwenye shule ya awali *a for apple b for ball and c for chair.* Watoto wa *private* wanajifunza kwenye shule za awali lakini watoto wetu sisi wa Serikali wanaenda kujifunza kwenye shule za msingi na ndiyo matokeo yake wakimaliza darasa la saba kwenye mitihani wanaandika mazombi hawajui kuandika majina yao, wakimaliza hawajui kusoma na kuandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati umefika wa elimu ya awali kuwa elimu ya lazima ili tuweze kuwa na msawazo mzuri kati ya vijijini pamoja na mijini na isiwe kwamba kwa ambae anaejisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia kwamba tunapo zungumzia ubora wa elimu na tuna zungumza suala zima la udhibiti wa ubora wa shule. Sasa tunao mradi mzuri, niwapongezeni kwa huu mradi wa *strengthen school quality assurance*. Mheshimiwa Waziri umeutengea takribani bilioni moja lakini mpaka tunavyo zungumza mwezi Februari hakuna hata senti kipande ambayo imeenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi una nia njema, una nia nzuri ya kuweza kusaidia suala zima tunaloliita ubora wa elimu. Tunakuomba kwenye kipindi kilichobaki hebu wapeni fedha ili waanze na mchakato wa huu mradi wa *strengthen school quality assurance*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema watu hapa wadhibiti ubora kwamba wadhibiti ubora tunataka kuwalinganisha na CAG katika masuala mazima ya elimu. Sote tunafahamu kazi nzuri inayofanywa na CAG katika masuala ya fedha lakini kama tunasema wadhibiti ubora

ndiyo *CAG* kwa upande wa walimu. Mheshimiwa Waziri muda umefika sasa wadhibiti ubora kuwaanzishia ama kuanzisha taasisi ya udhibiti ubora, wasiishie kuwa kwenye kurugenzi ama kwenye idara kwa sababu kazi wanayoifanya ndio tunataka kusaidia watoto wetu..

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia inaenda kasi sana, mambo yanaenda kasi sana. Kwa hiyo kama hatutakuwa na elimu iliyokuwa bora kwa watoto wetu, tutashindwa Kwenda kushindana huko duniani. Kwa hiyo muda umefika wa kuanzisha taasisi ya udhibiti ubora, muwapatie bajeti yao, muwapatie *vote* ya kwao ili waweze kufanya kazi bora na nzuri ya elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana, kubwa la kwangu nililokuwa nataka kulizungumzia ni hilo. Ifike mahala tuwe na elimu iliyokuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Chakoma, nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Mheshimiwa Constantine Kanyasu na Mheshimiwa Nusrat Hanje wajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara muhimu, Wizara ya Elimu. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambazo anazifanya hususani katika Jimbo la Manyoni Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Profesa Mkenda pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanazozifanya. Mwaka huu manyoni tumepewa chuo cha *VETA,* na nilikuwa nikiuliza sana swali la

*VETA*, mwaka huu tuna ujenzi wa Chuo cha *VETA* Manyoni, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshukuru vilevile Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Profesa Carolyne, mwalimu wangu wa Chuo Kikuu cha Sokoine. Nimshukuru sana pia Kamishna wa Elimu, Mkurugenzi wa *TEA* na Mkurugrnzi wa Bodi ya Mikopo. Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo tulikuwa tunapata vilio vingi sana vya vijana wetu lakini kwa kweli mwaka huu mmetutendea haki sana. Kwa hiyo nakushukuru Mheshimiwa Waziri lakini nampongeza sana Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Dkt. Badru vile vile kwa kazi kubwa ambayo ameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nina hoja mbili. Hoja ya kwanza nitazungumzia kuhusu hii Taasisi ya Elimu ya *TEA (Tanzania Education Authority),* lakini ya pili muda wangu ukiniruhusu nitachangia kuhusu mfumo wa elimu yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Taasisi yetu ya Elimu *TEA*, kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kupitia *TEA*. Tumeona kupitia *TEA* tumekuwa na programu mbili. Programu ya kwanza ni kupitia ule Mfuko wa Elimu, mmekuwa mki–*compliment* juhudi zinazofanywa na TAMISEMI kwa kujenga vyumba vya madarasa na kujenga vyoo kwenye shule zetu, na huu ni ubunifu mkubwa sana. Tusitegemee tu TAMISEMI waweze kuweka miundombinu kwenye taasisi zetu za elimu. Lakini Profesa umeliona hili, kuna maeneo ambayo yalikuwa yamesahaulika. Mkigundua lile eneo limesahaulika nyinyi mna-*top up* kwa kutumia taasisi ya elimu *TEA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, hawa wenzetu *TEA* vile vile wamepewa dhamana ya kuendesha yale mafunzo ya elimu ya ufundi wakishirikiana na *VETA* na vyuo vyetu vya ufundi. Taarifa niliyonayo ni kwamba zaidi ya vijana 45,000

wameshapata mafunzo haya, na sisi kwa Manyoni tumepata vijana wengi sana. Mpaka kwa sasa hivi nadhani wanafika Zaidi ya vijana hata 400 ambao wamepata haya mafunzo kwa kupitia huu mfumo wa *TEA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ushauri wangu ni nini kwenye taasisi hii ya *TEA;* tumeona impact kwa kupitia hiyo miradi ambayo mnajenga vyoo na madarasa kwenye maeneo ambayo TAMISEMI hawajagusa, lakini tumeona impact kwa kupitia fedha mnazotoa kwa ajili ya kuwapeleka wale vijana wetu wanapata elimu ya ufundi. Ni muda muafaka sasa kuijengea uwezo *TEA,* kuiongezea nguvu na bajeti ili waweze kuongeza vijana wengi. Pia tunatamani yale maeneo ambayo TAMISEMI haijaweza kupeleka miundombinu kwa kupitia Wizara yako Mheshimiwa Mwenyekiti lakini vilevile profesa ongezeni bajeti ili *TEA* waweze kufanya mambo makubwa zaidi. Kwa jhiyo kwa upande wa *TEA* mimi ningeshauri hayo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni kuhusu mfumo wetu wa elimu na *concept* ya kujiajiri. Tupo kwenye mapitio ya mfumo wetu wa elimu, kutengeneza mitaala na vile vile kuhuisha sera yetu ya 2014 ambayo kimsingi haijawahi kufanya kazi. Lakini ningetaka kujiuliza na tujiulize wote sisi kama nchi tunataka nini kwa kupitia elimu yetu ya Tanzania? Nadhani hili ni suala la msingi sana ambalo ni lazima tujiulize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mawazo ya aina mbili yanayokinzana. Wengi tunafikiri kwamba tunahitaji kuwatoa vijana vyuoni waende wakajiajiri. Lakini tukumbuke vile vile kwamba tunahitaji vijana hawa waingie kwenye soko la ajira, hususani soko rasmi Serikalini lakini hata kwenye *private sector*. Lakini hoja hii ya kujiajiri vilevile inatafsiriwa toifauti, na hili niliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana amesoma *IT,* lakini wengi ukisikia wanaongelea *concept* ya kujiajiri anakwambia

huyu kijana aende akafuge, Profesa ume-*invest* miaka minne kwa kijana amesoma *IT* unaenda kumwambia ajiajiri, nadhani *that is a very serious mismatch*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Profesa utuambie kwamba huyu kijana akajiajiri kwenye *area his of specialization*. Kama amesoma *IT* tuje na *micro business* ambazo atatumia ujuzi wake wa *IT;* na mimi hapo ndipo nilipotaka niweke hoja yangu. Kwa nini nasema hivyo; ni kwamba hawa vijana wengi tunapowahamisha kwenye *areas of their specializations*, matokeo yake wanakuwa hawana matamanio ya kukaa kwenye zile *field.* Atakaa kwa muda tu baadaye atakata tamaa. Atatamani siku zote arudi kwenye eneo ambalo alilisomea, kwa hiyo ni eneo ambalo mimi nadhani tunahitaji vilevile kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine ambalo nilitaka kuliangalia vilevile ni suala la mapitio ya huu mtaala. Kwenye mapito ya mtaala mmesema kwamba mnataka kuanza kuondoa mtihani wa darasa la saba. Sasa Profesa Mkenda tunaenda kuondoa mtihani wa darasa la saba, tutawapimaje walimu wa shule za msingi? Tunawezaje kuhakikisha kuna *accountability* kwa walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeshauri; ule mtihani wa darasa la saba bado ni muhimu unatakiwa uendelee ili tuweze kuwapima uwajibikaji walimu . Tunapoutoa maana yake mwalimu ataona hamna maana yoyote yeye kufundisha wala kuingia darasani kwa sababu hakuna kipimo chochote. Kwa hiyo bado ningeshauri kwamba ule mtihani uendelee ili tuweze kujua ni vijana gani na vijana wa aina gani ambao tunawapeleka huko juu kwa ajili ya kusoma kwa upande wa sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tumekuja na hoja nzuri sana, tunataka ku-*integrate* masomo ya amali na ufundi sekondari; na niliongea siku moja tulikuwa na kikao chetu

pale, mimi nikasema kwamba sawa, ni wazo jema tunataka kupeleka sekondari vijana wetu wapate elimu ya ufundi; lakini Profesa bahati nzuri wewe umefundisha Chuo Kikuu cha Dar es salaam mimi nimefundisha Chuo Kikuu cha Dodoma. Lengo la elimu ya msingi ni kutoa *general knowledge*. Inamuandaa mtu ili baadaye akienda vyuoni aende akasome masomo ambayo yatampa ujuzi, yatampa *skills*. Kwa hiyo katika *level* ya shule za msingi na sekondari hatutengenezi *skills,* pale tunamuandaa mtu ili baadae anapoenda chuoni aweze kuwa na *knowledge* ya kutosha ili tumjengee *skills.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ok*, tumekeja na *concept* kwamba tunataka sasa katika *level* ya sekondari hawa vijana wafundishwe ujuzi ili weweze kutengeneza *let say* washone nguo, waweze labda kutengeneza keki na vingine, ni jambo jema, lakini bado mimi nikasema kwamba sasa hivi Serikali inawekeza kwenye *VETA,* kwa nini sasa tusifikirie badala ya kusema kwamba tutapeleka mzigo mkubwa sekondari ambao vijana wengi tunawaandaa kwa zile *general knowledge,* kwa nini tusiweke nguvu kwenye *VETA* ambazo mmezianzisha ili wale wanaoshindwa darasa la saba, wameshindwa kuendelea sekondari hawa iwe lazima kwenda kwenye hivi vyuo vya ufundi? Na kwamba wale watakaoshindwa kutoka *form four* Kwenda *form five* hawa ndio iwe lazima Kwenda kwenye vyuo vya ufundi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine tukumbuke, sio kila mtu lazima awe fundi bado tunahitaji wahasibu, tunahitaji watu wa manunuzi. Kuna watu watastaafu, kuna watu Mungu atawachukua, kuna watu wataacha kazi kwa hiyo haitafika siku kwamba hii nchi yote inahitaji mafundi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunahitaji walimu , mainjinia, madaktari na watu wengine. Kwa hiyo mimi niliona, ni kwamba tunapofanya mapitio ya ule mtaala tuangalie

kwamba sawa tunaweka masomo ambayo yatakuwa na ubunifu lakini tusisahau kwamba katika *level* ya sekondari si *level* inayomuandaaa mtu kuwa *poroductive,* hapana. Level ambayo inamuandaa mtu kuwa *productive* ni *level* ya Chuo Kikuu tu, na ndiyo maana tunataka wakitoka pale wa-*accelerate* Kwenda vyuoni tuimarishe vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni nini; kwanza mimi nashauri mtihani wa darsa la saba uendelee, uendelee kwa sababu tunahitaji kuwapima walimu uwajibikaji wao. Tukiondoa mtihani wa darasa la saba haitakuwa na maana ya kuwa na walimu shule za msingi, hawatawajibika. Hilo ni eneo la kwanza. Lakini la pili, kwa wale ambao hawatabahatika Kwenda kidato cha kwanza na kwa wale ambao hawatabahatika Kwenda kidato cha sita kutokea kidato cha nne, sasa hapa ile elimu ya ufundi ndipo iwe ya lazima. Kwa sababu hawa hawawezi Kwenda hata vyuo vingine vya kati hawa sasa tuwarudishe kwenye vyuo vya ufundi ambavyo tumevijenga, na iwe ya lazima huo ni ushauri wangu wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, niliwahi kuongea huko nyuma, na Waheshimiwa Wabunge wengi wamelaalmika hapa, kwamba kuna tatizo sana kwenye *competences* za walimu wetu. Lakini tatizo, Profesa, na umefundisha Chuo Kikuu cha Dar es salaam, ukifuatilia wanaoenda kusomea ualimu ni mtu aliyepata *four*, *three* ndio wanaoenda kusomea ualimu. Wale waliopata *division one* na *two* wanaenda kusoma kozi zingine, iweje wewe ulipata *three* umtengeneze mwenzako apate *division one*? Kwa nini tusibadilishe mfumo, kwamba wale waliofaulu zaidi kwa *division one* na *two* ndio watufundishie watoto wetu? Lakini wale tumewaacha wamekimbia wameenda kusoma wanakuja kufanya masomo ya *business.* Kwa hiyo ni eneo mimi nadhani mnahitaji kuliangalia kwenye sera yetu, kwamba vijana waliofaulu zaidi tuweke motisha ili waone ualimu ni mzuri, waweze kurudi kufundisha kule

watutengenezee *brains* zingine huko katika nanii zetu. Lakini lingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Pius Chaya, nilimtaja Mheshimiwa Costantine Kanyasu, Mheshimiwa Nusrat Hanje na Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo wajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba na mimi nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, na niseme tu tangu mwanzo kwamba mimi naunga mkono hoja. Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameendelea kuifanya elimu kuwa kipaumbele kikubwa kwenye nchi, na hili tunaliona kwenye bajeti. Kwa mujibu wa bajeti ambayo tunayo takribani asilimia 17 imewekwa kwenye elimu, na haya ni maamuzi sahihi, na hakuna sehemu ambapo watu waliwahi kula hasara kwa kugharamikia elimu, kwa hiyo napongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwanza kwa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba pale Geita Mjini tuna Chuo cha *VETA* na kile Chuo cha *VETA* pamoja na kusua sua kwake kimefikia *level* ambayo naamini sasa tunaweza kuwa tayari kukifungua angalau tukaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu kumtaarifu mapema Mheshimiwa Waziri kwamba nimeunga mkono bajeti yake, lakini natamani kuona kwenye bajeti hii sasa ameweka mahitaji yote ya lazima ili kile chuo kiweze kuanza.

Tunahitaji walimu , vifaa na miundombinu mingine. Namna yalivyo sasa majengo yale yataanza kuharibika kabla hayajaanza kufanya kazi. Kwa hiyo nimesema naunga mkono hoja lakini namtahadharisha Mheshimiwa Waziri kwamba natamani kuona kwenye bajeti hii sasa chuo changu kinaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili Kamati imesema vizuri kwamba tuna upungufu mkubwa sana wa walimu ; na jambo hili liko kwenye Halmashauri yangu. Mimi nina upungufu mkubwa wa walimu takribani walimu 500. Naipongeza sana Serikali imekuwa ikitupa walimu wachache; na hivi karibuni Mheshimiwa Waziri ametuma vishikwambi tunakushukuru sana kwa vishikwambi, amepelekea walimu .

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka anieleweshe vizuri; vishikwambi kama vilivyo havitawasaidia kama kwenye bajeti yake hatutaona ametenga fedha kwa ajili ya *bundle* kwa sababu watabaki na madude ambayo hayana kazi. Lakini nataka kujua sasa vitasaidiaje kupunguza upungufu wa vitabu? kwa mfano hata kishikwambi kimoja kikiwa kwenye shule kama kuna mfumo wa kuhamisha kufanya kishikwambi kuwa *resource center* na kuhamisha *materials* sasa kuyafanya yaweze kupatikana kwenye shule nzima ni jambo jepesi. Lakini shule zetu nyingi hazina *printer*, *copier* na umeme. Nataka kuona huo makakti vishikwambi hivi viweze kutumiaka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu tuzungumzie habari ya mikopo. Naiomba Serikali, katika maeneo ambapo tumeendelea kufanya vizuri; tumeongeza fedha mwaka jana na nimeona mwaka huu pia wameongeza fedha kidogo kwenye mikopo lakini bado hatujatosheleza. Naiomba Serikali kapo kakundi kadogo sana ka walemavu, ambako kanahitaji tu kawekewe fungu maalumu, hata 1% au 2% ambao wanateseka sana. Ni moja ya kundi ambalo haliwezi kuhangaikia mikopo kama wanavyohangaikia watu

wengine. Kwa hiyo kakundi hhiki kiwekewe kiwango maalumu kwamba aina yoyote ya mlemavu anapofanikiwa kwenda *university* habari ya mkopo kwake iwe *granted,* na jambo hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza *NMB* kwa kuja na *package* ya mikopo kwa ajili ya kukopesha wanafunzi. Shida yangu pale ni moja tu *collateral* ni nini? Huyu mwanafunzi *collateral* yake ni *registration* anaipata chuo kikuu? Nimeona, marejesho yake ni kama *commercial,* ni kama ya kibishara. Asilimia tisa ni hela nyingi sana kwa mtu ambaye hana uwezo wa kujisomesha.

Mheshimwia Mwenyekiti. kwanza *registration* iwe ni *collateral numbe*r one, lakini cheti chake kiwe ndicho *guarantee* ya kumfanya huyu mtu aweze kuaminika. Familia nyingi hazina uwezo wa ku-*service* huu mkopo na riba ya asilimia tisa kwa mwanafunzi ambaye ameshindwa kujisomesha. Tunawapongeza sana kwa kuja na hiyo *package,* lakini bado naamini kwamba kuna haja ya kuapanua na kuona huyu anapopata udhamini peke yake iweze kumsaidia kwenda chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakwenda kwenye mambo yangu mawili ambayo nilitaka kusema. La kwanza, pamekuwa na *double standard* ya maelekezo kwenye ofisi ya Mheshimiwa Waziri. Unakuja waraka wa elimu. Kwa mfano kuna waraka wa elimu ambao umetoa maelekezo ya kuondoa darasa la kwanza mpaka darasa la nne kwenye bweni, na watoto wa bweni waanzie darasa la tano mpaka la saba. Mimi nataka Serikali inaisaidie; tunazo shule tayari ambazo zimefanya *investment* hii zaidi ya miaka 20 huko nyuma, na tuliwapa wenyewe leseni tukazisajili. Sasa tunapoleta waraka unaoanza sasa kuzuia tunafanya mambo gani? Maana yake tunazuia wale wasiandikishe watoto au tunawaambia wawekezaji wapya kwamba tunasheria *double standard* kwenye nchi moja kwamba ukienda shule B

utakuta watoto wapo, ukienda shule C utakuta watoto hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa mimi kwa maoni yangu Wizara itafute namna ambavyo itatoa waraka ambao utafanana kwenye usimamizi maeneo yote. Hata hawa wasimamizi wadhibiti ubora tutawapa kazi kubwa. Akienda kwenye shule A anakuta *criteria* tofauti, akienda kwenye shule B anakuta criteria ni tofauti, na wazazi pia tunawachanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme jambo moja hapa; hakuna mtu aliyechagua, anayechagua kwenda kwenye shule ya gharama kubwa wala anayechagua kupeleka watoto bweni. Wako watoto wako kwenye bweni si kwa sababu wazazi wanapenda. Kuna mtumishi anaajiriwa leo, mke wake anaajiriwa Dodoma, baba anaajiriwa Lindi. Anakopelekwa baba hakuna shule, anakobaki mama nafanya kazi asubuhi mpaka saa kumi, *solution* ni kumpeleka mtoto bweni, kwa hiyo hawa wanapeleka mtoto bweni si kwa kupenda. Ninaiomba sana Wizara iliangalie jambo hili kwa mapana yake, isilichukulie jambo hili kama jambo ambalo watu wanaopeleka watoto kwenye shule za bweni wanapeleka kwa kupenda. Wengi wanapeleka kwa sababu mazingira ya malezi yanawalazimisha kutokuacha watoto na *house boy* ama na *house girl,* na matokeo yake Watoto hawa ni bora uwapeleke shule ambako unaweza kuwa na uhakika angalau na asilimia chache ya malezi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuwepo na utaratibu ambao ni *uniform;* tusije na utaratibu ambao unaanza kubagua sasa, watu waliowekeza mpaka miaka fulani wana masharti tofauti na wengine wanaokuja wana masharti tofauti. Hii itatuharibia sana kwa sababu inatuletea *double standard* kwenye eneo moja ambalo mimi naamini linahitaji kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na jambo ambalo ni la msingi kabisa katika maeneo haya, tunaamini kwamba, watu wote, hata kwenye shule za Serikali ambazo tunazo, kipimo kikubwa ni kuona kwamba wanafunzi na watoto tunaowapeleka wanapata elimu kwa mujibu wa mwongozo, sera na sheria za Serikali. Kinachoendelea sasa hivi ni kama vile kuna ushindani, sasa kunakuja ushindani, kwamba wanaotoa elimu binafsi ni washindani wa Serikali, lakini mimi Mheshimiwa Waziri nataka kusema hawa sio *competitor* wako shule binafsi ni *partiners* kwenye hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuikumbusha Serikali kwamba siku ikitokea shule zote za msingi za watu binafsi zikafungwa au ikatokea shule zote za Serikali zikafungwa mzigo huu mkubwa ambao umebebwa na wawekezaji binafsi utachukua miaka mingine 10 au 15 kufikia kwenye *level* ambayo tunayo sasa ya utoaji wa elimu Serikalini. Tuwachukulie hawa kama wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alizungumza hapa mzungumzaji mmoja jana kwamba, kwenye elimu ya sekondari na shule za msingi kuna kodi nyingi sana kiasi kwamba zingine zinakatisha tamaa wawekezaji wakifikiri kwamba tunawakomoa; lakini kimsingi jambo hili lilipaswa kubebwa na Serikali kwa sababu huu ni mzigo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananfunzi zaidi ya 200,000 ambao wako kwenye shule binafsi wakirudi ghafla Serikalini, iko miji ambayo haina maeneo ya kujenga shule. Nataka tu nitoe mfano, mimi nina shule yangu moja ya msingi inaitwa Mbugani ina watoto 4,500. Katika eneo lile tukisema tunafunga shule binafsi, tukaongeza watafika watoto 6,000; hakuna sehemu ambapo tutawapeleka hawa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ninaiomba Serikali, kutokana na upungufu wa walimu kuna michango mingi sana kwenye shule zetu huko chini. Kuna maeneo

ambapo shule zinaamua kupeleka watoto kwenye kambi gharama zinakuwa kubwa. Kwa hiyo michango ile tuliyoifuta mwanzo imerudi kwa *style* kwa sababu ya ku-*cover* upungufu wa walimu.

Sasa niombe itoe mwongozo ambao kama tumeruhusu kuajiriwa kwa mikataba, utolewe mwongozo na namna gani ya kufanya ili wazazi waweze kupunguziwa mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Constantine Kanyasu. Nilimtaja Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Rehema Migilla na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi kama Mwenyekiti wangu wa Kamati na Wajumbe wenzangu wa Kamati na watu wote ambao wamepongeza jitihada ambazo zimefanywa na Kamati ya Mapitio ya Sera na Mitaala. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako ambaye alianza mchakato, lakini pia Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, ambaye na yeye alipokea mchakato wa mapitio ya sera na mtaala, lakini kwa upekee sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu, yeye alionesha *political will* kama kiongozi wa nchi kwamba, kuna umuhimu mkubwa wa kufanya mapitio ya mfumo wetu wa elimu kwa ajili ya kuendana na mazingira ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana nimpongeze Profesa Makenya Maboko kwa sababu, amefanya kazi iliyotukuka na viongozi wote, Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Wizara, mama yangu Profesa Carolyne Nombo, anatuheshimisha sana kama wanawake na tunaona kwamba, tukipewa nafasi tunaweza kufanya makubwa zaidi.

Kwa hiyo, majina yao yataandikwa kwa wino wa dhahabu kwa sababu, hii *document* ambayo wameitengeneza ukweli ni kwamba, ni *one of the outstanding documents* kwenye *East Africa,* inawezekana hata Nchi za Kusini mwa Afrika na inawezekana Afrika kwa hii *document* iliyotengenezwa, ni *one of the best,* kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamepitia na wataalam wamepitia. Nipongeze kwa sababu walijipa muda wa kukusanya maoni na hawakuchukua *speed* kubwa sana, kwenda harakaharaka, wali-*take time* waka-*exhaust* na wamefanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kabla sijaanza kuchangia nizungumze jambo moja kwa sababu, mapitio ya mtaala ya sasa hivi na sera tunasema falsafa ya sasa hivi ni *self-reliance,* elimu ya kujitegemea. Sasa labda kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Chaya ni Mwalimu wangu chuo kikuu niseme tu kidogo kwamba, alichokizungumza kwamba, tuache *VETA* tusubiri walio-*drop* wameshindwa waende *VETA,* maana yake tunakuwa hatutekelezi lile lengo la kusema kwamba, tunatengeneza mfumo wa elimu ya kujitegemea. Tunataka wazazi na Watanzania wote waone kwamba, aliyepo *VETA* ni ameamua tu *alternative pathway,* amechagua kwenda huko, sio kwamba, hana uwezo na ninajua ndio dhamira ya kufanya marekebisho na mapitio kwa sababu, tunajenga ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana nipongeze mchakato uliofanyika kwa ku-*integrate skills* za karne ya 21. *Study* za karne ya 21 ambazo wamezi-*integrate,* japo nina mambo kadhaa ya kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipongeze kwa sababu, wame-*integrate communication,* tulikuwa tuna tatizo hilo, lakini pia wame-*integrate collaboration,* wame-*integrate creativity* na *innovation,* lakini *critical thinking,*

tafakuri tunduizi na nimekuwa nikizungumza, lakini *problem solving,* utatuzi wa matatizo, *digital literacy, ethics and patriotism.* Wameamua kuzichukua kwa sababu ndio karne ya 21, labda niwaambie Waheshimiwa Wabunge dunia tunayoishi sasa hivi ni dunia *soft,* inahitaji watu ambao wanafikiri sana na wanatatua matatizo yanayowazunguka kwa sababu, matatizo yanakuja kila siku na yanahitaji akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli kuna maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia, lakini *the only thing* ambayo haiwezi kuwa *replaced* na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ni kufikiri. Kwa hiyo, ni lazima mfumo wetu wa elimu uendane na namna gani ambavyo tuna-*feed* hilo *gap* la fikira kwa sababu, mwanadamu pekee ndio Mungu amempa uwezo wa kufikiri. Sasa kama una mfumo wa elimu ambao mtoto anatumia muda mwingi darasani na mfumo huo haumwelekezi huyu mtoto kufikiri, kuanza kung'amua matatizo yanayoweza kujitokeza baadaye, maana yake mfumo wako wa elimu unakuwa *redundant. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nipongeze kwa hilo, ila nina changamoto moja; wameeleza, ukiangalia kwenye tamko la sera ambalo linaenda kusababisha mitaala kutengenezwa, tamko 3.3.6. Wanasema kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha mtaala unalenga kukuza stadi za karne ya 21 ambazo amezitaja hapo kwa mfumo wa kuchopeka, ku-*integrate.* Wasiwasi wangu ni hapo kwenye ku-*integrate* kwa sababu, unawezaje kupima kitu ambacho Umeki-*integrate* kwenye *process? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, hakuna utaratibu waliouweka kwenye kupima. Labda niseme hivi, wameeleza kwamba, anayeenda kutekeleza mtaala, tunajua anayeenda kutekeleza mtaala ni Mwalimu na anaenda kujenga umahiri kwa wanafunzi na anaenda kujenga hizi stadi za karne ya 21, lakini hata kwenye marekebisho ya elimu ya ualimu, Mwalimu hajawekewa

somo la kujenga umahiri wa hizi stadi. Mtu ambaye unamtegemea akazijenge stadi hujamwekea somo la kuzijua na nina mashaka sana kwa sababu tunawajua Walimu wetu ambao tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hizi stadi, kwani leo tunakosa nini? Kwa sababu, hizi stadi tukienda, tukirudi kwenye Sera ya mwaka 2014, tukirudi kwenye *competence based* hiki ambacho tunakirekebisha leo, hizi zilikuwepo na zilikuwa kwenye mfumo huu huu. Hazikuwa zimeandikwa kama hivi, lakini zilikuwa kwenye mfumo huu wa kuchopeka, sasa badala ya kuchopeka kwa sababu, tukichopeka tutakuwa hatuna namna ya kuzipima. Kwanza anayeenda kutekeleza hajajengewa umahiri wa hicho kitu, lakini kuzipima hatutaweza kuzipima kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini sasa tusitafute namna ya kuzifanya ziwe kwenye namna kama mada au somo kwa sababu, tumeweka ile elimu ya historia ya Tanzania na maadili? Kwa nini isiwe huko ili sasa tufuatilie hatua kwa hatua ili tuweze kujua ni namna gani ambavyo tunaweza tukampima mtoto mwisho wa siku kwamba, tumefanikiwa kumfanya awe ni mtatuzi wa matatizo kwenye jamii kwa kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika pia kwamba, kwenye hizi *skills, skill* ambayo ni muhimu sana ya *self-awareness,* kujitambua, haipo katika hizi *skills,* haijawekwa. Niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kujitambua ni pamoja na wewe binafsi, *intra personal* na *inter personal skills* ambazo zinamfanya mtu ajitambue kihisia yeye ni mtu gani na zitatusaidia pia ku-*solve* matatizo ya kimaadili kwenye jamii kwa sababu, inawezekana watoto wanaangalia vitu vingine ambavyo vinawafanya wasijitambue wao ni akina nani na ndio wanakua katika utaratibu huo. Kwa hiyo, *skills* kama *self-awareness* ni muhimu mno iwepo katika mfumo wetu wa hizi *skills* za karne ya 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, upimaji na tathmini. Niseme tu katika Rasimu ya Mtaala, Sura ya Nane, Kipengele cha 10, Wizara imezungumza na wameeleza *gaps* zilizokuwepo kwenye upimaji. Naunganisha na masuala ya hizi stadi za karne ya 21 kwa sababu hata upimaji wake haueleweki. Kwenye mfumo wa kawaida wa shule *continuous assessment,* upimaji endelevu, umepewa asilimia 30, halafu upimaji wa mwisho umepewa asilimia 70 kwenye mfumo wa kishule, lakini kwenye mfumo wa elimu ya ualimu ni *fifty-fifty* angalau, hamsini-hamsini, lakini kwenye *inactivate,* amali, wao wameenda mbali zaidi wana zaidi ya asilimia 70 na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kweli kabisa mtihani wa mwisho unaweza kumtambua mtoto kwamba ana akili au hana? Kwa sababu, hiki kilichoandikwa sasa hivi sio kwamba, hakikuwepo. Tumefanya *review* sasa hivi tume-*highlight* na vizuri kabisa Serikali imeonesha kuna *gaps,* lakini ni kwamba tume-*highlight* tu. Ukweli ni kwamba, *continuous assessment,* upimaji endelevu wa ndani ya shule, Mwalimu na mwanafunzi ulikuwa haufanyiki. Yale matokeo mnaona tunafanya *ranking* leo tunalalamika tumeondoa *ranking,* lakini yale ni matokeo ya mwisho. Kuna *factors* nyingi zinaweza kusababisha mtoto afeli mtihani wa mwisho, lakini sio kwamba, hana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuniambia kwamba, mtoto aliyefaulu *standard seven,* akafaulu kidato cha pili anakuja kufeli *form four* tena kwa *zero,* haiwezekani, kuna namna ambavyo huyu mtoto katika kujifunza kwake kuna vitu anajua. Kama lengo letu la elimu kama ninavyolielewa mimi ni kumjenga Mtanzania mwenye umahiri, anayeelewa, ambaye anaweza kuwa mwananchi ambaye atakuwa na mchango kwenye nchi, tunahitaji kuongeza asilimia za *continuous assessment. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio tu kuziongeza, tuzipime kiuhalisia kwa sababu, Mheshimiwa Waziri anajua kwa sababu yeye pia ni Mwalimu na wapo Walimu wanafahamu. Ukweli ni kwamba, hakuna namna ambavyo wanafuatilia, tunaambiwa tu huu ni mkusanyiko wa mitihani yako ambayo umefanya. Lengo la *continuous assessment* ninayozungumza mimi sio majaribio na mitihani, kama tunapima *problem solving* ni lazima tuwe tuna utaratibu wa kuwapima watoto kwenye matatizo yanayowazunguka katika mazingira yao pale pale shule. Kwa hiyo, ni ushirikiano wa Mwalimu na mwanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *NECTA* ni *machinery* ambayo ina *full autonomy* ya kwake, utaratibu wake wa jinsi ya ku-*operate,* itafutwe namna tunaweza tukai-*integrate*. Kwanza tuongeze asilimia ili tufike angalau 50 mpaka 60 au angalao *fifty-fifty,* lakini nzuri ikiwa 60 kwa sababu ya kitu ambacho tunategemea tukipate hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda umebaki kidogo nimalizie kuhusiana na lugha ya kufundishia. Kwanza niwapongeze Serikali wame-*play neutral role,* wame-*play neutral ground* kwa sababu wamesema kwamba, anayetaka kufundisha Kiswahili ataomba kibali na anayetaka kufundisha Kiingereza ataomba kibali, kwa hiyo, wamejaribu ku-*play politics* hapo, lakini tunajua, sitazungumza kwenye lugha ya Kiswahili sana, najua siku zote huwa nazungumza kwamba, ni muhimu sana tujifunze kwa lugha tunayoielewa, lakini hata hicho Kiingereza, mimi nimesoma *HKL Form Six,* tumesoma *syntax, phonology, semantics,* vitu ambavyo tunajua leo hapa hatuzungumzi *syntax,* hatuzungumzi *phonology*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunafundishwa Kiingereza tufundishwe kama *communication language,* lugha ya kuwasiliana, kwa sababu, tunataka hawa watoto wakitoka wamejua wamegundua vitu vyao, wawe wana uvumbuzi, waweze ku-*communicate,* waende wafanye

biashara bila kutafuta mkalimani, aendee nchi yoyote duniani. Kwa hiyo, kama tunakubaliana ni Kiswahili basi kiwe Kiswahili na kama tunakubaliana ni Kiingereza basi kiwe Kiingereza, watoto wasikutane na Kiingereza barabarani. Nazungumzia watoto wa Kantalamba huko, wasikutane na Kiingereza barabarani, waanze kutoka darasa la kwanza, kutoka awali, la kwanza, waende na Kiingereza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ni jukumu lake kujenga umahiri kwa Walimu ili wawe *the best*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu vingi hapa tunaweza tukavizungumza, vingine najua tutaviandika huko, lakini cha mwisho kabisa, bajeti ya Wizara ya Elimu. Asilimia zaidi ya 64 ya bajeti ya Wizara ya Elimu yote inaenda kwenye mikopo. Tutafute *solution* ya kudumu ya ku-*fund* mikopo ya elimu ya juu kwa sababu, tunakosa pesa za kufanya vitu vingine kwenye Wizara, kwa mfano, kitu muhimu kama utafiti hatuna pesa za utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat Hanje. Haya, nilimtaja Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa Rehema Migila, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Latifa Juakali wajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai leo hii tunachangia masuala ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu za kwanza napenda nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri aliyoifanya kuboresha elimu nchini kwetu Tanzania, hususan kwa kujenga shule za sekondari kila Mkoa kwa ajili ya watoto wetu wa kike ili waweze kusoma masomo ya sayansi. Nampongeza pia, kwa kujenga shule za *VETA* 63 ambazo zitaenda kujengwa kwenye Wilaya ambazo hazina shule za *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia kwa ujenzi wa shule za sekondari zinazoendelea nchini Tanzania na nampongeza Mheshimiwa Rais kwa ujenzi wa madarasa kwenye shule zetu za *primary* kwa kutumia mradi wa *Boost*. Baada ya pongezi hizo napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Profesa Mkenda na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingine ziende kwa watendaji wote wanaofanya kazi Wizara ya Elimu na walioandaa mabadiliko ya sera ambayo tutakwenda kuitumia nchini kwetu Tanzania ikiwa ni mwongozo wa nchi yetu kwa miaka inayokuja. Nawapongeza kwa kuja na hiyo sera, lakini ninayo mambo mawili ya kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu inaleta sera, mtekelezaji wa sera ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sasa bado tunayo matatizo kwenye shule zetu, matatizo ya madawati, matatizo ya upungufu wa vyoo, lakini pia na matatizo ya madarasa. Tunaomba huyu mtekelezaji wa hii Sera ya elimu aweze kuwezeshwa, lakini asimamiwe katika kutekeleza hayo, hususan kwenye suala la madawati, lakini pia kwenye suala la ujenzi wa vyoo, lakini pia kwenye suala la kukarabati zile shule kongwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye shule zile kongwe utazionea huruma. Ziko shule kule Mpanda ambazo hususan kama mimi niliondoka pale miaka mingi, ile rangi niliyoiacha bado ipo mpaka leo, mfano Shule ya Kashaulili

Mpanda. Pia zipo shule nilizitaja mara ya mwisho nilipokuwa nachangia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, watoto kutoka darasa la kwanza mpaka la nne wanakaa chini, Shule ya Msakila, Shule ya Shanwe, Shule ya Nyegere, Shule ya Mkapa. Shule hizo watoto kutoka darasa la kwanza mpaka la nne wanakaa chini, hawana madawati, ukienda kwenye shule hizo pia vyoo havitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuja na haya mabadiliko ya sera, naomba Wizara inaposimamia hii sera ili ikatekelezwe ihakikishe kwamba, hivyo vitu vipo vinatekelezwa. Madawati yapo na watoto wanakaa kwenye madawati, sio kukaa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichangie kwenye suala la Walimu. Hapo zamani miaka ya nyuma kwa wale tuliozaliwa mbele kidogo kulikuja mfumo kwamba, mtu akimaliza darasa la saba anaweza akafundisha shule za *primary,* elimu ikayumba. Naomba tunapokuja kutekeleza hii sera Wizara ya Elimu ihakikishe kwamba, inafundisha Walimu watakaoenda kutekeleza hii sera ambayo tunakwenda kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kutakuwa na program. Tuna matatizo ya watoto wetu kufeli, lakini tuna matatizo pia ya watoto wetu kutokuwa na *competence*. Hivyo basi, tunaomba hii *competence* ya watoto ipelekwe kwanza kwa Walimu wafundishwe ili waweze kwenda kufundisha vizuri. Haiwezekani wewe umepata *division four* ukaenda kumfundisha mtu apate *division one,* kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Chaya. Kwa hiyo, naomba hilo liwekewe mkazo. Walimu wapelekwe *training* ili waje wafundishe hizi shule ambazo Waziri ameziita amali, zamani tuliziita ufundi na sijui kwa nini amezibadilisha jina? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo ningependa kulichangia hapa, napenda niunge mkono hoja ya Kamati

ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Waziri katika Wizara yake ameruhusu Halmashauri zijenge shule za *english medium,* ameruhusu Halmashauri zichukue walimu ambao wanalipwa na Serikali wakafundishe shule za *english medium.* Halmashauri inakusanya kodi kutoka kwa wananchi, ina maana mimi kama nauza nyanya, nauza mitumba, nauza ndizi, nina duka, unakusanya kodi kwangu, ukishakusanya zile kodi kwenye halmashauri yangu unakwenda unanijengea shule ya *english medium,* halafu unarudi unaniambia kama nataka mtoto wangu asome pale nikulipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliona hili ni tatizo na linaenda kugawa Watanzania. Sasa hivi kuna halmashauri ambazo zimejenga shule za *english medium* na hili ni tatizo nimeona niliseme hapa na liko ni hoja ya Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliwasilishwa hapa Bungeni, lakini nimeona nichangie kwenye Wizara kwa sababu nafahamu hawa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hawawezi wakajenga hii shule kama hawajapata kibali kutoka kwenye Wizara ya Elimu ambayo Waziri ni msimamizi wa sera hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anawezaje kumtumia Mwalimu ambaye analipwa na Serikali akafundishe shule ya *english medium,* halafu utatumia yale mapato ambayo wewe umekusanya kodi kwa wale wananchi walioko kwenye hilo eneo? Hii si sahihi, tunakwenda kujenga matabaka na hatutaki matabaka nchini Tanzania kwa sababu, watakaosoma hapa watakuwa ni wale watoto wenye uwezo na wale watoto wa wafanyakazi. Yule mtu ambaye ulichukua kodi yake ya shilingi 200, anayechoma mahindi, anayeuza mitumba, anayeendesha bodaboda, hawezi akamleta mtoto wake pale kwenye ile shule ya *English Medium. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja nyingine nakaa nikijifikiria, kama Waziri alisema kwamba, anakuja na hoja

humu Bungeni kwamba, Kiswahili si ndio lugha yetu, masomo yafundishwe kwa Kiswahili, kwa nini anaruhusu Halmashauri zijenge shule za *english medium? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni hivyo, basi Kiingereza kifundishwe kwenye shule zote za Serikali kutoka darasa la kwanza, ili twende na usawa na ili tusiwe na matabaka. Suala la halmashauri kuanzisha hizi shule si sahihi, tuachie shule binafsi kwa sababu, wanakwenda kutumia *resources* zilezile za Serikali, lakini wanakwenda kutengeneza mapato, lakini ukiangalia chanzo chake ni hicho nilichokisema. Naona siyo sawa, na sioni sababu. Kama ni hoja kufundisha *english medium* basi namwomba Mheshimiwa Waziri hii *english* ifundishwe kutoka darasa la kwanza kwenye shule zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, tumesema lugha ni biashara, lugha ni uchumi, kama wachangiaji wengine waliopita walivyosema, lakini pia tunakwenda kwenye teknolijia ya kisasa. Unaposema nchi yetu ya Tanzania iendelee kukikumbatia Kiswahili, tuendelee kuwafundisha watoto Kiswahili hayo mambo yalitakiwa yafanyike 1961 tulipopata Uhuru, siyo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, 1961 tulipopata Uhuru ungesema basi tunakwenda na mfumo wa kufundisha watoto Kiswahili kitupu, lakini Kiswahili pamoja na Kiingereza ni *official languages,* ni lugha za Taifa, Kiingereza ni Lugha ya Taifa na Kiswahili ni Lugha ya Taifa. Sasa unapokuja kutoa lugha moja unasema ifundishwe kwa mtindo huu, ili nyingine ifundishwe kwa mtindo mwingine, mimi ninaona siyo sahihi. Ninataka Kiingereza kifundhishwe kutoka darasa la kwanza kwa watoto wote, kwa shule zote ili kila mtoto awe na *competence,* anapokwenda ku-*compete* huko nje kwenye *interview,* mtoto unakuta anajua kitu lakini kwa sababu hakuandaliwa na hakusomeshwa ana-*feel uncomfortable,* kwa sababu anashindwa kujieleza. Na matokeo yetu

tumekuwa tukidai nchi za jirani watu wake wanafanya kazi nje, wanafanya kazi nje kwa sababu wanajua lugha, wanaongea Kiingereza, wanaongea Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, utaendaje kufundisha Kiswahili Marekani, Ujerumani, Sweden kama hujui Kiingereza? Ni lazima ujue Kiingereza ili ukafundishe kile Kiswahili, ili uweze kutafsiri. Mheshimiwa Waziri ninaomba hili ulichukulie uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mengine nitaandika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Rehema Migilla, nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Latifa Juwakali ajiandae.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia kwenye Wizara yetu ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Utukufu wake. Pia ninapenda kumshukuru Rais wetu kipenzi, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa dhamira yake ya dhati kabisa kuhakikisha elimu ya Tanzania inakuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kumshukuru pia Kaka yangu, Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Kaka yangu, Mheshimiwa Omari Kipanga na dada yangu makini sana, Profesa Carolyne Nombo, kwa kazi nzuri sana ambayo

mnaifanya katika Wizara ya Elimu. Tunaona Wizara ya Elimu sasa hivi ina mafanikio makubwa sana ambayo yanakwenda kuleta mageuzi makubwa kwenye sekta yetu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kuna kuongezeka kwa bajeti ya Wizara ya elimu, tunaona walimu wetu wamepewa vishkwambi, tumeona wanafunzi zaidi ya 1,967 walikuwa wamekwama wameweza kurudishwa shuleni, tumeona pia kuna wanafunzi 593 wote hawa wameweza kupata Samia *Scholarship.* Mwenyezi Mungu awabariki sana muendelee kuwatumikia Watanzania kwenye suala la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya mafanikio makubwa tuliyoyapata kwenye sekta yetu ya elimu, ninaona bado kuna changamoto mahali fulani. Suala la kwanza ni uboreshwaji wa maslahi ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwalimu kabisa. Tunapokwenda kwenye suala la uboreshaji wa mitaala na sera, suala hili haliwezi kukamilika vizuri bila kuhakikisha maslahi ya walimu yanakamilishwa na kutekelzwa. Sasa hivi walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, hawana nyumba za kukaa, mishahara midogo, madeni mengi, huku wanafundisha wamerundikana darasani watoto kibao, kiasi kwamba ukiwapima sasa hivi afya za akili walimu wetu haziko sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitaka Serikali kuhakikisha kwamba tunapokwenda kutimiza hii sera na mitaala ya elimu tuhakikishe walimu wanaboreshewa maslahi yao, bila hivi tutakuwa tunapiga *mark time*. Suala lingine ni kuhakikisha kabisa hao walimu wanapewa mafunzo. Sasa hivi walimu wanapewa mafunzo pale tu Serikali inapotaka, tena kuna wengine yaani kuisikia semina mpaka afanye *lobbying,* wakati ni hitaji. Kuna walimu ambao wanataka kujiendeleza wenyewe, lakini hao walimu wanaojiendeleza wenyewe Serikali mnakwepa majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Halmashauri zetu mwalimu akitaka kwenda kujiendeleza inamwambia kabisa mpaka uingie kwenye mpango. Anasubiri kuingia kwenye mpango lakini huo mpango anakuja kupewa barua kwenda mafunzoni anaambiwa atajigharamia gharama za masomo tena iko *bolded* kabisa. Bado huyu mwalimu anapotoka kwenye masomo hathaminiwi, habadilishiwi muundo wake wa mshahara kwa wakati, na bado hata unapofika wakati wa kupanda daraja wakati yuko masomoni wenzake wakipanda daraja yeye hapandi daraja, eti kisa yuko masomoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamkatisha tamaa huyu mwalimu kujiendeleza, lakini bado ataona amepoteza muda wake bure, na ametumia gharama zake. Niombe Serikali tusikwepe hizi gharama. Naomba sana hizi Halmashauri zinaposema uko kwenye mpango, mpango huo ni pamoja na kumpa rushusa na kumsomesha kwa sababu ndiyo jukumu la mwajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu wadau wa elimu kuwekewa vikwazo vingi sana. Mheshimiwa Waziri Serikali ndiyo ina jukumu la kusimamia shughuli za elimu *a hundred percent*, lakini Serikali peke yake haitoshi, inabidi hao wadau wa elimu, hasa *private sectors* waweze kushirikishwa na wamekubali kujitoa lakini wanawekewa vikwazo vingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaona shule za *private* zinafutiwa matokeo eti kisa tu wamefanya udanganyifu kwenye mitihani, labda niulize swali moja, anayetunga mtihani huu wa Taifa si ni *NECTA?* Ni Serikali huyo huyo, Msimamizi wa hii mitihani ni *NECTA,* anapeleka walimu wakasimamie mitihani. Siyo walimu peke yao, kuna TAKUKURU, mgambo, polisi, Usalama wa Taifa, wote hao wanasimamia huu mtihani. Bado anayekwenda kusahihisha ni huyuhyu *NECTA*. Halafu leo matokeo yanapotoka

mnatangaza shule mmezifungia. Kabla ya kuzifungia jitafakarini huko ndani, nani anasababisha haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wazazi tunachangia pesa nyingi sana, tunawekeza hela nyingi sana kwa watoto wetu mnatuumiza wazazi, lakini pia mnawaumiza watoto. Mbaya zaidi baadaye mnawapa mtihani wale watoto kwenye mazingira mengine wamekuja ku-*perform* tofauti na ile mwanzo, *this is shame* jamani. Tunawakatisha tamaa hawa wawekezaji, hebu tuache hii tabia, tuweke mazingira ambayo *private sector* watafanya kazi yao ya kuisaidia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nimeoa eti tumeacha kutangaza matokeo, kuya-*rank* kwa sababu mazingira yako tofauti. Hivi wewe ukipeleka kwenye shule zako walimu wa kutosha, miundombinu ya kutosha na madarasa ya kutosha, wanafunzi watashindwa ku-*perform*? Wanafunzi wata-*perform* vizuri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba hili suala la kutozi-*rank* hizi shule kwa kigezo hicho hapo hatufanyi sawa. Kwa sababu hii pamoja na kwamba ni huduma lakini kwenye sekta binafsi ni biashara. Tunaposema tunazi-*promote* hizi shule, kwani hakuna shule za Serikali ambazo zinachukua wanafunzi *cream?* hazipo? Zipo, zinachukua wanafunzi *cream* kabisa, mnaziita shule maalum, zinachukua wanafunzi *cream.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sasa hivi, kama alivyochangia Mheshimiwa Taska pale, kuna shule sasa hivi Halmashauri na zenyewe zinafanya biashara. Maana yake walimu wa Halmashauri wanalipwa mshahara na Serikali, wengine wanafundisha *private schools,* Serikali haifanyi biashara. Kama inafanya biashara basi hawa wanafunzi wetu na wenyewe tuwafanyie *ranking.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niulize swali, hivi ingetokea shule kumi bora zikawa za Serikali, msingetangaza? Tuwe wakweli. Tunawakatisha moyo hawa wawekezaji wetu, wanaisaidia sana Serikali, lakini tunakuja na sababu ambazo wakati mwingine tusikwepe majukumu yetu, tutangaze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ni ushindani, shindaneni ili ajulikane bora ni yupi. Hauwezi kufanya biashara bila *promotion,* huu ndiyo ukweli. Wekezeni huko miundombinu iwe mizuri, walimu wawe wa kutosha, mtaona matokeo, hata hizi shule za *private* zitaji-*phase out* zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni vyuo vya *VETA*. Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana, tumeona kuna ujenzi wa vyuo vipya vya *VETA* 29 na vyuo vingine 63 vinakwenda kujengwa, hongereni sana kwa huu ubunifu. Ndiyo tunataka sasa haya mageuzi tunayosema tunakwenda kuyafanya yafanyike huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila tunachoomba sasa, *VETA* zilizopo, mfano *VETA* yangu mimi ya Ulyankulu ambayo inawakilisha Halmashauri ya Kaliua, kiukweli imechoka mno, imechakaa mno, haifai. Bado hata karakana hazitoshi. Kozi zinazotolewa kule zilishapitwa na wakati. Hebu tunaomba sasa kwenye hili, haya mageuzi ambayo tunakwenda kuyafanya tuweke kozi ambazo zinakwenda na soko la ajira. Leo kuna kozi ya udereva vijana wengi sana watashawishika kwenda huko, kuna kozi ya saluni, kozi ziko nyingi sana. Tumekazania kozi nyingine ambazo hazitoi ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana walimu wapelekwe huko, kama chuo changu kikarabatiwe, na kilishawahi kutengewa pesa, milioni 638, zirudishwe huko

vifanyiwe ukarabati, walimu mahiri waweze kupatikana ili waweze kuendana na soko la ajira. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mikopo ya vyuo vya kati.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Migilla, kengele ya pili imegonga.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rehema Migilla. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mheshimiwa Latifah Juwakali na Mheshimiwa Maimuna Pathan wajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii ya kuchangia kwenye mjadala huu wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nisichelewe kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa kuweza kuchukua hatua za kimapinduzi katika sekta hii ya elimu ambayo tumekuwa nayo muda mrefu lakini kila wakati tumekuwa tunashangaa kwa nini hatuoni wajasiriamali wakijitokeza, hatuoni watu wakifanya mambo ambayo yametokea maeneo mengine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu na uongozi mzima wa Wizara hii. Kabla sijasema lolote niseme kwamba niliposoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri nilikuwa nasisimka sana kwa sababu kuna vitu vingi ambavyo kusema

kweli ni ubunifu na ni vitu ambavyo vitahitaji nguvu ya kifedha kutekeleza katika kipindi cha miaka hii inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilipoangalia upande wa maduhuli, maduhuli yaliyokusanywa mpaka mwezi Machi, 2023, yalikuwa ni shilingi bilioni 338.2 ambayo ni asilimia 54 ya kilichokuwa kimekadiriwa ambacho ni shilingi bilioni 624.7. Kwa hiyo nikajiuliza kwa nini wakaendelea kuweka maduhuli makubwa hivyo kwa mwaka unaokuja, wameweka shilingi bilioni 667.3, ongezeko kubwa tu, lakini kwa jinsi ambavyo naona maduhuli yamekusanywa mwaka huu naamini hawataweza kufikia *level* hiyo na pengine wangepunguza hayo maoteo ya maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja zangu; kwanza ni kweli kwamba tunaona kwamba kuna upungufu wa watumishi katika sekta ya elimu na sekta ya afya pia tunajua tuna upungufu mkubwa sana wa elimu. Lakini kwanza tujue kwamba tatizo siyo kwamba hakuna walimu Tanzania, walimu wapo, tatizo ni bajeti. Bajeti ina ukomo, ina *constraints*, huwezi kuweka pesa zote mahali pamoja na wakati kuna mahitaji mengi kwenye sekta nyingine za kilimo, maji  na kadhalika na kote kunahitaji fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bajeti ina ukomo na kwa sababu Serikali haiwezi kusema tunaajiri leo kila mtu anayetaka walimu 200 au 300 wapate. Kwa hiyo mimi na-*sympathize* sana na uongozi wa Serikali, kwamba tumeji-*overstretch* sana, tumejiongeza sana kwa kuingiza *concept* ya *universal primary education* na *universal health care,* siyo kitu ambacho hakina gharama, gharama zake ni kubwa. Nchi nyingi zilizoendelea hazijaweza kufanya mambo haya makubwa ambayo Serikali yetu inafanya, ndiyo sababu kweli tunatakiwa tuipongeze tumeji-*overstrain* lakini bado tunaendelea na ndiyo tunajikongoja hivyohivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie kwa mfano katika upungufu wa walimu, mimi nafikiri kwamba tujiongeze zaidi. Kwanza kuna tatizo moja la kwamba walimu wale walio mtaani bado hawajapata uzoefu. Sasa kwa sababu hiyo mimi nina-*suggest* kwamba wale ambao wanatakiwa wastaafu kwa miaka 60 tuongeze kidogo ule muda wao wa kustaafu hata wakifika 65, lakini wale wana uzoefu na tukiwa-*refresh* kidogo wanaweza wakaendelea kufundisha, hasa yale masomo ambayo ni magumu kidogo kufundisha kama masomo ya sayansi, hesabu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo, hatukujifunza wakati wa *Covid* watu walijifunza namna gani? walitumia *artificial intelligence*. Mahakama imeweza kutengeneza mfumo ambao unatafsiri Kiswahili kwenda Kiingereza hapo kwa papo. Kwa hiyo, wakitoa ile hukumu ya Kiingereza na ya Kiswahili inatoka hapohapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna mambo mengi yametokea duniani jamani, huku tunakoenda kweli ni kutumia teknolojia kufundisha, siyo lazima kuwe na mtu asimame pale. Kutakuwa na *robot* anafanya hesabu zake, kutakuwa na mtu mmoja anaangalia tu vizuri watu wamekaa wanasikiliza na baadaye kusaidia ku-*interact*. *Otherwise* mimi naamini katika miaka mitano inayokuja mtashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *artificial intelligence* inakwenda mbali sana na *internet* inakwenda mbali sana. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kujibana sana, tujue kwamba kuna uwezekano wa kupunguza gharama za uendeshaji, siyo tu kwenye elimu lakini pia kwenye afya kwa kutumia mifumo hii ambayo inajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Serikali pia imeona umuhimu wa kutia mkazo kwenye shule za awali, shule za awali mnajua hazikuwepo, zilikuwepo za kudanganya danganya hizi za *private* na nini, lakini shule za

awali *proper* hazikuwepo na ninashukuru sana Wizara imeweza kutupa shule moja ya mfano pale kwenye Kata ya Kahe Magharibi kule Vunjo, lakini ukiangalia ile shule ilivyowekwa ni shule ambayo kweli watoto wengine wakienda wanaona wivu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kuna mkakati gani sasa wa Serikali kuhakikisha kwamba kwenye kila shule ambayo ni ya msingi kuna shule ya awali ya kuanzia wale wadogo ili kuweza kutekeleza sasa huo mkakati ambao pia watu wengi wanasisitiza kwamba uelewa wa mtoto unakuzwa kuanzia akiwa na miaka miwili au mitatu, siyo miaka mitano halafu hatajua kitu kabisa. Naomba hilo liangalie kwa sababu ni jambo ambalo ni la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo, kutekeleza hii mitaala mipya siyo kitu cha kufanya kwa siku moja, ni kitu ambacho kitahitaji muda wa mpito. Hatuwezi kusema mwaka huu tunaanza, hapana, hakitakwenda. Kwa sababu tunahitaji kuwaandaa hawa walimu na kuwa *reskill* na kuwa *retune* hawa walimu ambao tunao. Kwa sababu lazima tuwape nyenzo mpya za kufanyia kazi. Lazima tuwape elimu mpya namna gani kwa mfano mtoto mdogo unaanza naye, waangalie kipindi cha *Ubongo Kids,* mimi naangalia kipindi mpaka nashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule mtu anayetengeneza Kipindi cha *Ubongo Kids* ambacho kipo kwenye runinga nyingi za hapa kwetu, utaona kitu gani wanafanya, unaona wanafundisha watoto mpaka unashangaa unasema hata mtoto wangu akipita hapa akiangalia ataelewa maana ya utu ni nini na wanauliza maswali, na hiyo *issue* ya *continuous assessment* unaona kabisa pale inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninashukuru sana kwamba pamoja na hiyo nafikiri Serikali iangalie namna gani itaingiza kipindi hiki cha mpito kabla haijaanza kutekeleza.

Maandalizi gani, tunahitaji bajeti kubwa, hii bajeti waliyonayo Wizara hii ni ndogo kwa kipindi hiki ambacho tunakwenda. Kwa hiyo naamini kwamba watapata nyongeza zaidi ili waweze kujiandaa na waandae walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *VETA*. Wanasema wanajenga vituo vya *VETA* kwenye Wilaya. Wilaya yetu ina Jimbo moja Moshi *Municipal* halafu ina Halmashauri ya Moshi Vijijini ambayo ina Majimbo mawili. Sasa unaposema unatoa *VETA* moja inaenda pale Mjini Moshi basi. Kwa hiyo yale Majimbo mengine hayana kituo cha *VETA* ni makubwa watu chungu nzima. Unajua mtu anakwenda kusoma *VETA* ukamwambia achukue *transport* kila siku aende Mjini kusoma inakuwa vigumu sana, gharama zinakuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba tuangalie upya, kwamba pale ambako una Majimbo matatu au mawili kwenye Wilaya basi tuangalie namna gani tuta-*allocate* hivyo vituo vya *VETA* ili viweze kunufaisha watu. Hakuna sababu ya kuwa na kituo cha *VETA* ambacho kukifikia yule mwanafunzi lazima atumie shilingi 5,000, itakuwa ni kazi ngumu, kama kule kwangu ni vigumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namuomba Mheshimiwa Waziri aangalie hilo suala ili aweze kuona kwamba kweli wasituwekee kila kitu pale Mjini, Mimi sichukii kuwekwa Mjini lakini ukweli ni kwamba nataka tujue kwamba *distribution spatially* itakuwaje, *in terms of spatial benefits.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nashangaa tunavyozungumza ufundi stadi. Hivi hakuna vyuo vya kilimo? Kwa nini hatuna vyuo vya kilimo vile ambavyo tunachukua kwenye hii kada ya kati? Kama vipo, ni vichache. Watu watajifunza saa ngapi? Au kilimo hatujifunzi? Au tutajifunzia huko huko tulikozaliwa? Sasa hivi kimekuja kilimo cha umwagiliaji, kilimo ambacho ni chenye tija, kinaendeshwa na watu wanaofundishwa na wakajua faida zake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwamba tunapozungumzia Vyuo vya *VETA,* tujaribu kuweka vyuo vya kufundisha kilimo kwenye ngazi ya chini kabisa kuanzia hata darasa la saba au hata kuanzia darasa la tano kwenda juu huko, na wale wanaobobea zaidi wanakuwa ndio wataalam, mabwana shamba na kadhalika, tunawapeleka, lakini usitaje tu vituo hivyo. Tena vinahitaji hela sana hivyo vya *VETA*. Hivi vya kilimo hata havihitaji nyenzo nyingi sana, ni vitu vichache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kingine kwamba pengine kwenye suala zima la bajeti hii niliangalia kwamba, pengine ili kuleta tija kwenye elimu, walimu kuendelea kuripoti kwa TAMISEMI au kusimamiwa na TAMISEMI, naona hiyo, kwanza unapoteza kabisa mwelekeo wa walimu hapa. Ila kama wenzangu walivyosema, walimu kusema kweli ingefaa waangaliwe na wawe *graded* na Wizara ya Elimu, wasibakie tu kwenye sera lakini walimu wawe pale kwa sababu tutajua jinsi ya kuwafundisha na kadharika nakadharika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimea, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mheshimiwa Maimuna wakati anajiandaa.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwa wazima. Kipekee sana, naomba niendelee kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake makubwa na namna alivyojipambanua katika Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema vijana wa Tanzania tunamwelewa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunamaanisha, na tunaposema zaidi tunamwelewa katika Wizara ya Elimu, tunamwelewa sana; na tunaposema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejipambanua kwenye elimu, tunamaanisha kwamba ameyatafsiri maono yake kwa vitendo, huku akiamini kwamba, ili kuwawezesha vijana wa Tanzania, lazima tuwe tuna *human capital* na *physical capital. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi, Wabunge wa Majimbo hapa wamejinasibu sana, wamesema, katika maeneo mbalimbali ya majimbo shule nyingi zimejengwa, lakini siyo shule tu, hivi karibuni tumeiona Wizara ya Elimu imeendelea kufanya maboresho mapya ya mtaala wa elimu. Hiyo inaonesha jinsi gani Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa anataka Wizara ya Elimu iendelee kuonesha umahiri na ubora wa *human capital*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema *human capital,* majengo yanajengwa, miradi ya elimu inatekelezwa, lakini hatuwezi kuiboresha elimu kama hatuna uwezo wa kuendeleza *skills and knowledge* kwa wanafunzi wetu wa kitanzania. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunawashukuru wenzetu wa Wizara ya Elimu, kwa sababu kwanza wameendelea kuwa wasikivu na pia tunawapongeza sana, wameendelea kutoa ushirikiano mzuri kwetu sisi Wabunge huku wakiamini kwamba sisi kwa pamoja lengo letu ni kuwasaidia vijana wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, pia nataka niseme kwa dhati ya moyo wangu, vijana wa Tanzania wamenituma niseme kwamba wanampongeza na

kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Bodi ya Mikopo kwa kutuongezea kiasi kikubwa cha kujikimu kwa Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Rais amejipambanua na kuona kwamba sasa elimu yetu sasa ni sayansi na teknolojia. Hivi karibuni tumewaona wenzetu wa Wizara ya Elimu wameenda kutoa vishikwambi nchi nzima, na vishikwambi hivyo vimetolewa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Tunamshukuru sana na tunampongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zangu leo zitajikita katika maeneo matatu. Jambo la kwanza nalotaka kulizungumza, Mheshimiwa Waziri sasa hivi tupo katika *formulation* ya mitaala. Katika mitaala hii, yako mambo mengi yamezungumzwa, lakini nilitamani sana, na ninajua kwamba katika mitaala hiyo kuna vitu vingi ambavyo vinaenda kuonekana kwamba ni maboresho na vitakuwa vipya. Naomba niwazungumzie walimu. Walimu wanatakiwa nao wapate *skills* na *knowledge* mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Wizara ya Elimu hapa walituambia, na katika majibu ya msingi walikuwa wanajibu wakisema kwamba, wamepata kibali cha kuajiri walimu wapya. Nilikuwa naomba sana tuwazingatie na hata wale walimu walio katika *site,* tuwatengee fedha na bajeti ya kutosha ili nao wakapate mafunzo ya ziada waweze kuendana na mahitaji ya walimu ambao tunawataka katika maboresho ya mitaala yetu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, pia kuna jambo, hili sikuliona sana kwenye Wizara ya Elimu tu, hata katika Wizara nyingine na sekta nyingine. Tunaposema *promotion,* tunamaanisha kwamba, kuwa- *motivate* wale ambao wanatoka *stage* moja kwenda *stage* nyingine. Kumekuwa na changamoto moja, wenzetu walimu

wanapoomba vibali kutoka kwenye Wizara ya Elimu na Wizara nyingine tofauti, pengine mwalimu amemaliza shahada ya kwanza, ameomba kibali anakwenda kufanya shahada yake ya pili, lakini anaporudi kwenye kituo chake cha kazi kumekuwa kuna changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayojitokeza, hakuna aina yoyote ya *promotion* ambayo anaipata. Jambo hili limekuwa ni changamoto na linaweza kuwafanya wanafunzi wetu wengine wasizidi kwenda kujiongeza kwa sababu wanajua, anaporudi kwenye kituo chake cha kazi hakuna chochote kinachoenda kumwongezea yeye, na hakuna tofauti baina yake na yule aliyemwacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waziri wa Elimu na Wizara yetu ya Elimu tulichukue hili tulibebe na liwe kama ni *promotion* kwa wanafunzi wetu au wafanyakazi wetu ambao wanatoka katika maeneo ya kazi wanapoenda kusoma na wakirudi ili waweze kuwa kama wana *motivation* fulani kwa sababu wanajua, mimi nimemaliza *Degree,* nikienda kusoma *Masters* nikirudi, kuna kitu kidogo kinaweza kikawa kimeongezeka na hiyo inaweza ikawasaidia wengine ili kuweza kupata *promotions*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza vizuri sana hapa bajeti ambayo ilikuwa inasomwa. Nilitarajia sana, kwa sababu mmoja wa Mbunge ambaye alikuwa anauliza maswali mengi kuhusiana na vyuo vya kati, nilikuwa ni mimi. Nilitarajia sana leo au jana ikisomwa bajeti hapa, tuone walau kuna kiasi cha fedha ambacho kimetengwa kwa ajili ya vijana wa vyuo vya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza vyuo vya kati, hivi ndiyo vyuo ambavyo vinarejesha kwa haraka mikopo. Simaanishi kwamba vyuo vya juu wakipewa mikopo hawarejeshi kwa haraka, Hapana, lakini kwenye vyuo vya kati *return* yake inakuwa ni ya haraka, kwa sababu

mwanafunzi anachoenda kukisoma ndicho kile anachoenda kukifanyia kazi katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vyuo vya kati, huku ndiko tunapowapata vijana wanaojifundisha *driving*, ndiyo tunawapata vijana ambao wanajifundisha masuala mbalimbali, umeme na vitu vingine. Akitoka pale, mwanafunzi yule tunamtarajia aidha kwa kujiajiri mwenyewe au hata kwa kwenda kuajiriwa. Hata kama hakuweza kuajiriwa, atakuwa ana uwezo wa kujiajiri mwenyewe. Akiwa na uwezo wa kujiajiri mwenyewe, maana yake *returns* ya ule mkopo itakuwa ni ya haraka zaidi kuliko na wale wengine ambao wanasoma kwa ajili ya kuja kurudisha ile *return* baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kama Wizara, hili tulichukue kwa uzito wake, na Wabunge bahati nzuri wamelipigia kelele sana humu ndani wakiomba kwamba hili jambo tulibebe na tuweze kuwasaidia wenzetu ili waweze kupata mikopo katika hivi vyuo vya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka nimalizie katika maslahi ya walimu. Maslahi ya Walimu bado hayaridhishi. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri hili mlichukue, na muwe na wivu na watendaji wenu wa Wizara ya Elimu. Hivi leo ikitangazwa kazi ya *TRA* na kazi ya Ualimu vijana wengi watafukuzia kazi ya *TRA*. Kwa nini wafukuzie kazi ya *TRA* wasifukuzie katika Wizara ya Elimu? Maana yake inaonesha bado masilahi ya walimu yapo duni, na yapo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi walimu tunasema, kazi hii ya ualimu, malipo yake yapo kwa Mungu. Basi tunaomba walau kidogo wale walimu nao wapate moyo wa kuendelea kufundisha vizuri. Muda mwingine hapa unaweza ukasema mwalimu anafundisha shule mbili; leo yupo *private,* kesho

yupo katika shule ya Serikali, ni kwa sababu bado masilahi yao ni madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Latifa Juwakali. Nilimtaja Mheshimiwa Maimuna Pathan, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, ajiandae.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja kwenye Wizara ya Elimu. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi yake ya uhai na kufikia siku hii ya leo. Pia naomba nitoe sifa nyingi sana kwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa sana anazozionesha kwa upande wa elimu. Ameweka majengo mengi sana, madarasa ya kutosha, kwa kweli anastahili sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Waziri wa Elimu, ndugu yangu Profesa Mkenda na Msaidizi wake na Katibu Mkuu, Dada Carolyne na wasaidizi wake, kwa kweli wanajitahidi wanafanya kazi kubwa sana. Tumeona mitaala hii iliyotoka, kwa kweli kazi yao inaonekana, tunaendelea kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu mambo yawe mazuri ili nasi tufaidi, na nchi yetu Tanzania iwe vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuunga mkono hoja zilizopo mbele yetu mezani. Pili, nawaunga mkono Wabunge wengi waliotoka kuongea, akiwepo dada Latifa sasa hivi. Mitaala hii mipya inayokuja, tujitahidi sana tuwekeze kwa walimu. Tusipowekeza kwa walimu tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Walimu wapewe semina, wapewe mafunzo mbalimbali, tuache tabia ya kuanza kubagua. Najua Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake huko Wizarani hawana nia mbaya, lakini huku chini ukishuka, kuna mambo yanaendelea siyo mazuri. Kuna shule nyingine

utakuta kuna mwalimu fulani na mwalimu fulani wanajua kila kizuri kitakachotokea wao wanakuwepo, kila semina itakayotokea watakuwepo, kwenye kusimamia mitihani, watakuwepo, lakini kuna baadhi ya walimu masikini wa Mungu wananyanyasika kama wao ajira yao walikuwa wameenda kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa kutumia wafanyakazi wake walioko Wizarani, afuatilie vizuri haki itendeke kwa walimu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wakipata mafunzo vizuri na pia haki zao za msingi, naomba zikumbukwe. Wakati mwingine unaweza ukaenda kwenye shule za sekondari na za msingi, ukasikitika juu ya viti walimu wanavyokalia na meza. Kwa kweli wanakaa kwenye ofisi mbaya, viti vya ajabu, vimevunjika vunjika, meza ziko ovyo ovyo. Wakati huo tunawapa watoto wetu wawafundishe, unategemea watafanya kazi vizuri kweli! Basi tujitahidi. Kama mama yetu Rais alivyoleta majengo mazuri, na yale ya zamani tuyaboreshe na ofisi zao tuziboreshe. Tujitahidi. Tuweke agent ambaye atakwenda kurekebisha...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

## TAARIFA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa anayechangia kwamba ni kweli, walimu wanatakiwa waboreshewe mazingira, kwa sababu kuna shule nyingine, ofisi za walimu ziko chini ya mti. Yaani mvua ikinyesha, kila kitu kilichoko pale kinapeperuka.

Kwa hiyo, waboreshewe mazingira, yaani wawe na ofisi ambazo zina *furniture*. Unakuta wakati mwingine walimu wengine wanabeba viti kutoka nyumbani wanaenda navyo mashuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuunga mkono mchangiaji kwamba Serikali iwajali walimu, maana yake ndio wanatengeneza wataalam mbalimbali, hivyo iwaboreshee maofisi na ikiwezekana wawekewe na *AC* kabisa ili wawe na fikra nzuri wanapofanya kazi hizi za ualimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili taarifa hiyo, ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala moja, kuhusu Chuo Kikuu cha Iringa, ambacho zamani kiliitwa *Tumaini University*. Naomba Serikali yetu kwa kupitia Waziri wetu mpendwa, itupie macho mawili iangalie sana kile chuo, kina matatizo makubwa sana. Chuo hicho *system* yao ya kulipa ada na *administration* kwa ujumla iko *weak so weak,* haiko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmojawapo wa wahanga wa Chuo kile cha Tumaini cha zamani, sasa hivi kinaitwa Chuo Kikuu cha Iringa. Kuna watoto ambao walikuwa wanasoma pale walikuwa wamefanya malipo. Wanapofanya malipo, namba wanazopewa za kulipia, wanapewa na Wahasibu na watu wa *IT,* kumbe wanapewa namba *fake* za malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi wengi tunajua hali zao kiuchumi. Watoto wamefanya malipo yale, kumbe malipo yale kulikuwa na makundi mawili; wengine hawakujua,

walijua ndiyo namba halisi za kulipia, zaidi ni wale wa mwanzo mwanzo, lakini kuna wengine walikuwa wamekaa na hao baadhi ya wahasibu, wakaamua ku-*fake* yale malipo yakalipwa. Ilipofika kipindi cha kufanya mitihani, watoto wengi wakaanza kudaiwa. Wale ambao walikuwa wahawajui, wakasema tumelipa, wakapeleka risiti zao, lakini ikaonekana zile akaunti walizolipia ni *fake*. Baada ya kufuatilia mpaka wazazi, wakaamua wawaruhusu wafanye mitihani lakini wakaambiwa matokeo yenu yatazuiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli matokeo yalizuiliwa, baadaye uongozi wa chuo ukaanza kufuatilia tatizo ni nini kwa kuwaambia wanafunzi waliopata changamoto hiyo ambao ni zaidi ya 40, (na orodha ninayo Mheshimiwa Waziri nitakupatia), kwamba waandike barua za maelezo za kujieleza. Wanafunzi wale waliandika barua za kujieleza. Kweli kuna wengine walikuwa hawajui kinachoendelea, walioamua ku-*tamper* ni baadhi ya wafanyakazi ambao sio waaminifu. Kuna wengine baada ya kufungiwa matokeo yao, wakaambiwa tu wewe ume-*sup* somo fulani na somo fulani unatakiwa uje urudie mtihani, lakini kwenye mtihani unatakiwa ulipie tena ada kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri, mtu kama mimi, angalau namshukuru Mungu nina uwezo wa kulipia ile ada mara ya pili: Je, yule mkulima au yule mama aliyeko kule ndani na baba aliyeko kule ndani wenye uwezo wa chini, wana uwezo wa kulipia kweli mara ya pili jamani? Hiyo ni haki kweli kwa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipofanya vile, watu wengine wakalipia, mmojawapo ni mimi nikalipia mara ya pili. Baada ya kulipia mara ya pili, tena niliwafuatilia sana kutaka wanipe hiyo akaunti hiyo ya uhakika. Nilisumbuana nao kwa muda mrefu sana, mpaka nikaamua kumshirikisha rafiki yangu Mheshimiwa Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini

anisaidie. Baada ya kulipia mara ya pili, hawakutaka kufungua matokeo ya Watoto. Ilivyoanza *semester* nyingine, tukaanza kuwasiliana nao kusumbua, kwamba mlisema tulipie mara ya pili, tumeshalipia, mbona hatuelewi kinachoendelea?

Majibu yao ni kwenye simu, "mtoto wako amefaulu aje." Matokeo yako wapi? Tutajuaje kama amefau? "Aje baada ya kufanya marudio ya mitihani anafaulu tu, aje tutakupa matokeo baadae." Sasa unajua ukifuatilia muda mrefu kila siku unaona kama utakuwa ni kero unaamua umruhusu mwanafunzi nenda chuo ukasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tunafanya ufuatiliaji pale chuoni kwa Mkuu wa chuo, unapewa namba ya Mhasibu, unapewa namba ya Mwanasheria yaani tuna namba kibao za pale Chuo Kikuu cha Iringa. Tukiwasiliana nao wanapiga dana dana "sasa hivi lipeni hela tu ya *hostel* msilipe ada lakini mtoto atasoma". Anasoma vipi? Basi tukaona tuwasikilize wao walichosema. Wazazi wakalipia *hostel* wanawapa na watoto hela za chakula lakini *coursework* zao hazirekodiwi wala hawajasajiliwa. Tukawa tunafuatilia kila siku muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwishoni walipoona tunafuatilia sana wakasema "*senate* haijakaa kutoa majibu japokuwa walishafaulu subirini msiwe na wasiwasi majibu yatatoka". Ni lini? Baada ya kuona nimemshirikisha Mbunge wa Iringa, wakaanza kushtuka sasa, wakaanza ku-*forge* barua ku-*backdate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina barua hapa na baadae nitaomba nimpatie Waziri wa Elimu. Wakiwa wanaandika barua hii ambayo imeandikwa tarehe 5 Desemba, 2022 wakati nimeulizia mpaka Machi wakawa wanasema bado *senate* haijakaa, wamejisahau wamenijibu hivyo. Pia, wakasema kwamba kikao kilichokaa tarehe 14 Octoba, 2022

kimeamua Kumfukuza huyo mwanafunzi. Naomba ninukuu hivi "*This is to inform you that based on your abscondment from studies, The university Senate sitting on 14th October 2022.* Wakati waliniambia hizo tarehe mpaka Machi mwaka huu nawasiliana nao wakasema bado *senate* haijakaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wakasema kwamba unaweza ku – *appeal before 10th January 2023*. Wakati huo wanasema unaweza ku – *appeal before* hiyo ni Machi nimewasiliana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barua ni halali, *forgery* au ni nini? Ina maana kwenye ofisi nyingine bado mpaka sasa hivi kuna *forgery* za ajabu namna hii kweli? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umeisha?

**MWENYEKITI:** Ndio kengele imelia mara ya pili.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nitaonana na Mheshimiwa Waziri wa Elimu kumpatia *document* zote.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani na Mheshimiwa Philipo Mulugo atamalizia.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye wizara hii Muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kutoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita. Rais wetu Dkt

Samia suluhu Hassan, tangu alipoingia madarakani kati ya sekta ambazo aliziangalia kwa jicho la tatu ni sekta hii ya elimu. Mapema Kabisa alitoa msimamo wake na maelekezo kwamba anataka maboresho yafanyike lakini hakuzungumza tu aliendа kwa vitendo. Ametenga fedha nyingi amakwenda kuboresha maisha ya wanafunzi vyuoni, ameongeza wigo wa elimu bila malipo. Kwa hiyo, sisi vijana na watanzania kwa ujumla tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa maboresho haya ambayo ameyafanya kwenye elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri wewe pamoja na Wizara nzima, Naibu Waziri wetu, Katibu Mkuu na watu wako wote tunawashukuru sana na kuwapongeza. Kwa sababu rasimu hii ya maboresho ambayo mmetuletea kwa kweli inatia moyo. Kimekuwa ni kilio cha muda mrefu sana cha watanzania kwa ujumla na hata Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi, kwamba tuna maboresho ya haraka sana yanahitajika kufanyika kwenye mfumo wetu wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru hata Sera yetu ya elimu bado na yenyewe ina *recognize* kwamba tunayo changamoto kwenye mfumo wetu wa elimu. Hii rasmu ambayo mmetuletea imekuwa *exhaustive,* inatia moyo kwamba tukienda kweli katika utekelezaji huu na mkiendelea ku-*incorporate* mawazo ya Wabunge wengi ambayo wanaendelea kutoa basi naamini kesho yetu ni bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia kwenye masuala machache tu, la kwanza; nilishauri katika mchango wangu wa kwanza nilipoingia Bungeni hapa kwamba, tunahitaji kuwa na *agenda* ya Kitaifa. Nitoe mfano kwenye nchi za wenzetu kwa mfano China, wao walikuwa na agenda kwamba ifikapo mwaka 2025 wangependa *industrial product* zote asilimia 75 zinazokuwa *consumed* duniani zote zitoke China na kwa kiasi kubwa nasema wamefanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunazungumzia Tanzania ya viwanda, tukizungumzia kilimo, kiwanda kinachozalisha watu ambao wanakwenda kwenye sekta hizi ni Wizara hii ya Elimu ndio inatutayarishia watu hawa. Nafikiri kwa namna ambavyo tumeandaa hii rasmu yetu na kwa namna ambavyo na *quote* mwanzo kabisa wa sera ambayo ni rasimu inasema "Serikali imekusudia kuleta mapinduzi ya kiuchumi ili kuibadili Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025" na inasema inatarajia kuleta maendeleo ya haraka ya rasilimali watu kwa kutayarisha idadi ya kutosha ya watanzania walioelimika na kupenda kujieleimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mawanda mapana sana tusiogope kuota. Tunapenda Tanzania tuione wapi ili Wizara hii ya Elimu itusaidie kuandaa watu hao. Tunapenda Tanzania leo hii tukizungumza duniani kama tunataka nini tuje tukipate Tanzania na wizara hii ndio wakati wake huu na hasa muda huu ambao tunafanya mapitio mtuandalie watu wa kwenda katika mlengwa huo. Kama tunasema tunataka Tanzania ya viwanda tunatakiwa tuanze kuanzie *level* ya chini kuanda watu hawa ili mwisho wa siku tuone Tanzania kweli ikielekea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana na wala hatutakuwa tumeji–*stretch* sana tunatia hatari ya kuwa *jacks of all trades and master of none.* Lazima tuweze ku–*master.* Sasa hivi Afrika inaongelea eneo huru la biashara Afrika. Lazima tuseme sisi Tanzania tukinda katika hii *free movement of good, free movement of people* tunataka Tanzania tuwe na *speciality* ipi? Ndio wakati sasa hivi wa kuandaa kupitia mabadiliko hata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; niombe sana sana Wabunge wengi wamechangia sana juu ya suala la lugha. Lugha yetu ya kitanzania ni lugha ya kiswahili na ni lugha ambayo tunaipenda *we are very proud* na lugha yetu lakini

ni lazima tuangalie mabadiliko ya kidunia tunayoenda nayo. Sasa hivi tunakwenda kwenye dunia ambayo ni *free movement of people,* sio Afrika tu lakini dunia nzima kwa ujumla. Sasa tuki-*incorporate* lugha ya kiswahili peke yake tunamtenga mtanzania na dunia nyingine. Ni muhimu sana. Tuendelee kuitunza lugha yetu lakini tuendelee kuangalia lugha ambazo zitamfanya mtanzania aende katika dunia nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze kwa sababu katika rasimu hii mmekwenda mbali. Mmetoka katika *debate* ya Kiswahili na kiingereza mmekwenda kwenye kiarabu, kifaransa na kichina. Niwapongeze kwa sababu huko ndiko dunia inakotaka twende, kwenye hilo mmefaulu. Niombe mmesema anaetaka kufundisha kiswahili aombe kibali aruhusiwe anaetaka kufundisha kiingereza aombe kibali aruhusiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunahitaji kufanya marekebisho katika hayo. Kwa sababu kama tunataka tuifungue Tanzania na kimsingi hii ni *direction* amekwisha tuonesha Mheshimiwa Rais anataka Tanzania tusikae kama kisiwa twende duniani. Sasa tukisema tu kwamba kuna baadhi ya wanafunzi watafundishwa kiswahili peke yake tunawatenga watu hawa na hawawezi kwena duniani, nadhani katika hili tuliangalie upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine katika marekebisho haya tunayofanya *stakeholder* namba moja ni mwalimu. Yaani hatuta *achieve* chochote kama tusipoangalia maboresho katika hali za walimu. Wabunge wengi wamezungumzia katika kuboresha hali zao za kufundisha na mazingira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko *concerned* zaidi kama tunapokwenda kwenye mabadiliko haya ambayo kwa kiasi kikubwa sasa yanakwenda kumfanya mwanafunzi

aweze kupambana na mazingira yake. Je, anaemfundisha kwenda kupambana na mazingira yake yuko *well equipped* kumfundisha mwanafunzi ili akitoka akapambane na mazingira yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa walimu tulianzisha mfumo wa *competence based* lakini *as we speak* mpaka leo *less than 40 percent ya* walimu walioko wameweza kupewa elimu ya kutosha kuweza kurudisha hizo *knowledge* kwa wanafunzi. Je, tunapokwenda kufanya maboresho haya, walimu tulionao wanakwenda kupata hizo *knowledge* kwa mfumo upi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, bado tuna upungufu mkubwa sana wa walimu. Tumewekeza sana kwenye miundombinu, tumewekeza sana kwenye kuboresha mazingira ya wanafunzi kusoma lakini bado tuna upungufu mkubwa sana wa walimu. Kama ambavyo tuliifanya agenda ya kitaifa kwamba tunatenga bajeti ya kutosha kwenda kuongeza madarasa, tunatenga bajeti ya kutosha kwenda kuongeza madawati, ningependa pia tuifanye *agenda* ya makusudi kwamba tunatenga bajeti ya kwenda kuongeza idadi ya walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sekta inayoweza kusimama kama kiwanda kinachotuzalishia wataalamu hakitasimama na kiwanda hiki si kingine ni Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kutia msisitizo. Nashukuru kwa sababu rasimu hii imeanza kuonesha msisitizo wa mafunzo ya TEHAMA kuanzia *level* ya chini kabisa elimu ya awali mpaka mwisho. Lakini sasa dunia ya leo inakwenda kwenye *information technology* zaidi, dunia ya leo inakwenda kwenye *artificial intelligence*. Ni muhimu sana kuanzia elimu ya chini tuanze kuwafundisha wanafunzi wetu *information technology*. Tena sio vile vitu vya awali ambavyo tulikuwa tunajifunza mwanzoni kwamba, *label* hii ni *CPU*,

hapana. Tunahitaji kwenda ndani zaidi kwa sababu dunia ndiko ilikofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kimsingi *the future is closer than we think*. Kwa sababu wenzetu sasa hivi wanakwenda ku–*substitute* kabisa binadamu kuweka mashine. Sasa sisi tunawaandaaje watu wetu kwamba tunakwenda kuwa *substituted* tuanze kutumia mashine. Ni lazima tuangalie kwa karibu sana na napenda tusiweke msisitizo huu vyuoni tu, tuanzie kwenye elimu ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe tu *data* ndogo, mwaka 2015 wanafunzi waliokuwa wanamaliza shule za sekondari walikuwa ni wanafunzi milioni 1,648,000+ lakini mwaka 2019 sasa hivi wamemaliza wanafunzi milioni 2,185,000 hawa ni wanaomaliza elimu ya sekondari. Lakini wanaotoka vyuoni, mwaka 2015 walitoka wanafunzi 65000 tu kutoka milioni 1,600,000 wakatoka vyuoni wanafunzi 65,000, 2019 kutoka milioni 2.1 wakatoka vyuoni wanafunzi 87,000 hao zaidi ya wanafunzi milioni mbili wako wapi? Maana yake tumewaacha kwenye *level* za chini. Kama tunaanza kuwekeza lazima tuwekeze kuanzia *level* ya chini ili yeyote anayeweza kuishia chini basi atoke akiwa na *skills* za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzunguzmia wanafunzi wetu Watoto wa kike. Tulipitisha hapa katika Bunge lako Tukufu Sheria ambayo inatoa adhabu ya miaka 30 kwa watu ambao watawapa ujauzito Watoto wetu wa kike ambao wako shuleni. Sheria hiyo ilikuwa ni nzuri na na malengo yalikuwa ni mema. Lakini Sheria ile pia ilipata *resistance* kwa kiasi fulani kwa sababu wanaharakati waliona kwamba tunatoa adhabu upande mmoja wakati wakosaji wanaweza kuwa wawili au huyu binti akijifungua basi huyu bwana yuko gerezani hivyo huyu mtoto atalelewa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachelea kusema kwamba tulishindwa kuangalia kitu kingine ambacho kingeweza kuwa matokeo ya jambo hili. Kitu hicho ni kama kifuatacho;

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tafiti zinaonesha kuwa watoto wa kike wana *invest* zaidi kwenye kutokuonekana na mimba kuliko kuonekana na mimba. Kwa maana ya kwamba watoto wa kike sasa hivi wanatumia vidonge vya uzazi wa mpango, watoto wa kike wanatumia vidonge vya kutoa mimba ili asionekane na mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiangalia katika hii rasimu mpya uliyotuletea hakuna elimu ya kujitambua. Tumesahau kumuelimisha mtoto wa kike, kujitambua kuwa na *self-awareness,* kuwa na *self-respect* ili asiweze kuingia katika vitendo hivyo ku–*begin with*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kama tuna *risk* sana kuwa na wanawake ambao watakuwa na matatizo ya *cancer* za uzazi, watoto ambao hawana maadili japokuwa mimba hatuzioni. Ninaomba sana katika hii rasimu mpya ambayo tunaitengeneza tuiangalie upya ili tuweke elimu ya kujitambua turudishe watoto wa kike katika maadili ya kitanzania, turudishe watoto wa kike katika kujitambua kwamba hili jambo si sahihi kuanzia mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani. Nilimtaja Mheshimiwa wetu wa mwisho ambae ni Mheshimiwa Philipo Mlugo.

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa niweze kuchangia Wizara hii ya Elimu lakini *before that* nitoe kwamba ni mdau wa elimu

na ni mwalimu na ninamiliki shule. Kwa hiyo, nitakayoongea hapa nayaishi kwa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hapo ni lazima tuelewe kabisa kwamba Awamu hii ya Sita toka tumepata uhuru ukienda huko vijijini, kama Mbunge na-*declare* kabisa kwamba tumepeleka fedha nyingi sana kwa ajili ya shule zetu za msingi na sekondari. Hata kwenye kata yangu nilikozaliwa Udinde Kata ya Udinde, nimepewa milioni 600 na Serikali na wananchi wamejenga shule na wamenipa heshima inaitwa Mulugo Sali**.** Sasa hii ni heshima kubwa nitakufa lakini jina litabaki. Kwa hiyo, lazima nimshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Pfofesa Mkenda na Naibu Wake Kaka Kapinga, wanavyoshirikiana vizuri siku hizi na shule binafsi. Tumekaa baadhi ya vikao mara mbili mara tatu tofauti kabisa na miaka ya nyuma ilikuwa mkiandika barua Wizara ya Elimu mkae na shule binafsi wanaogopa kabisa kukaa. Sijajua walikuwa wanaogopa nini? Nadhani Mheshimiwa Profesa Mkenda, umekuwa na *GB* kubwa sana na unatusikiliza kwa unyenyekevu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekaa na wewe na wadau wa nchi nzima wametoka mikoani kuja pale Morena, umetusikiliza matatizo yetu yote na mengine unaendelea kuyatatua. Lakini nikuambie ukweli sio siri wanaokuangusha ni watu wako wa chini. Ulikuja wewe ukaja na Katibu Mkuu baada ya hapo kuanzia Kamishina na ngazi nyingine za huku chini yale tuliyoongea *no implementation.* Yaani hamyatejkelezi yale sasa sijui wanaokuangusha ni akina nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile kauli ya kusema kwamba hao ni wanasiasa tu kwa kweli hii kauli nchini hapa huwa ninakwaza sana. Hata juzi imejitokeza pale Kariakoo, yaani wizarani wanamuona waziri kama ni mwanasiasa, kama vile

akisema jambo watu wa chini huku hawawezi kutekeleza. Jamani hili jambo ni baya sana kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu amekemea hata mambo ya *TRA* pale Kariakoo. Nimeshakuwa Naibu Waziri najua pale wizarani Maafisa wa kawaida wengi wanamwambia tu waziri si mwanasiasa huyo. Jamani hili jmbo tulikomeshe kwa sababu waziri ana mamlaka makubwa kwenye wizara yake. Naomba hili jambo yaani ni jambo baya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tulifanyie utafiti tuone kwamba ni kweli viongozi wengine huku chini wanadharau mamlaka ya waziri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nikupongeze na endelea kuwa na moyo huo huo. Vilevile, lazima nikushauri mambo mawili matatu ili twende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nipongeze mfumo huu wa Sera mpya na Mtaala mpya wa elimu, kama mwalimu naona umekaa vizuri. Nimepitia sana nimesoma, vipo vitu vidogo vidogo ambavyo tutaendelea kushauri na uzuri mimi na wewe ni rafiki yangu siku hizi tunaongea. Zamani ulikuwa hupokei simu zangu lakini siku hizi unapokea simu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi Profesa Mkenda hata ukimuita hivi njoo mnaongea nae, *canteen* unaongea nae ni mtu mzuri sana. Sasa lazima tukushauri ili wizara yako ikae vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, katika mtaala huu mpya wa elimu na sera msisahau mambo ya kiutawala. Mmekwenda kwenye *practical,* kwenye madarasa, sekondari, elimu ya awali na msingi lakini mmesahau kwenye utawala huku ambako ndiko mnakosimamia elimu. Huku na kwenyewe kumeoza kabisa. Mwingiliano wa TAMISEMI na Wizara ya Elimu yaani huku ndiko kumeoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa jitahidi una shule za msingi karibu 16000 nchini. Tungekuona unafanya ziara unatembelea shule za msingi uone maisha ya kule chini wanavyokuwa wamekaa wale watoto lakini uone majukumu yanavyoingiliwa na TAMISEMI. Yaani Wizara ya Elimu wewe huonekani kabisa, kule wanaonekana Maafisa wa TAMISEMI tu yaani Wizara ya Elimu imepokonywa kabisa mamlaka yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kuna utofauti mkubwa sana. Sheria Namba 25 ya Mwaka 1978 inasema "Mtaaluma Mkuu katika nchii hii ni Kamishina wa Elimu" ambae unae wewe pale ofisini kwako na una maafisa wako pale. Sasa wachukueni Maafisa wa TAMISEMI basi muwarudishe Wizara ya Elimu. Kwa sababu huu ugatuaji umetuletea shida mno na hasa kwenye utitiri wa mitihani. Yaani kule chini Mheshimiwa Waziri, kuna mitihani ya kata mara mbili kwa wiki, mitihani ya wilaya mara moja kwa mwezi, mitihani ya mkoa mara tatu kwa miezi minne. Sasa kwa mfano sisi shule binafsi kwa nini mnatuingilia? Tuacheni na mitihani yetu. Sisi mitihani yetu inaweza kuwa bora kuliko mitihani yenu mnayoifanya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI wasimamie shule zao kwa sababu TAMISEMI ina shule zao na sisi shule za *private* mnatupotezea muda kutuletea mitihani ambayo tunakuja kufanya kwenye *Mock*. Mbona kwenye *Mock* tunatii na tunachangia na kwenye *NECTA* wanatuletea mitihani lakini jamani mpaka mitihani ya kata kweli? Yaani Afisa Mtendaji wa kata anawaambia shule za *private* siku fulani kuna mtihani halafu tunabaki kutoa hela tu na hizo hela wazazi hawaoni kwa sababu tunatoa shule. Mngekuwa mnatuambia mapema tuweke kwenye *joining instruction*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachangia shule za kata shilingi 100,000 kila wiki. Jamani maisha gani haya? Mitihani ya wilaya kila mwezi yaani wanabaki tu wanafaidi kwenye *computer, photocopy* kuna posho wanapata ndio

maana wanang'ang'ania ile mitihani. Fanyeni mitihani yenu kule chini kama shule za TAMISEMI. Ndio maana nakwambia Mheshimiwa Waziri kwenye utawala hapa msiache. Tunapokwenda kufanya mabadiliko kwenye elimu naomba twendeni na jambo la kupata chombo huru cha kusimamia elimu kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku kwingine kote Mheshimiwa Waziri utaweza lakini usipofanya jambo hilo mkachukue basi hawa wadhibiti ubora wa elimu Tanzania hawa basi wabadilisheni hao kiwe ni chombo huru kiwe na mamlaka kama ilivyo *TCU* kwenye vyuo vikuu, kama ilivyo *NACTE* kwenye vyuo vya kati. Sasa shule ya awali, shule ya msingi na sekondari hawana msimamizi yaani hawana Baba na Mama kabisa. Tena sisi *private* ndo tumbaki kama yatima hivi. Yaani unafikiri jambo sijui niende Wizara ya TAMISEMI, sijui niende kwa Mheshimiwa Profesa Mkenda lakini husikilizwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalia mambo ya tozo hapa nani wa kutusikiliza? Hamna. Waziri wa Elimu, huwezi kuzitoa tozo, najua Sheria huwezi kuzitoa tozo. Waziri wa TAMISEMI, ndiye anayetoza tozo kule chini kwa sababu mlilazimishwa mkatupa leseni za biashara. Kwa hiyo, nyie mmezi-*term* hizi shule kama biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii na-*quote* kwa sababu Afisa wako wa Baraza la Mitihani siku ametoa *ranking* anasema "hapa tunafanyia watu biashara" Mungu wangu. Watoto wetu ni watanzania hawa hawa wanapokuwa wamefanya vizuri kwenye *private* ni watoto wa ndani hawa hawa, wanakwenda kuajiriwa Serikalini huko huko watapata uelewa mkubwa na *GB* kubwa kwa kufanya kazi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Waheshimiwa Wabunge, tumsaidie Mheshimiwa Waziri afanye mabadiliko haya lakini baadhi ya mabadiliko Mheshimiwa Waziri hawezi. Sheria Namba 25 ya Mwaka 1978

inaniambia kama *private* nakwenda kusajili shule yangu kwa kamishina ananipa kibali, ananipa cheti lakini sikuambiwa kama ni biashara. Bila hivyo, shule hizi zisingeanzishwa ndio maana unaoana siku hzi hata uwekezaji wa shule umedolola kabisa. Nani anatamani kujenga shule saa hizi? Tuliojenga tumejenga kama ni kula hasara tumekula hasara. Mheshimiwa Waziri, tuwe *creative,* jambo ni kubwa mno nendeni huku chini mkaone mambo yanavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niendelee kuisisitiza jambo lingine kuhusu *ranking,* Mheshimiwa Waziri, *ranking* duniani kote, uliongea vizuri sana lakini kwa sababu Mheshimiwa Waziri anapoongea huwezi kumpinga wala huwezi kusema mwongozo kwa sababu tu unatoa taarifa. Jamani Profesa ulitusomesha vizuri pale lakini uliongelea upande wako mmoja. ungetukaribisha na sisi wadau wa elimu kama zinavyofanya wizara nyingine, kwamba kabla hamjaamua mambo mnakaa na wadau wanaokuwa kwenye sekta hiyo mnakaa pamoja mnasema jamani tuondoe *ranking* au msiondoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo shuleni watoto hawasomi kabisa wanacheza madarasani. Hakuna ushindani kwenye taaluma. Tunakwenda kuleta watoto mbumbumbu baada ya miaka 10 mtakuja kuniambia. Mimi nadhani sasa shule za *private* ndio zinakuwa maabara za kuangalia mfano kwamba hawa kumbe ndio wanakwenda hivi. Kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Waitara, kwenye *private* kuna kila kitu, Tunagharamia kila kitu kiwepo ili nyie watu wa Wizara za Serikali muige kule tupate Watoto ambao ni wazuri lakini sasa hivi ninyi mnashindana na sisi. Ngoja tutoe hiki ili hawa wa–*suffocate,* ngoja tutoe hiki ili hizi shule zife. Tutakufa sawa hakuna shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali ikiamua tutakufa lakini baada ya hapo tutapata vijana ambao ni mbumbumbu kwa miaka ijayo. Mheshimiwa Waziri na wote

humu mnajua ndio maana nilishasema siku moja, asimame mtu hapa aseme mimi mtoto wangu anasoma shule za Serikali. Sio kwamba na-*challenge* shule za Serikali lakini nataka nikupe changamoto ili uweze kuboresha shule zako. Ndio maana hata Serikali mmeweka baadhi ya shule kuwa ndio shule za mfano zipo, twendeni huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana lakini lingine ni kuhusu nyaraka za Serikali, ni utitiri, mwenzangu jana Mheshimiwa Rweikiza ameongea hapa. Nimesoma hapa yaraka 110 za Serikali yaani kama vile Sheria haifanyi kazi. Yaani kila bada ya miezi sita mpaka ukute waraka shuleni. Siku moja nilikwambia pale Mheshimiwa Waziri, mbona Wizara yako haitulii? Angalia wizara nyingine zilivyotulia hatuna malalamiko ni machache machache lakini Wizara ya Elimu kila siku mnataka kukwaza watu. Yaani hauwezi kutulia, huwezi kumfundisha mtoto kuanzia darasa la kwanza mpka *form four* angalau anakwenda katika mwelekeo wa elimu hii. Katikati pale anavurugwa, mara ondokeni *boarding* kuna wakati nashangaa sana siijui nani aliyewashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo ni darasa, kuna waraka unaosema kwamba daradsa la nne ni lazima wamalizie pale plae na mmetoa na namba ya kumalizia shule pale pale halafu mmetoa nan amba ya kumalizia shule shule palepale halafu mwezi wa saba mnasema waondoke, itakuwaje sasa? Nina shule Mbeya mtu anakuja kutoka Tunduma amekuja pale *St.* Marcus shuleni kwangu halafu sasa mwezi wa saba arudi Tunduma. Kule Tunduma aliko kule Chapwa hakuna *English medium* atakwenda wapi? Atahamia wapi? Lakini ulishampa namba ya *NECTA* afanyie mtihani pale pale kwenye kile kituo. *Sometimes* mnafanya vitu ambavyo hamshirikishi Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Eeh! Muda wangu umeisha?

*(Hapa kengele ilili kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana muda wako umemalizika. Waheshimiwa Wabunge niwapongeze kwa kuwajibika ipasavyo katika kuishauri Wizara yetu ya Elimu naamini kabisa Mheshimiwa Profesa Mkenda na Naibu wake pamoja na Watendaji wao wanapokea yale yote yenye maslahi mapana kwenye sektya yetu ya elimu na watayafanyia kazi kadri ambavyo Mwenyezi Mungu atawajalia. Baada ya kusema hayo nina matangazo mawili.

Tangazo la kwanza, kuna wageni ambao wapo mchana huu ni wanachama 100 wa umoja wa Chama cha Mapinduzi tawi la Chuo kikuu cha St. John hapa jijini Dodoma. Karibuni sana wanachama hawa kutoka chuo kikuu hapa Dodoma.

Pia tuna wanafunzi 83 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo vijijini cha hapa jijini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka hicho chuo cha Mipango na Maendeleo.

Wahesmiwa Wabunge, jioni tutakuwa na wachangiaji wawili ambao ninayo majina yao hapa ambao ni Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Condester Sichalwe.

Baada ya kusema hayo ninawatakia mchana mwena nasitisha shughuli za Bunge hadi Saa Kumi na Moja Kamili Jioni.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

**17 MEI, 2023**

*(Saa 11.00 Jion Bunge Lilirudia)*

Spika *(Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe atafuatiwa na Mheshimiwa Professor Kitilla Mkumbo, Mheshimiwa Naibu Waziri, ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakuskuru kwa kunipatia nafsi. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Profesa Mkenda pamoja na timu yake, lakini pili ninaipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia kwa namna ambavyo ameendelea kuboresha miundombinu kwenye elimu yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze walimu wote nchini kwa ngazi mbalimbali, kuanzia *kindergarten*, shule za msingi, sekondari mpaka vyuo vikuu. Hatuwezi kusema wala kujivuna wasomi tulioko Tanzania hii bila kuwashukuru na kuwaheshimu walimu wetu, hata wale ambao wamestaafu kwa namna ambavyo walijitolea kuhakikisha tunaelimishwa.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru walimu ambao wako ndani ya Jimbo la Momba. Kwa nini ninawapongeza walimu waliopo ndani ya Jimbo la Momba? Jimbo la Momba tuna vijiji 72 na vitongoji 302; yako baadhi ya maeneo hatuna zahanati kwenye baadhi ya vijiji lakini walimu hawa wameendelea kufanya kazi kwa kujituma na kujitoa pamoja hata kama hakuna huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo kuna changamoto ya miundombinu ya barabara na kuna wakati mvua zikianza kunyesha njia haziwezi kupitika walimu wanaweza wakakaa zaidi ya miezi mitatu hawajaenda mjini, lakini walimu hawa wameendelea kufanya kazi kwa kujituma na kwa kujitoa.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Jimbo la Momba vijiji 50 havina maji safi na salama lakini walimu hawa wameendelea kushirikiana kunywa maji na mifugo lakini wakiendelea kufundisha watoto wetu ndani ya jimbo la momba, wakiendelea kujitoa na kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Jimbo la Momba kuna maeneo hakuna umeme lakini walimu hawa wameendelea kujituma, yamkini wanaendelea kutumia vibatari mafuta ya taa na sola; kwa namna yoyote ile lakini wameendelea kuwa wazlendo kujitoa ndani ya jimbo la momba.

Mheshimiwa Spika, ombi langu nikuombe Profesa Mkenda, tutakapomaliza Bunge la Bajeti twende tukawatembelee walimu wa Jimbo la Momba, wanashida nyingi ambazo wanatamani mwalimu mwenzao uweze kujua. Kwa walimu wote wa Jimbo la Momba na wengine wote walioko vijijini ambao wanapitia changamoto lakini wanafundisha watoto kwa kujituma ninawapongeza wakiongozwa na *DC* wa wilaya yangu ambaye pia ni mwalimu.

Mheshimiwa Spika, ombi jingine, kwa kuwa sisi watu wa Momba tunalima kufuga na kuvuna, tunaomba tupate chuo ambacho kitafanana na shughuli zetu ambazo tunazifanya ili watoto wa Jimbo la Momba watakapotaka kusoma *whether* wajifunze kulima katika ubora unaotakiwa kuvua katika ubora unaotakiwa na kufuga katika ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, ombi lingine; Mkoa wa Songwe hatuna Chuo Kikuu chochote ambacho kinatoa digrii. Tunayo kampasi ya *Dar es salaam Institute of Technology,* ina mazingira mazuri na maeneo makubwa. Tunaomba kuanzia pale muwape hadhi waanze kutoa *degree* tupate chuo kikuu ndani ya Mkoa wa Songwe tukitumia *Dar es salaam Institute of Technology.*

Mheshimiwa Spika, ombi lingine, tunayo shule ya sekondari Songwe *Girls* ambayo tunasema ni shule ya mkoa; shule hii haina tofauti na shule ya kata, na mwanzilishi wa shule hii alikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Samia Hassan Suluhu. Tunaomba tumpe heshima Mheshimiwa wetu kwa kuiwekea miundombinu bora shule ile ili watoto waendelee kupata elimu ndani ya Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, sina mashaka na ufanisi wa Wizara ya Mheshimiwa Mkenda, anafanya vizuri sana, anasimamia vizuri sana sera ambazo zimewekwa kwa utaratibu kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kushauri mambo kadhaa. Inawezekana hata sasa hivi tunavyotaka kubadirisha elimu ni kweli tuko sahihi lakini kwa nini tunaona kumekuwa na uhitaji mkubwa sana wa kubadilisha mitaala yetu?

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba teknolojia tuliyonayo ndiyo inatusukuma kutuvuta kutupeleka hapo. Serikali haina makosa yoyote kuona kwamba kuna baadhi ya

ajira zinaondoka kwa vijana kwa sababu ya kuongezeka kwa teknolojia, lakini Serikali itakuja kufanya makosa kama haitataka ku-*adopt* hizi teknolojia kuziwekea mpangilio mzuri kwenye nchi yetu ili wananchi na Watanzania wasione kwamba *artificial intelligent* imechukua ajira zao bali tuione kwamba *artificial intelligent* tuitumie kama fursa ya kuhakikisha vijana wa Kitanzania wanapata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nikawa na wazo, nikaona Wizara ya Profesa Mkenda inaitwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Mheshimiwa Nape inaitwa Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Spika, Profesa Mkenda huyu kwenye Wizara yake a-*deal* na mitihani ya darasa la nne, darasa la saba, *form two, form four* wapi, bado wanafunzi hawajagoma, bado hatujaomba tubadilishiwe elimu, bado Walimu hawajataka kuboreshewa mazingira yao; mambo kede kede kwenye Wizara hii. Ni wakati gani Profesa Mkenda atakuwa anahangaika na timu yake kujua kuna *emerging technologies* ambazo ziko duniani zinaweza zikawasaidia watanzania kujiajiri?

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia Wizara ya Mheshimiwa Nape, Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari a-*deal* na wandishi wa Habari mikonge ya Habari, kule Momba kuna watu hawapati mawasiliano yote haya ni ya kwake saa ngapi tena atakumbuka na teknolojia ya Habari? teknolojia zinakuja kila wakati. Ushauri wangu kwa Serikali nilikuwa naomba yafuatayo;

Mheshimiwa Spika, kama itawapendeza, kama mtaona inafaa tupate Wizara mpya ya Teknolojia peke yake. Kipengele cha Mheshimiwa Profesa Mkenda kibaki Wizara ya Elimu na Sayansi, Teknolojia iondoke, kwenye Wizara ya Mheshimiwa Nape ibaki Wizara ya Habari na Mawasiliano, Teknolojia iondoke tupate Wizara ya Teknolojia. Ndani ya hiyo

Wizara ya Teknolojia kuwe kuna taasisi zake. Kuwepo na taasisi ambayo itasimamia *old technology* kwa sababu bado ziko taasisi hapa nchini kwetu tunatumia teknolojia za kizamani. Pia iwepo taasisi ambayo itasimamia *current technology* ambayo tunatumia sasa hivi muda huu lakini kuwepo na taasisi ambayo itasimamia *emerging technology* na *future technology* ili Wizara hii ndio iweze kusambaza ujuzi mbalimbali kwenye Wizara ya Elimu, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Uvuvi na vitu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najiuliza, mfano leo mimi nimwalike *Elon Musk* aje hapa Tanzania nitampeleka kwenye Wizara ipi akapeleke ujuzi wake kwa ajili ya kujadiliana na Serikali yangu? Tunashindwa kujua, atakwenda kwa Mheshimiwa Mkenda kwa sababu ana teknolojia au ataenda kwa Mheshimiwa Nape kwa sababu ana teknolojia ya Habari?

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ichukulie teknolojia kama ni jambo la muhimu. Matajiri wote ambao tunawaongelea sasa hivi, mfano sasa hivi tunapomuongelea huyo Elon Musk ambaye anayo kampuni ya *Spacex* ambayo imefanya mambo makubwa kwa ajili ya kwenda huko angani, ni mwanateknolojia, ni mtu ambaye alizaliwa tu hapo Pretoria, *South Africa,* sasa hivi anaonekana ni mtu mashuhuri sana duniani. Aliununua mtandano wa *twitter* kwa zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 44 kwa ajili ya teknolojia tu. Tukimwangalia mtu kama Mark Zuckerberg, wote hao waliwekeza kwenye teknolojia, tukimwangalia mtu kama Bill Gates, wote hawa ni matajiri ambao walitokana na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, tunabadilisha mtaala hii, ni kweli, lakini ninaona baada ya miaka kumi bado tutarudi hapa kuona kwamba bado mitaala yetu tuliyobadilisha haifanani. Ninasema hivyo kwa sababu gani, hatuwezi kushindana na

teknolojia, tutakuwa tunajidanganya kushindana na teknolojia ni kama kushindana na muda.

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu naongea katika hali ya Kibunge, lakini nilitamani ningewaonyesha pia watu kwamba teknolojia hii namna ambavyo inashabihiana zaidi hata na mambo ya kiroho. Wanaosoma vizuri Biblia wataelewa vizuri sana vita ya Urusi na Ukraine nini kinaendelea. Sasa hivi benki zinavyofungwa ni mambo ambayo kwenye Biblia yameandikwa. Sasa sisi kwa nini tusiendane na huo wakati?

Mheshimiwa Spika, vijana wa Kitanzania wanaona hakuna ajira kabisa lakini kama tukiamua kutumia *artificial intelligent in a positive way* tunaweza tukapata ajira nyingi zadi ya ajira ambazo zilikuwa zimeandikwa kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Tunaweza tukapitiliza.

Mheshimiwa Spika, vijana wa Kitanzania wamekosa *platform,* wamekosa sera namna ya kuja kuonesha ujuzi wao. Wako vijana huko nje ni mahiri, ni wataalamu, wapeni nafasi, wapeni *room,* wajue wakija wata-*fit* kwenye taasisi ipi, wata-*fit* kwenye taasisi ya teknolojia ya zamani teknolojia ya sasa au teknolojia inayokuja? Vijana wa Kitanzania muwape nafasi waweze kutengeneza hata *stimulation* za teknolojia ambazo tunazitarajia. Zipo teknolojia za *blockchain* hatujazikumbatia, zinatoa ajira nyingi sana huko duniani. Sasa hivi kuna wakati unaweza ukaona benki zinabisha, hawataki kupokea *digital currency*. Mimi nataka uwaambia hivi wanajidanganya, watashindana na ukuta. Huko tunakoenda na majira yaliyopo na benki ambazo zinafungwa huko duniani, na kwa namna hali ilivyo tupende tusipende tunakuja na *currency* moja duniani; na tumeshaanza kuona wachumi wa dunia ambavyo Dola ya Marekani imeshaanza kuteteleka. Kwa hiyo niiombe Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja, malizia Mheshimiwa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, hatua ya kumalizia ni kumuomba Profesa Mkenda atakapokuwa pia anahitimisha kwenye hitimisho lake aseme kidogo ni namna gani ambavyo ametumia *artificial intelligent* kutengeneza ajira nyingi ambazo ziko kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ukiacha hizi ajira ambazo vijana wa kitanzania tunagawana…

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Mheshimiwa Juma Kipanga, ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii. Kwanza kabisa mimi nadhani nimpongeze Profesa anawizara ngumu ameuikuta pagumu anajitahidi enedelea kujitahidi, anajitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kawaidia mimi natoa ushauri cha kwanza Profesa, hebu ile *VETA* ya Musoma Vijijini, na nilikueleza ukinipatia mimi *VETA* itakuwa ni ya mfano nchini; kwa sababu sitaki *VETA* ya mambo ya hoteli ya kutengeneza magari, hapana, mimi *VETA* yangu itakuwa mambo ya kilimo uvuvi na ufugaji. Naomba hiyo *homework* Profesa imalizie.

Mheshimiwa Spika, sasa Waheshimiwa Wabunge mimi natoa ushauri ifuatavyo. Elimu yetu, nilikuwa sipo, nimesikiliza, na ukweli ni kwamba iko kwenye hali mbaya, lazima kwanza tukiri hivyo. Lakini hakuna wa kulaumu, ni sisi wote. Tukitaka kumlaumu mtu ni kama hatujui tunalolifanya.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa muda umefika wa kujiuliza na pendekezo langu ni kwamba elimu ya awali

kuipeleka TAMISEMI, imekaa TAMISEMI kwa muda matokeo yake siyo mazuri. Kama inawezekana, maana huko nyuma tulivyopeleka madaraka ya ndani si ndiyo tulifanya mabadiliko? Sasa tukifanya *evaluation* mabadiliko hajazaa matunda. Kwa hiyo mimi napendekeza, kwa sababu tumerudi nyuma Wizara ya Elimu irudishwe tena. Yaani mambo ya elimu yawe ndani ya wizara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inakuwa ngumu sana eti shule za msingi *primary* zinakuwa na Waziri wake na Ofisi zake ikifika *university* nayo na ya kwake halafu baadaye mnamlaumu huyu wa juu, mnamuonea, mnamuonea. Kwa hiyo mimi napendekeza Profesa lipeleke kwenye *cabinet,* mwambie *PM* alifikirie, uwe na wizara inaitwa Wizara ya Elimu, Sayansi Utafiti na Ubunifu *Ministry of Education, Science, Research and Innovation*. Huna haja ya kutaja teknolokjia, teknolojia kwa sababu *innovation* maana yake una *innovate* kwenye *technology*, kwa hiyo huna haja ya kuitaja. Hilo ni pendekezo langu la kwanza, tukifanya hivyo tutona mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni miundombinu kwenye mashule yetu. Profesa wewe na TAMISEMI, yaani wizara mbili lazima mkae chini mkubaliane kwamba, ili tuwe na elimu iliyo nzuri na inaweka msingi mzuri lazima kila shule; vyumba vya madarasa sawa lakini ni wanafunzi wangapi? Kwa hiyo, *homework* yako ya kwanza na wahusika turudi nyuma tuone kama tutarekebisha. Huko nyuma enzi yangu Waheshimiwa Wabunge shule ya msingi tulikuwa 45, sekondari tulikuwa 35, *high school* tulikuwa 25. Sasa hebu turudi huko kwanza. Hii mitaala hata ukiwa nayo mizuri namna gani ikiwa wanafunzi wamerundikana madarasani hautafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shule yoyote inayoitwa shule duniani kote; na mimi nimezunguka kwelikweli duniani hapa; sijawahi kwenda shule nikakuta shule haina maabara haina maktaba, hiyo ni shule gani? Mimi sasa hivi Musoma vijini shule za msingi tatu nimeweza kujenga maktaba. Na watu

wananishangaa, wanasema Profesa mbona unang'ang'ana shule ya msingi iwe na maktaba? Nikasema kama unaona watu hawaelewi ushibishane nao sana, inabidi ukae kimya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba wanaoshughulika na elimu wahakikishe kwamba kila shule ina maktaba. Maktaba kwa nini, kwa sasa hawatahitaji vitabu? lakini maktaba zile tunakoenda tutaweka kompyuta zenye *capacity* kubwa na spidi kubwa; hata vitabu vingine mnavyovinunua sasa hivi vinatolewa bure, sasa kama hauna hizo kompyuta ndiyo maana ya hizi *library* lazima ziwe na *computer*, hata kama vitabu ni vichache mno, kusudu waweze kupata vitabu vya bure ambavyo sasa hivi vinagawanywa duniani.

Mheshimiwa Spika, lazima shule iwe na maabara, sekondari zetu zote lazima ziwe na maabara, hilo ni tatizo. Kwa hiyo ninaomba hayo yarekebishwe hayo. Kingine ninachokuja sasa nije kwenye mambo ya juu, Profesa haya yanakuhusu wewe na wengine wengine, nije Elimu ya Juu kidogo, na nilishapendekeza hapa.

Mheshimiwa Spika, hiyo *COSTECH* tuliyonayo hata tukimwaga humo fedha muundo wake *COSTECH* imekuwa kama idara ya Wizara. *COSTECH* haipaswi kuwa hivyo, inapaswa kwanza jina la *COSTECH* libadilishwe, iitwe *National Research and Innovation Foundation*. Iweke mkazo kwenye utafiti na mambo ya ubunifu, halafu na yenyewe ianzishe kufanya *rating* ya wasomi. Unajua haiwezekani, Maprofesa hawalingani jamani, au ma-Dkt. wote hawalingani. Sasa kwa kuwa hatuna *rating* hakuna Profesa wa *grade* "A" Profesa wa *grade D,* hakuna Dkt. wa *grade A, grade D*, kila mtu anaruka tu na *title*. Mimi Profesa, mimi Dkt., sasa inabidi wengine wale halali wakae kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hii kazi hii ni lazima tuiachie *National Research and Innovation Foundation* na duniani

kote *foundations* ndio zimefanya vizuri. Uende Marekani, uende *South* Africa, uende wapi na wanapata fedha wanakuwa na watu wengi, hapo mambo yetu yataenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye vyuo vikuu, hapa ndio naomba Profesa aache *legacy* kwamba hiyo Wizara ilikaliwa na Profesa. Ni lazima ainge kwenye kila chuo, tatizo letu moja sasa hivi ndio maana ukichukua vyuo vya Tanzania, vyuo vya Tanzania vyote hakuna ambacho kiko kwenye kumi bora ndani ya Afrika, hatumo. Inamaanisha kwamba utafiti kwenye vyuo vyetu umeenda chini.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri ni kwamba mimi bado napokea ripoti ya machapisho. Kila niki–*check* Tanzania naona hamna, tuko chini, hivyo, Mheshimiwa Profesa akae na *Vice Chancellors* wake, watu wameanzisha *journals*, majarida kwa sababu ya *promotion* na yatazidi kudidimiza elimu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku moja Mwalimu alitutembelea, nashukuru mimi nilisoma *Dar es Salaam University*, *Chancellor* alikuwa Nyerere, akaja pale alikuwa amezowea kuonana na wafanyakazi na mimi ndio nilikuwa naanza kazi. Akasimama mtu mmoja *senior* akasema Mwalimu hiki chuo kina upendeleo sana, mimi sijapandishwa cheo. Mimi sikujua Mwalimu anamfahamu vizuri kumbe alimpa *scholarship* kwenda kusoma Marekani. Kaongea kaongea Mwalimu akatujibu wote akasema, jamani mimi nilikuwa nadhani mtu anayekuwa profesa, ni kweli mnahakikisha kweli kweli kwamba uprofesa unamstahili, kama ni suala la mshahara si wapandishieni tu mishahara, lakini msiwape hizi *titles* kwa urahisi rahisi hivi.

Mheshimiwa Spika, sasa vyuo vyetu vimefikia hatua hata idara zimekuwa na *journals*, hizo ni *just for promotion*. Sasa Mheshimiwa Profesa nimsaidie najua anayafahamu,

atakavyokaa na *Vice Chancellors* wake atamwambia kila *Vice Chancellor* aje na *journal* za chuo chake. Wakikaa kwenye meza na wote wakae sehemu ambapo kuna *internet* au na nini, anamwambia anaanza ku–*check journal* yake moja baada ya nyingine. Ambazo hazifai, nyingi hazitafaa kwa sababu mimi nimeshazifanyia utafiti.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *citation index (CI),* wanaonisikiliza andikeni *CI*, *Citation Index* au kingine kinaitwa *IP (Impact Factor)*. *Citation Index* maana yake ni kwamba hilo *journal,* hilo jarida unalolitumia ni wangapi wanafanya rejea zao, wanaofanya utafiti. Profesa Mkenda akikuta zina– *impact factor* ya *0.05* nitamwomba tuje tuongee, nadhani hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia *0.05, Impact factor* au *Citation Index,* inamaanisha hizi *journal* wanazozitumia duniani hazijulikani, kwa hiyo ni zetu tu hapo, *backyard journals,* lazima azipige vita Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuna maeneo matatu ambayo lazima tuwekee mkazo na lazima vitu viunganike humu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Profesa muda wako umekwisha.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, namalizia hako ka mwisho.

**SPIKA:** Nakuongezea dakika tatu umalizie.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tena unaona maprofesa waungwana, ahsante profesa. Ni hivi, jamani tulieni mtafanya anisimamishe, *stop*. Ni

kwamba Profesa Mkenda kuna maeneo matatu lazima ayaanzishe akiwa kwenye hiyo Wizara, ni *space science and technologies* na hiyo ndio yanaingia mambo ya *satellites* na mambo ya nini. Lazima aanzishe *research* kubwa na elimu kubwa kwenye eneo la mbegu, *seed science,* lazima si tunataka kwenda kwenye kilimo? Hata hii *space science* ni kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kuna ambalo ni kubwa, *non-sciences, non-technologies* hata wale wagonjwa wa *TB* duniani wameacha kutumia vidonge vingi siku hizi wanachukua kidonge *size* kama ya unywele inatibu *TB,* huko ndio dunia inakokwenda.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, Naibu Waziri na Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuniahidi kunipatia Chuo cha *VETA* kwenye Jimbo la Ubungo kwa sababu huwezi kuwa na kiwanda cha pili kwa ukubwa cha kutengeneza nguo, kinaajiri zaidi ya watu 4,000, unayo pale *EPZA* kubwa kuliko zote Tanzania ipo pale na Naibu Waziri anayeshughulikia kazi anafahamu alishafika pale. Kwa hiyo kuna vijana wengi, hivyo, nashukuru sana kwa kuniahidi kwamba tutashirikiana tupate Chuo cha *VETA* kwenye Jimbo la Ubungo hususan Kata ya Makuburi ambapo ina *high concentration* ya viwanda hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka niongeze sauti yangu ni kwenye suala ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelichangia kwa hisia kubwa, suala la lugha ya kufundishia. Kwanza nianze kwa kuungana mkono kabisa na

jinsi ambavyo sera imependekeza, nadhani iko sahihi kabisa kwamba lugha zetu mbili zitatumika kufundishia Kiswahili kwenye ngazi ya chini na Kiingereza kwenye ngazi inayofuata.

Mheshimiwa Spika, suala la mjadala hili huwa lina sehemu mbili tu. Unaweza ukajadili kwa kuzingatia uzalendo wa lugha na utamaduni, hiyo ni sawa pia, hawa wanaita *cultural romanticism,* lakini unaweza kujadili pia kwa kuangalia taaluma. Nadhani sisi hapa kwa maana ya sera tunaangalia taaluma na kuangalia tunazingatia kupanua wigo kwa vijana wetu lakini pia hali halisi. Hali halisi ni nini? Moja ni makosa, kudhani kwamba Kiingereza ni lugha ya wakoloni, ilishaisha siku nyingi.

Mheshimiwa Spika, Waingereza wapo milioni 67 tu tunavyozungumza, lakini duniani hapa kuna watu bilioni moja wanaotumia Kiingereza kama lugha ya kwanza. Kwa hiyo Kiingereza kuwa lugha ya wakoloni iliisha siku nyingi ndio maana kuna Kiingereza cha *West* Afrika, Kiingereza cha *South* Africa, Kiingereza cha Kenya, Kiingereza cha Scandinavian kuonyesha kwamba Kiingereza kwenye lugha ya ukoloni kilishaondoka lakini sikiliza takwimu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, asilimia 53 ya tovuti kwa maana ya *website* zote duniani zinatumia lugha ya Kiingereza. Lugha ambazo zinafuata ni chini ya asilimia 10. Kwa mfano, Kichina hiki ambacho watu wanakizungumza sana hapa asilimia mbili tu, Kifaransa asilimia nne, Kirusi asilimia sita, Kijerumani asilimia sita, Kihispaniola asilimia tano, Kireno asilimia tatu. Asilimia 53 iko kwa lugha ya Kiingereza, hiyo nakwambia kwamba lugha ya Kiingereza imeendelea kuwa lugha ya taaluma na biashara duniani. Ndio maana Lufthansa ambalo ni shirika kubwa la ndege lipo Ujerumani na Ujerumani ni Taifa ambalo ni *very conservative* kwenye lugha, lakini waliamua kubadilisha *policy* yao mwaka 2010 kufanya kwamba lugha

ya Lufthansa ni Kiingereza kwa sababu ndio lugha ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hilo tuondoke kwenye uzalendo wa lugha, hii sio lugha tena ya wakoloni. La pili, katika nchi kumi zenye mfumo bora wa elimu Afrika, nazizungumzia Seychelles, Mauritius, Afrika ya Kusini, Botswana, Kenya, Cape Verde na Namibia. Nchi saba zinatumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia na tatu zinatumia Kiarabu hizi ni Algeria, Tunisia na Misri. Pengine niwape mfano wa karibu hapa Afrika nchi ambazo zinasemekana kama ni bora kwa elimu ni Seychelles na Mauritius na zinafanana na sisi, kwa sababu wale wana lugha Yao, Seychelles na Mauritius lugha yao ni Krioli ndio lugha ya Taifa, lakini lugha yao ya kufundishia ni Kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukiingia mtaani, mtaani hutosikia Kiingereza ni Krioli lakini kwa Seychelles wanaanza na Krioli mpaka *primary* kama sisi, wakifika sekondari *all the way* ni Kiingereza. Mauritius wenyewe tangu awali wanaanza na Kiingereza *all the way* lakini ndio nchi ambazo tunazungumza zipo bora katika suala la elimu. Nchi 47 duniani zinatumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia, kwa hiyo usije ukadhani ni hapa tu na nchi 143 duniani Kiingereza ni somo la lazima.

Mheshimiwa Spika, tazama kwa hapa Tanzania, nikupe takwimu hii na unisikilize kwa makini sana hii. Ukichambua takwimu za matokeo ya darasa la saba ambayo tunatumia Kiswahili miaka mitatu iliyopita, ukiangalia shule pale, kwa mfano Dar es Salaam, ukichukua shule 50 za juu ambazo zimefanya vizuri, shule ya kwanza mpaka ya 50 zote zinatumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia ikiwemo shule ya Msingi Olympio ya Serikali ambayo ni moja ya shule za Serikali ambazo zinatumia Kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo maana yake nini? Hatuwezi kulaumu Kiingereza kama ndio chanzo ya wanafunzi kufeli, sio kweli, kwa sababu shule za msingi zinatumia Kiswahili, lakini tafuta shule 50 bora utakuta ni zile ambazo wanatumia Kiingereza.

**MBUNGE FULANI:** Aliongea bila kutumia kipaza sauti.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Hilo sitaki kusema.

Mheshimiwa Spika, tunapoandaa mitaala tunaangalia *factors* nyingi. Moja ya msingi ambayo lazima uzingatie mtaala wowote lazima uzingatie matakwa ya wazazi, wazazi wanataka nini na tuna takwimu mbili hapa. Kabla shule za binafsi hazijapamba moto Tanzania, Watanzania *middle class* wengi wakiwepo Wabunge hapa walikuwa wanawapeleka watoto wao Uganda na Kenya, walikua hawafuati elimu, walikua wanafuata Kiingereza. Baada ya shule kuanzishwa hapa wamerudi.

Mheshimiwa Spika, takwimu ya pili tulishafanya utafiti kati ya mwaka 2015 mpaka 2017, tuliwauliza wazazi, mngetaka watoto wako wafundishwe kwa lugha gani, asilimia 63 yaani wazazi sita mpaka saba kati ya kumi walisema walitaka watoto wao wafundishe kwa Kiingereza kuanzia awali mpaka chuo kikuu na utafiti wa mwaka jana, wa karibuni unaonyesha kwamba ni asilimia 70. Kwa hivyo ukiwa Waziri wa Elimu unapotengeneza mtaala huwezi kutengeneza mtaala ambao upo mbali na matakwa ya wazazi, wazazi ni sehemu muhimu sana kwenye suala hili.

Mheshimiwa Spika, hapa nazungumza nini? Ninachosema hapa hakuna shaka kwamba lugha ni nyezo muhimu sana kwenye suala la elimu na ni muhimu watoto na Walimu watumie lugha ambayo wanaijua, lakini lugha huzaliwi nayo, lugha unaipata kwenye mazingira hili ni jambo la msingi ambalo tunatakiwa tulizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo na hatusemi hakuna tatizo la lugha Tanzania, la Kiswahili na Kiingereza, lipo, ni kubwa, lakini jambo la msingi hutatui tatizo kwa kulikimbia, unalitatua kwa kulikabili. Hapa nataka nipendekeze kwamba, maadam sera imeshaelekeza hivyo, hatua mbili lazima zichukuliwe. Hatua ya kwanza lazima tukubali kwamba tuna changamoto kubwa sana ya Walimu kwenye somo la Kiingereza, kwa maana ya idadi na hata ubora wao. Sasa nchi zingine walifanyaje na mimi nilipitia pitia, walipoamua kwenda mfumo ambao tunataka kwenda nao, walikiri tatizo, lakini jambo la pili waliamua kufungulia milango.

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri kwamba Serikali itumie nafasi ya uwepo wa *protocol* ya hii ambayo tunazungumzia ya *free movement of labor* tumeshafungua *East Africa*. Sisi tunauza Kiswahili, sisi ndio wababe wa Kiswahili katika Bara la Afrika lakini wapo wenzetu ambao wametutangulia kwenye Kiingereza, tufungulie mipaka, miaka mitano mpaka 10 waje Walimu hapa kutoka ndani ya Nchi za Afrika, waje Walimu hapa wa Kiingereza wale tunawapelekea Kiswahili tunakarabisha Walimu wa Kiingereza. Ndani ya miaka mitano mpaka kumi tatizo hili litakuwa limekwisha.

Mheshimiwa Spika, nadhani hili ni jambo la msingi, kwa hiyo tuombe Wizara ya Elimu, lakini pia Ofisi ya Waziri Mkuu pale kwenye Ofisi ya Kamishna wa *Labor* kwa sababu wako *very rigid,* pale kupata vibali vya kazi ni kazi ngumu sana. Kwenye suala la elimu lazima walipitie upya, tu-*relax* ili tupate Walimu wengi wa somo la Kiingereza kutoka Nchi zingine. Itakuwa ni hatari sana Mheshimiwa Waziri tukabadilisha sera, tukabaki na sera ambayo tunayo ya kutumia Kiingereza halafu tusiwe na wafundishaji wazuri wa Kiingereza, itakuwa ni hatari kwa nchi, tutakuwa tumetwanga maji kwenye kinu. Kwa hiyo suala moja muhimu tuwekeze sana kwenye suala hili la Walimu wa somo hili la Kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka kusisitiza kwamba hakuna shaka, tunakipenda Kiswahili chetu. Tunachosema ni kwamba watoto wa Kitanzania hapa walipofika lazima wawe Kiingereza kizuri, Kiswahili kizuri na itafika mahali hata kitabu kitakuwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lugha ya Kiingereza. Akisoma *Archimedes Principle* haielewi anafungua Kiswahili. Hata mtihani ukija hakuna tatizo lolote, anapewa mtihani upo kwa Kiingereza upo kwa Kiswahili. Akiona anaweza akajibu kwa Kiswahili vizuri anafanya kwa Kiswahili wala hatuna sababu, muhimu ni kwamba maarifa yapatikane kwa lugha mbili hizi, Kiswahili na Kiingereza na lugha isiwe kikwazo kwenye kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo walirejea kwenye ripoti yetu kwenye suala hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, naungana na Watanzania wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja za ustawi wa kijamii, kiplomasia, amani na utulivu na kutuepusha na majanga mbalimbali katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana viongozi wenzangu wote, wananchi wote wa Jimbo la Mbulu Mjini na wote wenye mapenzi, kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima kwa jinsi tulivyotekeleza Ilani ya CCM yam waka 2020-2025, kwa kweli kwa miaka miwili sasa yapo mambo mengi sana yaliyoshindikana huko nyuma na sasa tayari yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri na Naibu Waziri, Kamati yetu, Katibu Mkuu na watendaji wetu wote katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuishukururu sana Mamlaka ya Elimu Tanzania *(TEA)* kwa kutupatia fedha za ujenzi wa mabweni mawili mwaka 2017 na 2018 katika Jimbo la Mbulu Mjini hivyo basi tunawaomba watusaidie ujenzi wa mabweni mawili katika Shule yetu ya Sekondari ya Kata ya Daudi (Marangw) kwa kuwa ni shule kongwe iliyoko maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana ya elimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itazame upya muundo wa ngazi za Wadhibiti Ubora wa Elimu kwani kwa sasa shule za sekondari nchini zimekuwa nyingi sana, hivyo basi kuwe na Wadhibiti Ubora wa Elimu ya Sekondari wawepo kwa ngazi ya kanda, mkoa na halmashauri kote nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie vigezo vya usajili wa vituo vya malezi ya watoto wadogo na elimu ya awali nchini hususan walimu wanaoajiriwa wengi wao hawana taaluma ya kutosha kwa ustawi wa Taifa unaanzia malezi na makuzi ya mtoto hivyo eneo hili ni muhimu liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie utaratibu wa kila halmashauri nchini kuwa na shule moja yenye kitengo cha elimu maalum kwani kuna kundi kubwa la watoto wenye mahitaji maalum ambao mazingira yao hayana huduma hiyo muhimu sana, kwa mfano Shule ya Msingi Endagikort katika Halmashauri ya Mbulu Mji ina wanafunzi zaidi ya 30 kwa miaka sita sasa hali inayofanya wanafunzi hao kusoma kwenye mazingira magumu sana, hakuna miundombinu ya

madarasa, mabweni, vifaa vya kufundishia na walimu wa elimu maalum, ajira kutoka Serikalini.

Kwa hiyo, ninaomba Waziri wa Elimu afanye ziara mahususi katika Jimbo la Mbulu Mjini, kutembelea Shule ya Msingi Endagikort, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tango *FDC* na Chuo cha Ukunga na Uuguzi Mbulu kwani maeneo hayo yana changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie utaratibu mzuri wa matumizi ya vituo vya walimu *(TRC)* kwenye tarafa zetu nchini kwa kujikita kwenye misingi yake ya kuanzishwa kwani kwa sasa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu na hayafanyiki na baadhi ya vituo havitumiki, hata hivyo uamuzi wa walimu waratibu kupangiwa vipindi vya kufundisha kwenye shule zilizoko karibu utasaidia sana kuongeza vipindi vya masomo kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi kumi ya mwaka wa 2022/2023, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya elimu hasa kuboresha ufaulu na hata miundombinu ya madarasa na mabweni. Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imeendelea kupitia kipindi kigumu cha changamoto za kuporomoka kutoka kuongoza kimkoa katika ufaulu wa elimu ya sekondari. Pia ufaulu kwa shule za msingi unapitia katika changamoto kubwa hasa kutokana na mazingira ya shule za vijijini ikiwemo upungufu wa walimu. Pamoja kuwa ni jukumu jumuishi kwa wazazi, bado kunahitaji uharaka wa kupitia sera ya elimu kuweza kuboresha taaluma kwa shule za vijijini ambazo kwa kiasi kikubwa hazifanyi vizuri ukilinganisha na shule za mijini.

Mheshimiwa Spika, walimu bado wanaendelea kufanya kazi katika mazingira magumu kwa kukosa majengo ya nyumba za kuishi. Napendekeza Serikali kuendelea kushirikiana na wananchi katika ujenzi wa nyumba za walimu iende sambamba na ujenzi wa maboma na pia madawati kwa wanafunzi wote. Ni muhimu kuhakikisha motisha kwa walimu ili kuboresha taaluma iwe ya kiushindani kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, *SADC* na hata Afrika. Napendekeza pia Serikali itoe kipaumbele kwa kulipa madai ya malimbikizo kwa walimu, ili kupunguza muda wa kufuatilia malipo yao na badala yake waelekeze muda zaidi kwenye kufundisha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tunapopambana na magonjwa yasiyo ya kuambukizwa yakiwemo magojwa ya kansa, shinikizo la damu, figo, moyo na kadhalika, narudia tena kuishauri Serikali kuweka kipaumbele cha kuboresha elimu ya afya, ikiwemo upanuzi wa ujenzi wa ndaki ya sayansi ya afya ya Chuo Kikuu cha *Dar es Salaam - Mbeya College of Health and Allied Sciences (UDSM-MCHAS)*. Serikali itoe kipaumble cha kutenga eneo la kutosha kwa chuo hiki

kutoka kwa eneo la iliokuwa *Tanganyika Packers Ltd.,* Mbalizi Mbeya.

Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha uwekezaji na uendelezwaji wa viwanda endelevu, Tanzania inahitaji kuzalisha wataalam wengi na hasa ujasiriamali na taalum ya ufundi ngazi za kati na chini ambapo mahitaji ni makubwa. Pamoja na kujiwekea malengo ya kuongeza viwanda, nashauri Serikali ilitazame upya suala la uwepo wa nguvu kazi (vijana kupata mafunzo ya ufundi na ujasiriamali) ya kutosha na itakayowezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko mbalimbali hasa ya kisayansi na kiteknolojia na hata kiuchumi, yanayoendelea duniani, napongeza hatua ya Serikali kwa kuchukua hatua za kuboresha mitaala ya elimu kuwa ya kisasa zaidi ili kuendana na mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka kadhaa iliyopita Tanzania imeshuhudia mafundi mchundo wengi wakiongeza *(upgrade)* ngazi za utaalamu wao kwa kusomea kozi za uhandisi wakati idadi ya mafundi mchundo wanaofuzu masomo ya ufundi mchundo ikipungua huku mafundi wa kawaida *(artisans)* wanaoongeza utaalamu wao ikiwa haiongezeki. Hali hii imepelekea kupungua kwa kasi idadi ya mafundi mchundo pamoja na mafundi wa kawaida na hivyo kuathiri utendaji wa viwanda (na sekta nyingine) kwa kuwa hawa ndio wanaotenda kazi kwa mikono. Ukizingatia kuongezeka kwa uwekezaji katika viwanda, hali hii inabidi irekebishwe haraka kwa kuongeza idadi ya mafundi husika ili kukidhi mahitaji ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa uwiano wahandisi/mafundi mchundo/mafundi wa kawaida ni wa chini sana na hautaweza kuisiadia Tanzania kufikia malengo tarajiwa. Hata ukilinganisha wataalamu wa juu wa stadi mbalimbali za Taifa na wenye stadi za kati na za chini uwiano

wake sio mzuri ukilenga uwezo wa kusimamia viwanda vya kisasa kiasi cha kuhitaji marekebisho ya uwiano kama mpango wa Taifa wa kuendeleza stadi unavyotegemea *(National Skills Development Strategy)*.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iongeze msukumo kwenye mafunzo ya mafundi mchundo na mafundi wa kawaida na pia elimu yetu ilenge mafunzo ya ujasiriamali. Hii pia ishirikishe elimu ya kujitegemea toka elimu ya awali na hata kutumia watalaam wetu wa kilimo, mifugo na uvuvi kuanzisha mashamba darasa mashuleni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda na Naibu wake Mheshimiwa Omari Kipanga na wataalamu wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye kutekeleza Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia kuhusu nafasi ya vyuo vikuu vya Tanzania kimataifa, na uhitaji wa kuboresha *website* za vyuo vyetu ili vionekane kimataifa na kukamata nafasi za juu Barani Afrika na duniani.

Mheshimiwa Spika, Tanzania yetu ni nchi inayokua kwa kasi hapa Afrika Mashariki na kwa kuwa nchi yetu ina muundo bora wa elimu, ni vyema ubora huo ukaonekana katika vyuo vyetu vikuu.

Mheshimiwa Spika, kwenye mpangilio wa vyuo vikuu 200 bora Barani Afrika, kwa kutumia mtandao wa *uniRank* kwa mwaka huu wa 2023, Chuo Kikuu cha Nairobi ni cha sita kwa ubora, na cha Makerere ni cha 16 kwa ubora na *Kenyatta University* ni cha 24.

Mheshimiwa Spika, Chuo chetu Kikuu cha Dar es Salaam kimeshika namba ya 34, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine ni cha 67, Chuo Kikuu cha Afya cha Muhimbili ni cha 94, *State University of Zanzibar* ni ya 163 na *University of Dodoma* ni ya 184.

Mheshimiwa Spika, katika vyuo vikuu bora 200, Kenya na Uganda wametuzidi kwa mbali kwenye Ubora.

Mheshimiwa Spika, vyuo vya Afrika Kusini vimeshika nafasi za juu na nyingi Barani Afrika kwa sababu nchi yao imewekeza kikamilifu kwenye elimu ya vyuo vikuu, na vimefanikiwa kwa sababu vina mahusiano mazuri na vyuo vikuu bora duniani ambapo wamekuwa wanajifunza kutoka kwa wenzao kwa kushirikiana katika shughuli za utafiti na programu za kubadilishana uzoefu.

Mheshimiwa Spika, *uniRank* inatumia vigezo vya kimtandao kuorodhesha vyuo bora Afrika na duniani kwa ujumla. Ubora huo hutegemea machapisho ya kisayansi yaliyofanywa na chou; shughuli za kiutafiti za chou; uwepo wa cheti cha usajili wa chuo na kutambuliwa na Mamlaka za nchi *(TCU)*; chuo kutoa mafunzo ya shahada ya kwanza au za juu *(Masters na Ph.D)*; na chuo kutoa elimu kwa njia ya kawaida ya kuingia darasani na kukutana ana kwa ana na waadhiri.

Mheshimiwa Spika, kufanya vibaya kwa vyuo vikuu vya Tanzania kumesababishwa na viongozi wa vyuo vyetu kukosa ubunifu wa kuonyesha mambo mazuri yanayofanyika vyuoni kwenye mitandao. Pia changamoto ingine kubwa ni kwamba wasomi na watafiti wa Kitanzania katika vyuo vyetu wamekuwa wavivu kuchangia machapisho yao katikaa jukwaa la wasomi duniani. Vilevile *website* nyingi za vyuo vyetu zinakosa taarifa muhimu za chuo na matokeo ya utafiti hubakia kwenye kuta za chuo.

Mheshimiwa Spika, ubaya wa kushika nafasi za chini kwa vyuo vyetu vikuu inaondoa heshima ya chuo na wafanyakazi katika macho ya wadau, kama vile wanafunzi na wafadhili; umaarufu kidogo wa wafanyakazi wa chuo kwenye wasomi wa vyuo vingine vya ndani na nje; kuathiri ushirikiano na vyuo vingine vikubwa duniani kwenye kufundisha na utafiti. Hawatashirikiana na vilaza; na kukosekana nafasi kwa wasomi wetu katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, ushauri kwa Wizara na vyuo ni kama ifuatavyo; iwe ni lazima kwa wahadhiri wote wa chuo kujisajili na *google scholar (point* huchakatwa kutoka huko); walimu na wanafunzi wote wahimizwe kuandika tafiti zao katika majarida ya kimataifa. Tafiti mpya tu ndio hutumika kutoa alama; iwepo sera ya kuweka machapisho yote kwenye *repository* ya maktaba kuu ya chuo, ni iweze kuonekana kwenye mtandao; walimu wote wahimizwe kuweka machapisho yao kwenye sehemu ya wazi *(open source research repository);* benki ya machapisho ya chuo kikuu iwe na mfumo wa kuonesha kwenye mtandao vitabu vya *degree* za *Masters* na *Ph.D;* kuwe na mfumo wa *online* kuonesha *abstracts* zote za kazi za wanafunzi za *Masters* na *Ph.D;* matukio yote muhimu ya chuo yapigwe picha na kuwekwa mtandaoni; wekeni mtandaoni nyaraka za mawasilisho yaliyofanyika katika mikutano au makongamano mbalimbali yaliyofanywa na walimu au wanafunzi katika sehemu duniani.

Mheshimiwa Spika, nihitimishe kwa kusema kwamba nafasi za chini kwa vyuo vyetu vikuu vya Tanzania siyo kitu chema kwani kinapunguza heshima ya nchi yetu kwenye macho ya wadau mbalimbali kama vile wanafunzi watarajiwa, watafiti, wasomi na wafadhili. Ni vyema Wizara ikachukua hatua mapema kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, suala la ubovu wa majengo ya vyuo vikuu ni la muda mrefu. *MUST,* Mkwawa, *UDOM* ni baadhi ya vyuo vikongwe ambavyo vinahitaji maboresho kabla havijaharika zaidi.

Mheshimiwa Spika, viwanja vya Chuo cha Nelson Mandela viharakishwe kujengwa ili vitumike.

Mheshimiwa Spika, suala la mshahara wa wakuu wa vyuo vikuu lifanyiwe kazi na maelezo yatolewe kadri Mheshimiwa Waziri wa Elimu alivyoahidi katika Bunge la Kumi na Mbili kwa mwaka 2021/2022.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi nzuri na kubwa iliyofanyika katika kuinua na kuboresha elimu katika Taifa letu, lakini sambamba na kuyafanya mazingira kuwa bora na ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri inayofanya lakini pamoja na kuwa wanapokea ushauri mbalimbali unaotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kuhakikisha elimu yetu ya Tanzania inakuwa ya viwango vya ushindani kwenye soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara iangalie sana suala la mabweni kwa shule za sekondari hasa za watoto wa kike kwani watoto hawa wanakutana na changamoto nyingi sana kutokana na umbali wa makazi wanayoishi na shule walizopangiwa mfano Shule ya Sekondari Morogoro hakuna mabweni ya kutosha kwa watoto wa kike hali inayopelekea watoto wa kike wa kidato cha sita tu ndio wanaopewa kipaumbele, lakini watoto wa kike wa kidato cha kwanza mpaka cha nne wanatakiwa wajitegemee huko nje.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Wizara isiige mfano wa chuo kikuu wanavyofanya ambapo watoto wa mwaka wa

kwanza ndio wanapewa kipaumbele cha kupata hosteli kabla ya wenyeji? Watoto wa kidato cha kwanza ni wadogo sana hata busara ya kujilinda huko nje kwenye nyumba za kupanga bado hawana, tunaomba walindwe kwa kujengewe mabweni ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia Wizara iweke utaratibu mzuri wa kuwahamasisha watoto wa kike kupenda masomo ya sayansi kwa kutoa motisha na kuwatambua watoto wa kike vinara kwenye masomo ya sayansi, hesabu na ufundi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia watoto wa kike ambao wanapata mimba wakiwa shuleni wanaporudi baada ya kujifungua waruhusiwe kijiunga madarasa ya watu wazima kwani wengi wao wanajisikia vibaya kurudi shule zile zile.

Mheshimiwa Spika, kuna wanafunzi ambao wazazi wao walipokuwa na uwezo walikuwa shule za *private,* lakini baada ya wazazi hao kupoteza maisha au kupata changamoto za kimaisha inakuwa ni ngumu sana kurudi kwenye shule za Serikali, tunaomba Kamishna alishughulikie hili kwani limechukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe kwa kinipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Makadirio na Mapato ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Pili nachukua fursa hii ya kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoongoza nchi yetu kwa umakini mkubwa sana. Nchi

imetulia na maendeleo yanaonekana. Namuombea kila la kheri katika uongozi wake huu.

Mheshimiwa Spika, napennda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na wasaidizi wake wote kwa namna walivyotayarisha hotuba hii kwa ubora wa hali ya juu na hatimaye kuiwasilisha katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nianze na mikopo ya wanafunzi; napenda kuipongeza Serikali yetu kwa namna inavyojitahidi kuwasaidia wanafunzi katika kuwawezesha kuendelea na masomo yao ya juu. Hili ni suala zuri sana hasa ukizingatia kuwa watoto wengi hali zao za kiuchumi ni ndogo.

Ushauri wangu katika jambo hili ni kwamba Serikali izidi kuboresha mfuko huu wa mikopo ili wanafunzi wengi zaidi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyuo vya *VETA* nchini; vyuo vya *VETA* ni vyuo muhimu sana katika kuwawezesha wanafunzi wetu kujijengea uwezo wa kuweza kujitegemea baada ya kumaliza mafunzo. Tatizo la ajira ni kubwa sana sio tu nchini mwetu bali ulimwengu mzima. Vyuo hivi vya *VETA* vinaweza kuwa ni suluhisho kubwa kwa tatizo la ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kuongeza bajeti ya kuviwezesha vyuo hivi kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Watu Wazima ni jambo zuri sana. Jambo hili lilikuwepo katika miaka ya nyuma lakini hivi sasa inaonekana sasa hivi Serikali yetu imelegeza kidogo kuliendeleza suala hili.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kurejesha elimu ya watu wazima nchini kwa manufaa ya wananchi wetu ambao kwa namna moja au nyingine walikosa fursa ya kuweza kusoma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kuja na wazo la kupitia upya mitaala yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu kwa utendaji mzuri katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika walimu wa vijijini kufundisha kutoka asubuhi mpaka saa 11 kasoro jioni, lakini walimu wa mijini wanamaliza kazi saa 8.30 mchana.

Mheshimiwa Spika, walimu wote mijini na vijijini, walimu wa vijijini wote wanahitaji muda wa ziada wa kujiandaa na masomo lakini pia kufanya kazi za kujiongezea kipato kama vile kilimo na ufugaji. Naomba sana sana muda wa kazi uwe ni mmoja.

Mheshimiwa Spika, elimu ya watu wazima ni jambo la muhimu, kuna wanaokosa elimu kwa sababu mbalimbali lakini pia kuna watu wazima wanaotaka kujiendelaza, hivyo Serikali iweke mpango wa kuendeleza elimu ya watu wazima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza hotuba ya Wizara na kwa ujumla wanavyofanya kazi kwa ushirikishwaji, napongeza sana hili linaloendelea la kuhuisha mitaala na sera, ushiriki mpana wa wadau bila

shaka utasaidia kupata mawazo mapana ambayo hatimaye tutapata kile tunachokusudia.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Watendaji wa Bodi ya Mikopo kuanzia Meneja wa hapa Dodoma na Mtendaji Mkuu wa Bodi Ndugu Badru na wasaidizi wake, wamekuwa msaada sana hasa wakati wa changamoto za mikopo, wapo watoto wa wapiga kura wetu wakiwa na changamoto kwa kweli watu wa Bodi ya Mikopo wako *very cooperative* katika kutusaidia nini cha kufanya, nawashukuru, nawapongeza na endeleeni na moyo huo huo wa kuwa *solution oriented.*

Mheshimiwa Spika, sasa katika vyuo, baada ya mtoto kupata mkopo kumekuwa na changamoto, mara fedha hazijaingia au zitaingia kwa awamu, nashauri vyuoni, vitengo vinavyohusika na *disbursement* ya *funds* kuwafikia wanafunzi vifanye kazi kwa *speed* kama wanavyofanya Bodi.

Pili, nawapongeza kwa ujenzi wa Vyuo vya *VETA*, hata hivyo nina ushauri na maombi maalum kwa ajili ya Halmashauri ya Mji Mafinga.

Mheshimiwa Spika, eneo hili linakua kwa kasi na hii ni kutokana na sekta ya mazao ya misitu, nafahamu kwamba kunajengwa Chuo cha *VETA* Mufindi, hata hivyo kwa ombi maalum, naomba katika mpango ujao kujumuisha *Mafinga TC* kutokana na umuhimu wake hasa kwa kuwa ni *centre* ya uzalishaji wa mazao ya misitu.

Kuhusu elimu ya awali; nafahamu kuna muingiliano wa majukumu katika baadhi ya maeneo ya usimamizi wa elimu kati ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI, hata hivyo kuimarika au kuporomoka kwa elimu, mwenye dhamana ni Wizara ya Elimu, kwa sababu hiyo bado tunao wajibu wa kuyatazama kwa macho mawili baadhi ya maeneo hasa eneo la elimu ya awali. Kwa mfano, kwa ufahamu wangu ukiacha *course* za

*early childhood* katika baadhi ya vyuo vikuu, kuna vyuo maarufu kwa muundo wa ki-*montesory* ambavyo ni mahususi kuwaandaa walimu wa kufundisha watoto wadogo. Lakini kama Serikali tunapoajiri walimu ni nadra kabisa kuona ajira mahsusi kwa ajili ya walimu wa kufundisha watoto wadogo kwa maana ya madaraja ya awali.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu tusichukulie elimu ya awali kama ziada bali tuchukulie kuwa ndio msingi wa kuanza kumjenga mtoto kujiamini, kujitambua, kushirikiana na wenzake na hivyo kumjengea msingi wa kuanza kuwa raia bora na mwema.

Mheshimiwa Spika, kuna kama woga wa ku-*declare* kuwa elimu ya awali itambulike kama sehemu ya elimu ya msingi na izingatiwe na kupewa uzito katika mipango yetu kama Taifa. Ushauri wangu, tusitawaliwe na woga wa gharama na tukumbuke kauli ya Mwalimu *if you think education is expensive, try ignorance*. Kwa hiyo, kama tumefikia hatua ya kuhuisha mtaala na sera, ni muhimu kuifanya elimu ya awali kuwa ni jumuishi. Tusiogope maana wakati ni sasa.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaendelea na mijadala na mashauriano kuhusu kuhuisha mitaala na sera yetu, ni muhimu tukawa makini hasa katika kuangalia wapi tulikosea na wapi tuparekebishe na kwa kiwango gani. Nasema hivi kwa sababu wapo baadhi yetu ambao tunaona kama mfumo wetu umefeli kabisa *which is not,* mfumo huu umewezesha baadhi ya Watanzania kufanya kazi duniani kote, wapo madaktari wanaofanya kazi nchi za Kusini mwa Afrika na wanategemewa, wapo wahadhiri wanafanya kazi katika vyuo mbalimbali duniani, lakini pia vijana wetu wanaosoma katika mfumo wa elimu yetu wanapata udahili katika vyuo mbalimbali duniani iwe ni Amerika, Ulaya, Asia, Arabuni na kadhalika hawajawahi kukataliwa kwa hoja

kwamba mfumo wa elimu yetu ni mbovu au haukidhi vigezo vya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunapofanya mapitio haya tusije tukafikia hatua kuona kama vile mfumo wetu wa elimu uliopo ni kama haufai, ni *zero;* hapana, lazima tujivunie mfumo wetu ulikotutoa mpaka hapa tulipo, na kwa hiyo tufanyie marekebisho baadhi ya maeneo muhimu na kwa uzito wake.

Mheshimiwa Spika, mwisho nimekuwa nikijiuliza, hivi hatuwezi kuja na utaratibu wa kidato cha tano kuanza mapema kuliko ilivyo sasa ambapo kijana anamaliza shule kwa maana ya kidato cha nne Novemba, kwenda kidato cha tano anasubiri mpaka Julai jambo ambalo ni *risk* sana hasa kwa watoto wa kike kukaa *idle* miezi *almost* sita. Kwa kuwa kuna maendeleo ambayo yamewezesha matokeo kutoka mapema, je, hatuoni ni wakati sasa watoto wanaojiunga kidato cha tano kuanza mapema kadri wataalam watakavyolidadavua. Nafahamu linaweza kuleta ukakasi na kuvurugika kwa mihula ya shule/vyuo lakini kwa kuwa tuna wataalam tujaribu kuwaza nje ya *box* kuona kama linaweza kufanyika.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwanza mtihani wa darasa la saba usifutwe kwani hali hii itafanya walimu wasiwajibike. Wale ambao hawatafanikiwa kuendelea na kidato cha kwanza waingie kusoma masomo ya ufundi na iwe kwa mseleleko.

Pili, wahitimu wa kidato cha nne na darasa la saba ambao hawatafanikiwa kufaulu vigezo vya kusonga mbele hawa iwe lazima waingine elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Spika, tatu, walimu wa kufundisha elimu ya msingi na sekondari ifundishwe na mwalimu ambaye alipata

*division one* au *two* kidato cha nne na sita. Walioko makazini wataendelea kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali ianzishe Wizara ambayo itasimamia mambo ya kujiajiri vijana ambayo itaitwa *Ministry of Self Employment and Micro Business.*

Mheshimiwa Spika, Serikali ipitie umri wa kustaafu uwe miaka 55 ili kutoa fursa ya vijana walioko mtaani kutumikia Taifa wakiwa na nguvu na kupata muda wa kujiajiri.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napongeza kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ya uboreshaji miundombinu ya elimu na uboreshaji wa bajeti ya elimu. Nampongeza pia Waziri Mheshimiwa Profesa Mkenda, Naibu Waziri Mheshimiwa Kipanga, Katibu Mkuu Profesa Nombo na wataalam wote wa Wizara kwa jinsi wanavyoendelea kuipaisha sekta ya elimu hususan kwa kufanya maboresho ya sera ya elimu na mitaala.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwanza suala la elimu ya awali lizingatiwe na kujumuishwa kama ni elimu ya lazima kwani hapa ndipo sehemu muhimu ya kumjenga mtoto.

Pili, kuna tatizo kubwa la uhaba wa walimu katika nchi yetu lakini vibali vya ajira ni vichache. Nashauri Serikali yetu ifanye kila liwezekanalo idadi ya walimu iongezeke kwani zipo shule zina madarasa ambayo hayatumiki kutokana na uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Spika, tatu, wakati elimu ya amali itakapoanza ni vyema Serikali ikatumia mfumo wa *PPP* ili kuweza kupata mazoezi ya vitendo kwa wanafunzi wetu kutoka sekta binafsi. Kwa mfano wanafunzi wataweza kwenda katika *garage,* hoteli, maduka, vituo vya ushonaji

nguo, mashambani na kwingineko ili kujionea na kushiriki kufanya shughuli husika kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, napongeza dhana ya Serikali ya kuhamasisha utafiti. Hata hivyo kuna taasisi za utafiti ambazo hazipati fedha yoyote kutoka Serikalini na kuishia kuwa tegemezi kwa wahisani. Mojawapo ya taasisi hizo ni *REPOA* ambayo ni kati ya *top ten research instructions* Barani Afrika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Ali Juma Mohamed ambao ni Viongozi wa UVCCM kutoka Jijini Dar es Salaam, wapo sehemu gani hao? Haya, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wakufunzi 11 kutoka Chuo cha Afya Mwanza *City College* wakiongozwa na Mkurugenzi wao Ndugu Zabibu Urassa, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu na adimu, kwanza kabisa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa kibali mimi pamoja na ninyi tukaweza kukutana, lakini vile vile tukaweza kujadili hoja iliyokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nishukuru kuwa mmoja miongoni mwa wachaingiaji wa hoja hii iliyokuwa mezani ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Pili, nichukue nafasi hii kipekee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kutuamini mimi na

Profesa Mkenda kuweza kutupa mamlaka na madaraka ya kuweza kushiriki kwenye uongozi wa Wizara yetu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano, kwa maelekezo, kwa miongozi mbalimbali ambayo imeniwezesha kushiriki lakini vile vile kuweza kuongoza Wizara hii. Vile vile nimshukuru sana Katibu Mkuu, Profesa Nombo, Naibu Makatibu Wakuu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi wote na Menejimenti nzima ya Wizara ya Elimu pamoja na taasisi zilizokuwa chini ya Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nikushukuru wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge lakini vile vile na Kamati yetu ya Elimu na Wabunge wote. Tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano ambao wanaotupa ili kuweza kurahisisha majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nichukue fursa hii vile vile kuwashukuru sana wananchi wangu, wapiga kura wangu wa Jimbo la Mafia. Kwanza kwa kuniamini, lakini pili kwa kuendelea kunipa ushirikiano. Pamoja na majukumu mengine haya ya Kiserikali lakini bado jimboni kule salama na kila nikienda wananipa ushirikiano wa kutosha ndani ya chama pamoja na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho, naomba niishukuru sana familia yangu kwa kuwa karibu na mimi katika kipindi chote wakati natekeleza majukumu yangu. Tunashukuru kwa hoja ambazo tumezipata, tumezipokea. Nichukue fursa hii niwatoe wasiwasi na hofu Waheshimiwa Wabunge kwa yale yote ambayo wamechangia kwenye Wizara yetu, tutakwenda kuyasimamia. Kuna maeneo ya ushauri, kuna maeneo ya maelekezo, lakini kuna maeneo ya maagizo na kuna maeneo vile vile vya marekebisho. Tutakwenda

kuyasimamia haya yote waliyoyapendekeza katika utekelezaji wetu wa bajeti katika mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa uniruhusu nami niweze kuchangia kwenye baadhi ya maeneo katika hoja iliyopo mbele yetu. Eneo la kwanza naomba kuchangia kwenye eneo la ujenzi wa vyuo vyetu vya *VETA*.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi nafahamu iko Ibara ambayo inazungumzia Serikali itakwenda kujenga vyuo vya *VETA* kwa lengo la kusogeza huduma ya elimu haswa ya ufundi karibu na wananchi na Serikali imejidhatiti kuhakikisha kwamba tunajenga.

Mheshimiwa Spika, tulianza ujenzi huu karibu miaka miwili iliyopita katika mwaka wa fedha 2020/2021 lakini tumeweza kuendelea nao katika mwaka 2021/2022 tumeweza kujenga vile vyuo 25 katika Wilaya 25 nchini lakini baadae na vile vyuo vinne vya Mikoa. Katika mwaka huu wa fedha tumeweza kuanza ujenzi katika Wilaya zile 64 ambazo zilikuwa hazina vyuo vya *VETA* na katika Mkoa mmoja wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge tutaenda kusimamia eneo hili kwa uadilifu na uaminifu mkubwa,tayari shughuli za ujenzi kule zimeshaanza. Tunafahamu ziko Wilaya ambazo zina Majimbo zaidi ya moja, kulitokea malalamiko mengi humu kwamba tunakwenda kujenga katika Wilaya na siyo katika Majimbo. Niwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge tunajua kuna baadhi ya Majimbo, tunajua kuna baadhi ya Halmashauri zimetenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivi lakini *categorically* tulisema kwamba tunakwenda kujenga katika Wilaya na siyo Halmashauri au Jimbo.

Mheshimiwa Spika, niwaondoe hofu tumepokea hoja zenu. Mipango ya Serikali ni mingi na mikubwa sana, tutakwenda kuangalia namna gani ya kufanya ili huduma hii iweze kufika katika kila Jimbo na katika kila Halmashauri. Hilo eneo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo tulisema niweze kulizungumza na katika Mradi wetu wa *HEET* ambao ni mradi wa vyuo vikuu. Tunafahamu Mheshimiwa Rais ametoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 972 kwa ajili ya kuongeza au kuboresha mazingira ya vyuo vikuu nchini. Fedha hizi zitakwenda kutumika katika maeneo makubwa matatu. Eneo la kwanza ni kwenda kujenga miundombinu katika vyuo vikuu hivi vilivyopo lakini vilevile kwenda kujenga kampasi nyingine mpya.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kufundisha walimu, wahadhiri mbalimbali ili kuwaongezea ubora. Tumezungumza hapa Profesa Ndakidemi amezungumza, Profesa Muhongo saa hizi ametoka kuzungumza kwamba ubora wa vyuo vyetu, hatuwezi kuwa na vyuo bora bila kuwa na mazingira bora. Kwa hiyo eneo la kwanza tunakwenda kujenga miundombinu lakini eneo la pili tunakwenda kufundisha wahadhiri wetu, eneo la tatu tuhakikishe kwamba ni lazima tuwe na vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Kwa hiyo, fedha hii tunakwenda kuitumia zaidi ya asilimia 75 itakwenda kwenye hizo *infrastructures.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo ya namna gani tunaweza tukatumia fedha hii na alielekeza kwamba tusogeze huduma za elimu ya juu karibu na wananchi. Kwa mantiki hiyo, taasisi ambazo zitanufaika na fedha hizi karibu taasisi 19 na vyuo vikuu karibu 14 lakini na taasisi nyingine mfano, Taasisi yetu ya Elimu ya Juu *(TCU)* nayo itafaidika na fedha hizi, Bodi ya Mikopo itafaidika, amezungumza hapa Profesa Muhongo. Taasisi yetu ya

*COSTECH* nayo vilevile tunaendelea kuifanyia *reform* kubwa sana. Fedha hii itakwenda kutumika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba niitaje Mikoa ile michache ambayo itakayokwenda kunufaika moja kwa moja au tunakwenda kujenga kampasi mpya kabisa katika Mikoa ambayo ilikuwa haina kampasi hizo. Mkoa wa kwanza ni Mkoa wa Katavi, tutakwenda kujenga huko, Mkoa wa pili Mkoa wa Lindi tunakwenda kujenga, Mkoa wa Tanga, Tabora, Ruvuma, Manyara, Shinyanga, Singida, Geita, Kigoma, Kagera, Mwanza, Rukwa na Mkoa wa Simiyu. Mikoa hii yote tunakwenda kufanya kazi, mchakato uko katika hatua za mwisho. Tulianza kwanza na *feasibility study* wameshafanya *procurement* ya *consultant* na sasa tunafanya *procurement* ya *contractors* na tayari kazi inakwenda kuanza ndugu zanguni. Kwa hiyo, naomba niwaondoe hofu jambo hili linakwenda kufanyika kwa uaminifu na uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni eneo la Wadhibiti Ubora; limezungumzwa sana suala la Wadhibiti Ubora na tunafahamu kwamba kulikuwa na waraka toka mwaka 2014, namna gani wadhibiti ubora wanakwenda kuwa na stahiki zile zao za kawaida lakini vilevile mishahara. Ni kweli waraka ule hatujaweza kuutekeleza kwa kipindi chote hiki lakini niwaondoe hofu, Mwezi Aprili mwaka huu tulipeleka muundo mpya wa Wizara ambao umeingiza sasa hawa Wadhibiti Ubora kama viongozi na Mheshimiwa Rais tayari amesharidhia waraka ule toka mwezi wa nne mwaka huu na ifikapo mwezi wa saba, Wadhibiti Ubora wale wote wanakwenda sasa kuwa katika zile kada za uongozi wanaweza sasa wakalipwa zile stahiki kadiri mlivyoshauri tutakwenda kufanya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo liliambatana na hilo la wadhibiti ubora ni mazingira yao ya kufanyiakazi, imezungumzwa hapa kwamba katika ukaguzi wa taasisi zetu

za shule ni asilimia chache sana kama 26 tu ndiyo ambayo imeweza kukaguliwa. Niwaondoe hofu Serikali imeshafanya makubwa sana kwa upande wa Wadhibiti Ubora. Miongoni mwa mambo ambayo tayari yameshafanyika na Serikali ni ujenzi wa ofisi mpya za Wadhibiti Ubora 160 lakini tumefanya ukarabati wa ofisi za Wadhibiti Ubora 31 lakini vile vile tumenunua magari 119 na kusambaza kwenye Halmashauri pamoja na Wadhibiti Ubora katika Kanda pamoja na Mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hiyo tumeweza kufanya ununuzi wa kompyuta 195 zile kompyuta za mezani, lakini tumenunua *laptop* 1,082. Sambamba na hiyo tumesambaza vile vishikwambi ambavyo vilitumika. Vile vilivyogaiwa walimu vilevile wadhibiti ubora wamegawiwa. Lengo kuu hapa la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatengeneza mazingira wezeshi ili wenzetu wadhibiti ubora waweze kufanya kazi yao katika mazingira mazuri na salama kwa sababu ndiyo jicho letu kule la kuangalia elimu ya vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ambalo ningependa labda nilifafanue kidogo ni kwenye eneo la lishe. Nalo vilevile limezungumzwa sana, mnakumbuka tulitoa Waraka wa Elimu Na. 3 wa mwaka 2016 ambao ulikuwa unaeleza wazi namna gani jamii itashirikishwa kwenye suala la kutoa lishe mashuleni. Vilevile tulitoa mwongozo wa mwaka 2022 wa namna gani vile vile jamii itahusishwa.

Mheshimiwa Spika, tumepata malalamiko hapa uchangiaji ule unatofautiana kutoka eneo moja na eneo jingine. Tutakwenda kufanya marekebisho katika eneo hilo ili kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapokuwa shuleni wanaweza kupata lishe ambayo itakayowawezesha kujifunza katika mazingira ambayo ni salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii ya kuchangia na kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi, rekodi inaonesha tumepata michango jumla ya 51 na shukrani za kipekee nazipeleka kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Husna Sekiboko. Michango yote ya Kamati tumeipokea mingi ni muhimu sana kwa asilimia kubwa tutayafanyia kazi na mahali tutakapohitaji kujadiliana tutajadiliana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla tunashukuru sana kwa kuungwa mkono kwa sehemu kubwa mno kwa hoja yetu hii tuliyoileta, kwa ushauri na maelekezo ambayo Waheshimiwa Wabunge wametupa, naomba niseme ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge na ahsante hizi ni kutoka kwangu na kutoka kwa wenzangu wote wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana mpitishe bajeti hii kama tulivyoomba. Kabla sijazungumza hoja na masuala mbalimbali ningependa kumshukuru sana kwanza Mheshimiwa Omari Kipanga, Naibu Waziri wa Wizara yetu na Katibu wetu Mkuu Profesa Nombo, Naibu Katibu Mkuu

Profesa Mdoe, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Rwezimula pamoja na Kamishna wa Elimu Dokta Mtahabwa na watumishi wote wa Wizara na taasisi zote kwa kufanya kazi pamoja nasi, kwa sehemu kubwa na chochote ambacho tutakuwa tumefanikiwa kwa kweli ni kazi imefanyika kama *team work*. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niitumie fursa hii vilevile kuwashukuru wananchi wetu wa Rombo kwanza kwa kumuunga Rais wetu mkono, wanaendelea kumuunga mkono kwa asilimia kubwa sana. Wanaiunga mkono Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dokta Samia Suluhu Hassan na vile vile wanaendelea kuniunga mkono katika shughuli zangu za Ubunge na wanatambua kwamba muda mwingi nipo huku kwa shughuli za Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee sana naomba nikushukuru wewe na uongozi wote wa Bunge letu. Naibu Spika na Wenyeviti kwa kutuongoza vizuri sana katika shughuli hizi. Natoa shukrani zangu za dhati sana kwa Walimu wote, Wakufunzi na Wahadhiri hapa nchini na nadhani tuliwaleta wale walimu wanaofundisha kwa namna ya ubunifu na hamasa sijui kama wapo humu ndani. Sasa hivi *clip* zao zilikuwa zinatembea, labda wangesimama sijui kama mimi naruhusiwa kutambulisha watu lakini walimu hawa katika mazingira hayo hayo wako Mikoani wanafundisha kwa namna ambayo kwa kweli inatia hamasa unatamani ungerudi kuwa mtoto ufundishwe na walimu kama hawa, wako wengi lakini tumewaalika wawili hapa kwa kuwapa heshima na wengine tutaendelea kukutana nao.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao wadau wengi wa elimu. Wadau wetu wa elimu kwa ujumla tunashukuru sana na wengine wako hapa, wengine ni *local* kwa mfano nadhani Meneja Mkazi Roselyn Marik wa '*So they can Tanzania*' ambaye tunashirikiana nadhani yuko humu ndani vilevile tuko naye, na Rais wa *Tanzania Academy of Sciences* Profesa

Yunus Mgaya ambaye nadhani yuko humu ndani. Wamiliki wa shule binafsi ambao kwa kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mulugo na ninakushukuru sana kulisema hili, nakushukuru sana kwa dhati ya moyo wangu, kwamba tumefanya nao kazi kwa karibu sana sekta binafsi, tumeshirikiana nao sana kama nitakavyoeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja zilizotoka hapa nyingi kama nilivyosema tutazibeba. Zipo hoja nyingine ambazo zinagusa sekta ya elimu zote lakini nyingine za TAMISEMI, nyingine Utumishi na kadhalika lakini zote zinagusa sekta ya elimu, nitajaribu kuzieleza zote nyingine tutazifanyia kazi ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia wote kabisa wote kabisa wamempongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wamempongeza sana kwa jinsi ambavyo ametoa kipaumbele kikubwa sana kwa ujasiri mkubwa sana kwa utashi mkubwa sana wa kisiasa kwa sekta yetu ya elimu kama ambavyo nitajaribu kueleza kidogo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaona kama alivyosema Naibu Waziri hapa *VETA* sasa hivi katika Wilaya 64 pamoja na mikoa, kumaliza wilaya zote ambazo hazina *VETA*. Mradi wa *HEET* Mikoa 14 inanufaika kupata kampasi za vyuo vikuu ambavyo vilikuwa hamna. Hakuna Mheshimiwa Mbunge yeyote hapa ambaye kwake katika jimbo lake hakuna shule mpya, madarasa mapya, pengine kampasi ya chuo kikuu, kuna *VETA* inajengwa na kadhalika. Hakuna Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye hana suala la elimu ambalo analo la kujivunia na kulisemea kwa wananchi na kwa sababu kwa kweli haya ni maelekezo *specific* ya Rais wetu Mheshimiwa Dokta Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Walimu, Walimu ndiyo watumishi walio wengi zaidi Serikalini, kwa walimu ujasiri wa Rais wetu kusema kwamba tuende kwenye sensa, tutumie vishkwambi ili vishikwambi hivyo vianze sasa kutumika katika kufundisha na vimegawanywa kwa walimu wote kabisa wote Tanzania Bara na Visiwani pamoja na Maafisa Elimu na wakufunzi wa vyuo vyetu vya *FDC, VETA* pamoja na Wadhibiti Ubora hapa nchini, yalikuwa maamuzi ya Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanafunzi wa vyuo vikuu, pamoja na kukutana uongozi wa wanafunzi wa vyuo vikuu kuwaongezea maslahi yao lakini ameendelea kuongeza fursa ya mikopo kubwa sana kwa wanafunzi wote. Kwa hiyo, kwa kweli ninaelewa kabisa ni kwa nini kila kila kila Mbunge aliyezungumza hapa bila kukosa na tumerekodi wote kila mmoja alianza kwa kusema tunampongeza na kumshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa kuliko yote na ninadhani Mwenyekiti wetu wa Kamati Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo alilieleza vizuri sana. Kubwa kuliko yote ni maamuzi magumu ya Rais wetu kwamba tufanye mageuzi makubwa sana kwenye elimu, kwa kufanya mapitio ya sera na mabadiliko ya mitaala. Mageuzi haya yana gharama na mara nyingi ni rahisi sana kutafuta kitu ambacho matunda yake yanaonekana katika miaka miwili, mitatu, minne, mitano, lakini mageuzi haya ya elimu matunda yake halisi yataonekana kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, inahitaji utashi mkubwa sana wa kisiasa kuingiza Taifa katika maamuzi haya mazito, kufanya mabadiliko yatakuwa na gharama zake na matokeo yake makubwa yatakuja mbele ya safari. Kwa jambo hili kubwa hata mimi binafsi na yote aliyoyafanya Rais wetu, naungana na Waheshimiwa Wabunge wote kumpongeza na

kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kweli mimi na wenzangu wote katika Wizara tunajisikia tuna bahati kubwa sana kupata fursa ya kuhudumu kipindi hiki ambacho Rais wetu ameelekeza jicho lake, ameelekeza maono yake katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, chochote kitakachotokea hapa pengine wengine watatutaja mimi, wengine watamtaja Ndalichako kwa sababu tulikuwepo lakini yalikuwa ni maelekezo ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana vilevile viongozi wetu Wakuu Mheshimiwa Dkt. Isdor Mpango, Mheshimiwa Dkt. ` Hussein Mwinyi kwa sababu suala la elimu kuna sehemu inaenda *across the border* na Rais wetu na kutupa miongozo mingi mizuri kutuwezesha kusonga mbele na Mawaziri wenzangu ambao tunafanya kazi vizuri kwa pamoja kumsaidia Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo moja ambalo limezungumzwa kubwa sana ni kuhusu muingiliano na mgongano wa majukumu kati ya sekta ya elimu na TAMISEMI. Kamati imezungumza, nadhani Mheshimiwa Mulugo ndiyo amelifafanua zaidi *specific* maeneo ambayo yanaumiza na mapendekezo yametoka kwamba kuwe na chombo maalum cha kusimamia elimu nchi nzima au pengine elimu yote iwe chini ya Wizara moja na kadhalika. Sasa kuna suala la ugatuaji na suala la kuendesha ugatuaji kwa ufanisi nadhani suala linahitaji mjadala.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwa na chombo cha kusimamia elimu ni pendekezo ambalo nadhani limeletwa katika mapitio ya sera na ninajua tutapata fursa Waheshimiwa Wabunge wote kupitia mapitio hayo na

kulizungumza, vilevile tukumbuke kwamba ugatuaji wa madaraka una sababu zake, msingi wake na umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, nitalizungumza suala moja ambalo lilizungumzwa hapa na Mheshimiwa Mulugo. Tunajua kwamba TAMISEMI inamiliki shule kama ambavyo BAKWATA inamiliki shule, Baraza la Maaskofu linamiliki shule, sekta binafsi zinamiliki shule. Wizara ya Elimu iko pale inasimamia sera, sheria na kadhalika. Kama ambavyo Waziri wa Kilimo anaweza asiwe na mashamba lakini kuna watu wana mashamba na kuna mashamba mengine ya Serikali mengine ya watu binafsi anamiliki pale.

Mheshimiwa Spika, sasa changamoto moja aliyoisema Mheshimiwa Mulugo na ninaitolea utatuzi hapa hapa ni kwa TAMISEMI kuchukua wakati mwingine jukumu la kutoa amri kwa shule binafsi kwamba sasa kuna mitihani wote lazima mfanye, lazima mfanye leo, keshokutwa mfanye na mlipie. Nimeongea na Kamishna wa Elimu kwa sababu na mimi naheshimu mamlaka yake japokuwa mimi ni Waziri na ameniambia atatoa tamko, maelekezo kuanzia sasa hivi, kuanzia leo shule binafsi hazitalazimishwa kufanya mitihani ambayo inapangwa na Halmashauri na kadhalika kwa amri na kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahimiza zishiriki kwa hiari kufanya mitihani hiyo lakini hazitolazimishwa kufanya mitihani, taratibu za mitihani na kadhalika zinatolewa na Kamishna wa Elimu kwa mujibu wa Sheria yetu ya Elimu ambayo ipo, nadhani hilo tunaweza tukalimaliza. Yako mambo mengine chungu mzima ya ufanisi tu kati ya TAMISEMI na Wizara ya Elimu kwa sababu na tunafanya kazi vizuri sana kwa kweli na nadhani tutaendelea kufanya hivyo lakini suala la mitihani Kamishna ameniambia atalileta, tutaliona, tutalimaliza kwa namna hiyo. Mengine tutaendelea kuyajadili katika sera na sheria.

Mheshimiwa Spika, wengi wamezungumzia sana kuhusu mapitio ya sera na mitaala. Mmoja alisema kwanza tuanze kubadilisha sheria. Kimsingi sheria inatokana na sera. Ni vigumu sana kubadilisha sheria ya mwaka 1978 sasa hivi ya elimu kabla ya kubadilisha sera. Kwa mfano, sera ya mwaka 1978 ndiyo inasema elimu ya lazima ni miaka saba. Huwezi kwenda kubadilisha sheria kwanza ukasema kwamba sasa sheria iseme elimu ya lazima miaka 10 bila kuwa na sera inayosema elimu ya lazima ni miaka 10. Nawahakikishia na mtakumbuka mwaka jana wakati nilivyokuja hapa mbele yenu kwenye Bunge lako Tukufu, nilieleza kwamba kuna mambo saba ambayo tutakuwa tunayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nilisema ni sera, nikasema mitaala, nikazungumzia sheria, nikazungumzia idadi ya walimu, nikazungumzia ubora wa walimu, nikazungumzia miundombinu, nikazungumzia vitendea kazi na kadhalika. Vitu saba tuliweka kwenye bajeti ambavyo bado tunavifanyia kazi. Kwa hiyo, suala la sheria litakuja tukishamaliza tu sera hii, kuna masuala chungu nzima ambayo itabidi tuende tukabadilishe kwenye Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978, ama kuifumua yote upya au kufanya mabadiliko kulingana na jinsi ambavyo sera itakuwa imepita.

Mheshimiwa Spika, kadhalika mitaala, kwa kawaida mitaala mingi inapita Waheshimiwa Wabunge haiji Bungeni, haiji kujadiliwa hapa. Sasa hivi tumeileta hapa kwa sababu mitaala hii inaendana na *structure* mpya ya sera ambalo ni jambo kubwa sana, hatuwezi kulibeba wenyewe tu kama Wizara na kwenda nalo. Kwa hiyo, naona tumeleta tutakapopeleka hata *cabinet paper* itakuwa na mapitio ya sera na itakuwa *addendum* ya mitaala jambo ambalo mara nyingi linamalizwa kwenye taasisi ya elimu tu huko nyuma tulivyokuwa tunakwenda. Kwa hiyo, ndivyo ambavyo tutakuwa tunakwenda katika kufanya hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa yako masuala chungu mzima yamezungumzwa hapa kuhusu mapitio ya sera. Pengine nisingependa niyajibu yote, kwa sababu gani? Tuliomba na ulitupa ruhusa tukafanya semina kwa Waheshimiwa Wabunge, tukawapitisha kwenye mapitio ya sera na mitaala, lakini tulifanya wakati wa *break* baada ya kukutana asubuhi halafu tulikuwa turudi mchana. Wabunge wengi wakasema; najua Mwenyekiti wa Kamati ambaye alikuwa ana-*chair* pale, akasema atakuona, kwamba ni vizuri tutafute siku ya *weekend,* tuwe na kutwa nzima ya kupitia mapitio ya mitaala tuliyoyafanya pamoja na sera hiyo ili tuweze kupata maoni kamili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baadhi ya maoni niliyokuwa nayasikia hapa kwa kweli, naamini kwa sababu kumekuwa hakuna muda wa kutosha kupitia, na tutaomba tupate kibali hicho hapa tunavyoendelea, na ninaomba sana tuweze kupata kabla ya tarehe 31 Mei, 2023.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba tutaomba tuwapitishe tupate maoni yenu, kwa sababu tunaamini sana nyie ni wawakilishi wa wananchi wote wa Tanzania, lakini hata mwenye maoni tutaendelea kuyapokea, kwa sababu baada ya kufanya kongamano lile kubwa tulitangaza hadharani makusudi ili kuchochea watu wengi zaidi walete maoni, na watu wengi sana walifuatilia na wengi wanaendelea kuleta maoni. Tunaendelea kupokea maoni. Tunatarajia kwamba tukifika tarehe 31 Mei, 2023, kwa kweli kila mtu atakuwa ameshaleta maoni yake, tutayachakata na kuandaa *cabinet paper* kwenda kupata *approval* kwa Mheshimiwa Rais kupitia washauri wake ambao ni Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata baada ya mambo tuliyoyazungumza hapa, japokuwa nitayazungumza tena kidogo, kwa mfano suala la lugha, bado kuna fursa ya kutoa maoni, kuyaleta na kuona namna ambavyo tunaweza

tukayachakua. Nitafafanua kidogo kuhusu suala la lugha, lakini umuhimu wake ndiyo huo, bado safari ya kukusanya maoni ipo. Ilianza mapema wakati Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako akiwa Waziri wa Elimu, tumeendelea nayo. Ndiyo maana nasema haya mageuzi ni makubwa sana, na hatufanyi kwa kukurupuka.

Mheshimiwa Spika, kuna suala limezungumzwa sana kuhusiana na sera na sheria, kwamba sasa hii sheria mkifanya, kuna uhaba wa walimu na uhaba wa miundombinu. Hatuwezi kukataa ukweli wa uhaba mahali ulipo, takwimu zenyewe zipo. Tuna kitabu kinaitwa *Basic Education Statistics of Tanzania,* kiko hadharani, kila mtu anaweza akaangalia. *Pupil Teacher's Ratio* katika kila Halmashauri ni kiasi gani? Ni *facts* ambazo tunazo na sisi Wabunge tunafahamu maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, upo upungufu tunaweza tukaukiri, lakini shukrani zote tulizompa Mheshimiwa Rais hapa ni kwa sababu *speed* ya kuongeza miundombinu mashuleni sasa hivi wote tumeiona. Kwa kasi hii, tunatarajia kwamba tunaweza tukaendelea na safari hii ya mageuzi tunayoyafanya wakati tuna-*catch up* na miundombinu. Tunaona jitihada za Rais wetu sasa hivi za kuanza kuajiri. Ujue kwamba ajira ilikuwa *frozen* kwa muda fulani ambayo inaleta changamoto kidogo kwa sababu kuna watu wengi walimaliza shule hawajaweza kuajiriwa, lakini tunaona kwa kuangalia *budgetary implication* jitihada za kuajiri zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, zaidi niseme vilevile kuna suala limezungumzwa hapa la mwongozo, Mheshimiwa mmoja alisema hapa, mwongozo wa walimu wa kujitolea. Wiki hii tunautoa na tumeanza kuzungumza na watu ambao wanaweza wakatusaidia kuhakikisha kwamba kweli, tunaweza kuhakikisha kwamba hawa wanaweza wakatusaidia kufundisha. Tutatumia teknolojia vilevile kuhakikisha kwamba tunapambana na uhaba huu wa

walimu. Kuna mambo mengi sana tunaweza tukayafanya wakati ambapo Serikali inaangalia *budgetary implication* inaongeza ajira za walimu, nasi tutajitahidi kufanya hivyo hivyo. Hii ni pamoja kwa wakufunzi na Wahariri wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi unaweza kuona kuna Mhadhiri wa *Econometrics,* yuko Dar es Salaam anafundisha darasa la *UDOM*. Tumefanya hivyo, najua nilivyokuwa nafundisha pale, watu wanafundisha kwa *zoom,* unafundisha watu wako Ghana, unafundisha kutokea Dar es Salaam. Nadhani tunaweza tukajitahidi hivyo kwenda mbele. Hata hivyo, Rais wetu kwa mwendo anaoenda nao, tunaamini kwamba tunaweza tukasogea mbele kuhakikisha kwamba tutapata hivyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kubwa ambalo limezungumzwa sana ni tahadhari, kwamba mageuzi haya tumejiandaa vipi? Tunaendaje kutekeleza mageuzi haya? Yupo Mheshimiwa mmoja, nadhani ni Mheshimiwa Shigongo kama sikosei, alisema, tusijadili sana, dunia inaenda kwa kasi sana. Tutakuwa na mitaala, kabla haijatekelezwa utakuta tumeshapitwa na wakati. Wako wengine nadhani Mheshimiwa Tabasam alisema, tuwe tahadhari. Alitupa historia sana ya mageuzi ya mitaala tangu wakati wa Ujerumani mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, haya yote ni muhimu, kwenda kwa kasi ili tusichelewe na kuchukua tahadhari ili tusiboronge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kalenda ile ya utekelezaji ambayo tuliileta kwenye semina kwenu, tulisema kwamba mwezi Januari mwakani tunaanza na *pilot.* Tunaishi kwa matumaini kwamba kwa kweli pendekezo letu litapita, rasimu hizi zitakubaliwa, iwe ni sera ya elimu na mafunzo 2014, Toleo la 2023 na mitaala yake itapita. Sisi tumeamua tunaanza kidogo kidogo mafunzo ya amali kwa sababu tunataka mafunzo ya amali tusiharibu. Hatutaki anayekwenda kwenye

mafunzo ya amali ajisikie ni *failure*. Hatutaki kujenga mazingira ya mwanafunzi ambaye angependa kwenda upande wa mkondo wa mafunzo ya amali, aone kwamba kila mtu atamwona ni *failure*. Ndiyo maana tumeweka *pathway* ya mikondo yote miwili.

Mheshimiwa Spika, ukienda elimu jumla unaweza ukaenda mafunzo ya amali baadaye, ukienda mkondo wa mafunzo ya amali, utapunguza masomo, lakini bado kuna *pathway* ya kwenda *high school* na kwenda chuo kikuu kama kawaida. Tunataka tuhakikishe kwamba wote wanajisikia ni Watanzania bila kubaguliwa. Tutajenga mkakati baadaye wa namna ya kuwashauri wanafunzi kwamba wewe umefika Darasa la Sita, tunadhani itatusaidia sana, wewe unapenda sana michezo ukichukua masomo yako manne, matano halafu ukaenda Shule ya Michezo *A-Level,* utaenda mbali sana kwenye michezo, lakini unaweza ukaenda Chuo Kikuu kupitia yale masomo machache ambayo unachukua, halafu baadaye ukaenda ukafanya *Diploma* ukaendelea. Kadhalika mwingine anaweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa tulichofanya, tumechagua shule ambazo ni *prestigious.* Zamani kila mtu anajua tuliosoma enzi hizo, kwamba walikuwa wanaenda zile shule zilikuwa zinaitwa *Tanga Tech.*, *Ifunda Tech.*, *Bwiru Boys Tech.*, *Moshi Tech.,* ndio wale waliofanya vizuri sana darasani. Tena uwe mzuri sana kwenye hesabu, lakini yale mafunzo ya amali, ukisoma *form one* ukiingia *form two* unapata cheti. Hata ungeacha shule, unaweza ukaajiriwa kwa sababu una cheti. Ukifika *form five* unapata cheti cha *level* fulani unaondoka.

Mheshimiwa Spika, sasa tumeamua kwamba sisi tunaanza na vyuo vya ufundi vile tisa. Tumeweka bajeti hii ambayo tunaomba muipitishe sasa hivi, ili vyuo vifuatavyo tunaenda kuviwekea miundombinu. Tunavifahamu, tumevikagua ili mwezi Januari vichukue wanafunzi, waanze

mwaka wa kwanza kwa mitaala mipya ambapo watakuwa na masomo machache ya elimu jumla. Watafanya shughuli nyingi zaidi ambazo ni mafunzo ya amali, wakimaliza pale, ni *full technician,* wako *very qualified,* wanaweza wakaajiriwa, lakini wakitaka, wanaweza kwenda kwenye *diploma*, wakitaka yale masomo machache wanaweza wakaenda *high school.* Shule hizo ni Bwiru, Chato, Ifunda, Iyunga, Moshi, Mtwara, Musoma, Mwadui na Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niseme, hapa yuko mdau, nilimtaja Rose Mariki makusudi kabisa ambaye alitusaidia sana kujenga chuo kule Babati, wamesema na wenyewe wanataka kuweka hela kuhakikisha kwamba tunaweza tukaanza shule ya mafunzo ya amali. Sekta binafsi pia, wengine wameshajitolea sasa hivi wanasema tuko tayari. Sijui kama naweza nikawataja, walisema tuko tayari, tupate maelekezo na mitaala hiyo na sisi tuhakikishe na sisi tuna shule zetu za mafunzo ya amali ambazo zinafuata mitaala yetu, halafu tunasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaanza kwa *pilot,* lakini tunavyoenda kufanikiwa, tutasonga mbele. Zaidi ya hapo, tunaanza na walimu. Tumetenga bajeti. Kwenye bajeti hii ambayo tunaipitisha sasa hivi, tumetenga bajeti za kuandaa walimu wa kwenda kufundisha. Tunaangalia shule za ufundi, zina walimu, lakini hawatoshi, kwa hiyo, tunafanya juhudi za kuwafundisha lakini *training, re-training, and re-orienting* kwa walimu wetu itakuwa ni kazi kubwa sana mbele yetu kwa sababu baada ya *document* hizi kupita ambazo nadhani baadhi ya Wabunge walisema ni *one of the best* kwa kweli, tunaweza tukaharibu kama tusipokuwa na *very good management* ya *process* ya *implementation.* Kwa hiyo, tunakwenda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo suala la lugha kwa sababu limeleta mjadala hapa. Kwanza niseme, hatujafunga mjadala, hatujafunga maoni, kwa hiyo, siyo

suala la kusema kwamba tumeshapitisha. Zile zinaitwa rasimu na tumesema maoni mpaka tarehe 31 Mei tutapokea maoni. Tuna semina ya Wabunge inayokuja na kuna nafasi ya kuzungumza sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye lugha kuna vitu viwili ambavyo vimefanyika ambavyo ni vizuri sana tuvione. Kwanza, kwenye sera yenyewe imetoa fursa ambayo ipo sasa hivi, kwamba ukitaka kuanzisha shule yako hii iwe *english medium* ambayo ni *primary,* wakati huo itakuwa kuanzia elimu ya awali mpaka darasa la sita, unaomba kibali maalum, unakaguliwa, umejiandaaje, unaweza ukapata. Ukifika *form one* kwenda juu ni Kiingereza, ila ukitaka *form one* kwenda juu kufundisha Kiswahili, unaomba kibali maalum, ukaguliwe kama umejiandaaje. Kama umejiandaa vizuri unaweza kufundisha unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, hatuwezi sisi kama Taifa tukasema tumefungia Kiswahili, lakini najua mwendo wa kwenda kwenye Kiswahili utakwenda kwa tahadhari kubwa hata wazazi wengi, kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, kwa tahadhari kubwa kwa sababu tutapenda kuhakikisha kwamba kweli tunapokwenda kule hatutashusha kiwango cha elimu. Milango iko wazi, nasi kama Serikali tutajitahidi kuhakikisha kwamba hata watakaokwenda kule, kweli wakatoe elimu ya viwango. Kwa hiyo, hilo lipo.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo tumelifanya kubwa, na maoni yametolewa na Mheshimiwa Husna, na Mheshimiwa wakati unaongea nilijua ulisoma *document thoroughly,* kwa hiyo, nilikuwa *very excited* wakati unaongea. Kwa sababu ufundishaji wa lugha umebadilishwa kwenye mitaala, na ninaomba msome mitaala hiyo. Hatufundishi tena sijui *syntax,* sijui nini; *rules* nyingi sana, halafu unamaliza darasa la saba huongei Kiingereza. Unafundishwa Kiingereza cha kuongea, ukimaliza darasa la saba ni aibu uanze kusoma Kiingereza, unamaliza huwezi kuongea, darasa la saba.

Kadhalika unamaliza darasa la saba, unaboronga Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, hata tunaposema kwamba vijana wetu wanamaliza darasa la saba sasa hivi hawaongei Kiingereza, ina maana ufundishaji wetu hauendi vizuri. Kwa hiyo, tumefanya mapitio, tutumie wataalam wa lugha, ufundishaji huu uache kukazia *rules* ambazo ni *so boring,* mwanafunzi hajui kama anajifunza lugha, ajifunze *straight* namna ya ku-*communicate* na kuongea, kwa sababu watu wanajifunza Kimasai, wanajifunza Kiusukuma, wanajifunza Kinyakyusa, wanaelewa ndani ya miaka mitatu. Utakaaje shuleni miaka minne unajifunza Kiingereza utoke huwezi kuongea Kiingereza chenyewe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, sasa hivi somo la Kiingereza litaanzia darasa la kwanza. Litafundishwa kama somo moja na tutahakikisha kwamba ukimaliza Darasa la Sita, kweli uweze kuongea Kiingereza. Hizo *rules* zitakwenda tu kwa sababu huko mbele ya safari tutazungumza suala la *communication* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa alipokuwa anazungumza hapa, kwa kweli na mitaala iko huko. Nakuomba usome, kama kuna *comments* zaidi tutazipokea na *comments* nyingine kutoka kwa watu wote mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Kiswahili, kwa sababu tusije tukadhani kwamba watu wanaongea Kiswahili fasaha kwa Tanzania. Kwa sababu tunasema kwamba tuongee Kiingereza fasaha, Kiswahili chenyewe tunaboranga. Sikilizeni tu watu wanapoongea, hata tafsiri tu na lafudhi na kadhalika, ni vitu ambavyo lazima shuleni tujaribu kuviimarisha na kuvifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze suala lingine; je, Serikali inaona sekta binafsi ni washindani? Yaani shule binafsi ni washindani wa Serikali? Narudia tena, yaani Wizara inaona shule binafsi, vyuo binafsi ni washindani? *Never,* hapana, haijawahi kutokea, haitatokea na haiwezi kutokea chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na haitatokea baadaye. Hii ni Serikali ya wananchi na hizi shule zinafundisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi, bosi wangu alikuwa Mheshimiwa Charles Mwijage, alikuwa Waziri wangu, ndio aliniagiza tutengeneze *blueprint* ya kuimarisha sekta binafsi. Tulifanya kazi hiyo, siyo kwa sababu nilielekezwa na bosi wangu, *we had passion* ya kusimamia na kuendeleza sekta binafsi. *Blueprint* mpaka sasa hivi inazungumziwa. Haiwezekani leo, mimi binafsi kwa mfano, niko Wizara ya Elimu halafu nianze kufanya kazi dhidi ya sekta binafsi. Hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shule binafsi pamoja na vyuo vikuu vimekuwa msaada mkubwa sana Tanzania, na nadhani Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, sikumbuki nani alisema hili. Tulikuwa tunaona watoto wetu wadogo wanaondoka wanaenda kusoma Kenya na Uganda. Leo mabasi shule zikifunguliwa, huoni wanakwenda, shule zimetufuata nyumbani. Tunazifurahia, tutazilinda, tutazitetea. Narudia tena Mheshimiwa Mulugo kwa kusema ukweli hapa, kwamba tumekutana mara nyingi sana na kuongea. Kwa kweli ndiyo mwendo wetu, na tutakwenda kufanya kazi hivyo hivyo mbele ya safari. Tutakaa pamoja na tutaendelea.

Mheshimiwa Spika, niwaambieni ukweli maelekezo ya Rais wetu. Hivi vyuo binafsi, tumetenga hela kwa vyuo binafsi kuwasomeshea wahadhiri wao. Mara ya kwanza Serikali inatoa hela kwenda kusoma. Wataenda kusoma Wahadhiri binafsi *South Africa.* Unalipiwa na Serikali kwa sababu

unafundisha chuo binafsi. Kwa hiyo, Serikali hii haioni kabisa sekta binafsi kama ni wapinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tulipokutana mara ya mwisho, alikuwa Mwenyekiti wa Wamiliki wa Shule, alisema kitu kimoja, na nitakirudia, kwamba na sisi sekta binafsi tusaidiane na Serikali, kwa mfano katika kupambana na wizi wa mitihani. Tusionekane sisi tunalalama kwamba Serikali kwa nini tunapambana na wizi wa mitihani, na sisi tusaidiane kupambana na wizi wa mitihani. Yeye mwenyewe ni *owner* wa shule akasema, mimi binafsi niligundua nilikuwa natoa motisha kwa walimu wanaofanya vizuri wakawa wana-*organize* wizi wa mitihani, nimechukua hatua. Hiyo ilitoka sekta binafsi yenyewe. Kwa sababu sisi tunapopambana na wizi wa mitihani, hatupambani na sekta binafsi wala sekta ya umma.

Mheshimiwa Spika, sisi tuliofanya mapitio ya mitaala katika mikutano yetu yote kabisa, tumekuwa tukiita sekta binafsi, wamiliki wa shule, walimu kutoka sekta binafsi, wote wameshiriki na ukweli wametoa mchango mkubwa sana hapa. Sasa vitu vingine ambavyo vimesemwa kwamba pengine ni dalili kwamba sisi tunapambana na sekta binafsi. Hili sikutarajia nitatoa tena maelezo. *Ranking of schools,* ooh mmeondoa kumi bora kwa sababu hamzipendi shule binafsi. Nilieleza vizuri hapa, lakini sasa niulize swali, kwamba ooh, mmeondoa ushindani, kwa hiyo, shule zetu zitaboronga. Ushindani gani tumeondoa?

Mheshimiwa Spika, bado tunatoa A, tunatoa B, tunatoa C, si ushindani huo! Tunatoa *first class, second class* na tunatangaza, si ushindani huo? *Samia Scholarship,* unapewa kulingana na *performance* yako na watu wanatangaza, si ushindani huo! Kwenye *Samia scholarship* wako wanafunzi wametoka *private sector* ambao wamepata *Samia scholarship,* si ushindani huo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachosema sisi, ushindani lazima tutegemee kigezo kinachokubalika. Sisi tunashindanisha wanafunzi waliosoma masomo ya *science* na tumewapa *full scholarship* ambayo sisi Wizara ndio tumeamua iitwe *Samia Scholarship.* Tunaangalia wame-*perform* vipi na tunakutaja. Tumesema hivi kuhimiza watu washindane, kwa sababu wanafunzi wamekaa kwenye mtihani wa *physics,* wanafanya mtihani huo wa *physics* wote wanakwenda.

Mheshimiwa Spika, kushindanisha shule ni tofauti na kushindanisha wanafunzi. Kwani Kenya haipendi *private sector!* Mbona imefuta kutoa *best school* kwa kutegemea vigezo vya mitihani? Uganda je? *UK* je? Sasa sidhani kama nina haja ya kurudia tena maelezo tuliosema. Tunachosema, tutaangalia vigezo bora vya kushindanisha shule, siyo vigezo vya kusema kwamba wewe tu kwa sababu wanafunzi wanafanya vizuri sana, wewe ni shule bora.

Mheshimiwa Spika, nilitoa mfano mdogo sana hapa, na nirudie tena, hivi shule ambayo imechukua wanafunzi wenye C, C, D, halafu wale wanafunzi wakatoka wote A; na shule nyingine imechukua wanafunzi wote A, wakatoka wote A, wewe unadhani shule gani ni bora? Je, mnafahamu kuna shule zina matawi mawili; moja huku, anayefeli anahamishwa kwa nguvu, mzazi hapewi choice. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtoto ameugua, tunatarajia shule sasa imlee, imsaidie, badala ya kumsaidia, inamtoa ili wabaki kupata A. Ushindani huo hauna afya sana, lakini wanaotaka kutangaza, matokeo yako hadharani. Serikali haiwezi yenyewe ikasema hii shule bora kwa vigezo ambavyo wanataaluma wamevikataa, na machapisho yako mengi, na nchi nyingi zimeacha.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, *Association of Private School Owners,* wakitaka kusema haya, wasituweke sisi, matokeo tunatoa hadharani. Sidhani kama

nina sababu ya kuelezea hili. Kwa nini watu wanadhani hii ni kupambana na *private sector?* Kwa hiyo, hizi nchi ambazo kwa kweli ndiyo *private sector,* zimekubuhu, wameacha. Sasa watu wanawahitaji. Sisi hatuwezi kupambana na *private sector* kwa sababu hiyo. Hata kidogo, na hatuna sababu ya kufanya vile.

Mheshimiwa Spika, tunafurahi wanapofanya vizuri, na ndiyo maana *Samia Scholarship* wapo watu walisema, angalia watu waliosoma *private* wasipate. *No!* Tumesema tunataka wanafunzi waliofanya vizuri waje wawe madaktari wazuri sana, waje wawe ma-*engineer* wazuri sana. Kwa hiyo, haijalishi wametoka wapi? Wametoka wengine *Feza School,* wametoka *private schools,* wameenda mpaka *Samia Scholarship* kwa mashindano hayo. Kwa hiyo, mashindano hatujayakataa, kabisa, naombeni dhana hiyo tuache.

Mheshimiwa Spika, lingine ni mitihani. Kwa nini Olympio kulikuwa na wizi wa mitihani hamkufungia shule kama kituo cha mitihani, lakini shule binafsi mnakuwa na haraka sana ya kufungia? Cha kwanza, wanafunzi wote wanaohusika na wizi na udanganyifu wa mitihani, tunafuta matokeo. Haijalishi anatoka shule ya umma au binafsi. Nyaraka zinaonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shule inayofungiwa kuwa kituo cha mitihani, ni shule ambayo tumeona kulikuwa na *organized effort* ya ku-*cheat* ndani ya shule. Mfumo wa kitaasisi wa kufanya udanganyifu, sio mwanafunzi mmoja mmoja. Hata shule binafsi ambazo unakuta mwanafunzi mmoja mmoja ame-*cheat* hatuzifungii. Nitatoa mifano miwili, mmoja mnaufahamu. Iko shule moja mlisikia binti mmoja analalamika, mimi namba yangu ya mtihani nilibadilishiwa, nikawa nalalamika hawataki. Mtihani wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa nne. Ule wa mwisho ndiyo wakatubadilishia namba, wakarudisha ile namba yangu ya mwanzo, halafu akaitwa na walimu wote wakaambiwa msiseme kilichotokea.

Mheshimiwa Spika, tusingejua kama yule binti asingetoa taarifa. Siyo jamani! Alivyotoa taarifa, tukachunguza, tukagundua ni ukweli. Hiyo shule ilikuwa *one of ten best at some point*. Shule hiyo nadhani iliongoza kwenye mkoa, ikawa *one of the best*.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba mwanafunzi ame-*cheat,* lakini walimu wameshirikiana, wamebadilisha namba za mitihani, wamempa huyu na huyu, *for whatever reasons,* halafu baadaye wanabadilisha, halafu wanaita wanafunzi wanaambiwa msiseme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hata watumishi wa umma walikuwepo tumewachukulia hatua na wale wa nani tumewachukulia hatua alafu tumefunga kama kituo, sasa hiyo tumefunga kwa sababu ya kuchukia *private sector*.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine iko shule mwanafuzi kaingia na simu, hairusiwi lakini ame–*manage* kuingia na simu, ameingia kwenye mtihani akawa anapiga picha maswali halafu amemtumia mwenye shule halafu mwenye shule nje akapanga watu wa ku–*solve* matokeo. Sasa huyo tuna mtetea *private sector* mtakuwa mnafanya kazi nzuri sana, msitetee hiyo *private sector* msitetee hiyo, kwa sababu *private sector* inafanya kazi nzuri sana. Hawa wachache wanaweza waka *tarnish image* huo ni mfano lakini kwani *private sector* tu tunakwenda?

Mheshimiwa Spika, hapa navyozungumza wako watumishi Shinyanga wako ndani, alikuwa Afisa Elimu kwanza alihamishwa haraka haraka akakimbia nadhani akapelekwa Tukuyu tumemfuata, tumemdaka, tumemrudisha yupo mahabusu kwa *reason* tu *organized*. Wako polisi, wako ndani, kwani polisi ni *private sector?* Afisa Elimu ni *private sector?* Na sisi tuna *deal* zaidi kwa nguvu kubwa zaidi na Maafisa wetu ambao tunagundua wanaiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hao ambao tumewakuta, tuliwakutaje? Mtihani umeibiwa Serengeti, kwa kufungua mtihani mapema kwa kufanya mchezo kupiga picha, umetumwa kwenye simu Kahama. Sasa hamuwezi kujua *system* tuliyonayo sasa hivi ukiiba mtihani rahisi sana kukudaka, Kahama watu wamedakwa simu zimekamatwa, tumeangalia zimetoka wapi? Tumekwenda kule tumegundua, polisi aliyehusika kulinda mtihani hao wako ndani, Afisa Elimu yuko ndani na hili hawa ni Maafisa wa Serikali walikuwa wanafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, isihusishe vita dhidi ya *private sector* nakuombeni sana. Kwa nini tufanye vita dhidi ya *private sector*? Kwa nini? Kwa hiyo, Olympio hatukupata mfumo wa kitaasisi wa wizi ni kweli, walikuwa wana–*cheat* wamepatikana, wamefutiwa matokeo kama ambavyo kuna shule za *private* ambazo tumekuta watu wame–*cheat* zikafutiwa matokeo. Shule moja ya Mwanza ilichukua muda kabla ya kuiondoa kama kituo cha mitihani kwa sababu tulikuwa tunafanya uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hilo nilipenda nilizungumze sana, kwa sababu nisingependa *private sector* ione kama tuna pambana nayo ili iweje? Lakini wizi wa mitihani hakuna mtu atakae vumilia mahali popote kabisa. Tushikamane *private sector* na *public sector* tushikamane, tupambane na wizi wa mitihani. *Then* shule hizi za *private* ni nzuri sana, nyingine wala hazifanyi mtihani wa *NECTA* ndiyo wanachukua mtihani wa *Cambridge* wanafanya. Kwa hiyo, tushikamane jamani namna wanafanya kazi nzuri na mimi *I can promise* na Rais wetu, kwa sababu Rais wetu kwanza yuko hivyo hatuwezi kupambana na shule binafsi hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa nilizungumze labda niseme tu mambo mengine ambayo kwa kweli ni *operational* nadhani alikuwa Mheshimiwa Tabasamu

alizungumza hapa kuhusu wananchi wamejiunga, wamejenga shule zao, wamemaliza karibu wamekamilisha wanaomba usajili halafu sisi hiyo lazima niseme sisi kwa sababu mimi nachukua jukumu. Tunakwenda pale tunasema haa hapa kimepunguka maabara kwa hiyo, hatutoi usajili.

Mheshimiwa Spika, tumeishakubaliana wale wananchi ambao wameishajipanga wamefanya kazi imebaki kitu kidogo sana baada ya sisi kukatalia usajili tunapeleka hela tunamalizia shule, shule isajiliwe ianze kufundisha wanafunzi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Tabasamu na wengine wote katika mazingira hayo na tukifanya hivyo tutaimiza wananchi maana yake hamuwezi kuwaambia wananchi hebu changieni tena, tukifika mahali Serikali itakuja itatushika mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuacha kusajili shule kwa sababu haina maabara tu, haina kichomea taka na kadhalika lakini tuna Taasisi yetu ya Elimu na Mamlaka ya Elimu ambayo kwa kweli tunaweza tukai–*direct* bwana peleka kule kwa sababu wananchi wameisha pambana na tuone na tushafanya hivyo naomba hilo twende nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala jingine lilizungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa nadhani suala la *recognition power learning actually* ukisoma Sera ndiyo utapenda zaidi. Ipo sasa hivi lakini, ipo ilikuwa inafanya chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ipo vijana wapo mtaani wanafanya shughuli zao, *VETA* wana wa–*trace*, wanawafatilia, wanasimamia, wana–*observe* vizuri wanakuja wanawapa cheti kwamba kwakweli wewe uwe fundi magari ni mzuri sana cheti hiki ili uweze hata kufanya kazi hata za Serikali ipo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwenye Sera kuna utaratibu nyumbufu, mzuri zaidi wa kuwawezesha watu kupata kila kitu na hata ile nadhani alisema Mheshimiwa Kishimba,

kuwafundisha vijana sijui *house girl* na kadhalika lakini iko kwenye *hospitality* ukarimu, ukarimu unafundishwa kutandika kitanda, kupiga pasi, kupika chakula na kadhalika, kufagia nyumba na vitu vyote vile ambavyo ni muhimu lakini tunachohitaji tumefanya *tracer study* kuangalia wanafunzi wetu waliyotoka kwenye vyuo vyetu wanakubalika vipi? Ili tuweze kubadilisha mitaala kazi yetu kubwa ni kuimarisha tunavyo fundisha kule ili kila mtu aone kweli hawa wanafaa kwa cheti kile waweze kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jingine kubwa niliseme mabweni chini ya darasa la tano. Waraka wa kamshina unasemaje? Unasema kama mwongozo wa 2020 unavyosema yeyote haruhusiwi kuanzisha mabweni chini ya darasa la tano bila kibali maalum cha kamshina. Kama huna hicho kibali maalum, ulipewa *deadline* ambayo tu baada ya kukaa na *private sector* tumesogeza tunaongeza jitihada za kukagua.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mtoto elimu ya awali siyo kwamba anaenda shuleni tu, hata kwenda choo kujisaidia nini *care* yake ni kubwa zaidi ni *more vulnerable*. Kwa hiyo, lazima ukaguzi wake na vigezo vyake view vikubwa zaidi, tunatambua kwamba kuna mahitaji lakin vilevile tuna wajibu sasa sisi tukishatoa kibali kitakachotokea kule tutaulizwa sisi na sasa hivi tunafanya utafiti wa kuangalia ni namna gani ya kubana zaidi kuhakikisha kwamba kwakweli wale watoto wanalindwa lakini kwa kibali maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekutana na *private sector* tukasema na wapo wenye vibali, tukasema mnaendelea lakini tutawakagua, tutawakagua kuhakikisha kwamba kweli hawa watoto wanakuwa *well taken care of* na tuna–*encourage* zaidi watoto wakae na familia lakini tunatambua wako yatima wamechukuliwa na vituo mbalimbali, wako wengine walikuwa nao hawana vibali wamekuja wametuletea *document* tumewapeleka kwa kamishna. Peleka timu kubwa ika kague kule kwa ajili ya kuhakikisha

kwamba hawa yatima wanakuwa *supported* wataondoka wataenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo tunalijua lakini walioko huko *very clear* na maneno yako vilevile bila kibali maalumu cha kamishna haijasema hairuhusiwi. Kwa hiyo, kibali chake ni kigumu kuliko kuanzisha bweni tunaomba tu mtusapoti kwenye hilo na tutafanya kazi vigezo hivyo na *private sector* kuhakikisha kwamba ni vigezo ambavyo kweli vinaleta na. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine la mwisho, mwisho hapa kuna hoja nzuri sana ya vyuo vikuu imezungumzwa sana hapa Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, Mheshimiwa Dkt. Chamuriho na Mheshimiwa Profesa Muhongo wamezungumza vizuri sana, vyuo vyetu kuhusu sasa hapo ndiyo *rank* ipo, unataka ku–*rank* vipi? Hatu–*rank* vyuo vikuu kwa matokeo ya darasani. Vyuo Vikuu vina heshimika kwa utafiti, namba moja na utafiti mzuri ni mwalimu mzuri.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Bunge lako Tukufu lilipitisha fedha shilingi 50,000,000. Kwa muhadhiri yeyote, sasa hivi tunaanza na wahadhiri watakao fanya kazi kwenye *natural science au medicine* waka–*publish* kile alichosema Mheshimiwa Profesa Muhongo kwenye *high impact factor journal* na mwenyekiti wa kamati ya kuweka mwongozo ni Profesa Yunus Mgaya ambaye tuko nae hapa nae ni mtafiti.

Mheshimiwa Spika, akifanya akipata anaondoka na kitita cha milioni 50. Mwanzoni niliona watu wanasema kwa nini usi–*support local journals* Mheshimiwa Profesa Muhongo amezungumza vizuri sana namshukuru sana, sasa hilo linaeleweka. Hatuwezi kuleana hapa kuanzisha *journal* na kupandishana vyeo tutakuwa ni kichekesho, unaweza ukaitwa profesa hapa nchini ukienda nje ukikutana na watu wanavyoongea unawaambia msaidizi hebu usinite profesa

hapa mpaka nirudi nyumbani, kwa sababu hapa nitahadhirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka maprofesa wetu wapande na ushindani wa kimataifa na tunataka kama ambavyo tungependa wachezaji wetu wa mpira kama wale wa simba na wale wengine waweze kucheza kimataifa wakubalike. Tunataka wote Simba na Yanga, wote tunataka wahadhiri wetu wachapishe kwenye ma–*journal* hayo huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuta ku–*reward* kwa kuchapisha huko na yako nje kwa sasa hivi, wenzetu wame *catch up* kwa kuanzia huko leo India wana *journal* nzuri sana lakini walianza kuchapisha huko. Kwa hiyo, siyo matumizi mabaya ya fedha, kwa hiyo, fedha mlipitisha Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana, muongozo tunao nadhani tarehe Katibu Mkuu atatangaza na tutatangaza lini tutatoa tuzo hiyo kwa wale ambao wamechapisha kule na imehamasisha sana utafiti wetu kufanya vile.

Mheshimiwa Spika, nakadhalika tumefanya kitu kingine ambacho ni kikubwa kwenye Tuzo ya Mwalimu Nyerere ambapo na Waheshimiwa mlitoa hela. Tumefanya, tumeshangaa, Miswada iliyokuja mingi kweli kweli washapewa. Namba moja amepewa milioni 10 na Miswada ile inaenda sasa kwa wachapishaji itachapishwa na kuhamasisha *publish industry* hapa nchini unaweza kushangaa hata tuna vitabu vyetu, nexty tutaongeza na vitabu vya watoto tusiwe kama watu wa kubana tu, kubana tu vitabu lakini tunahimiza uandishi wa vitabu vile tulivyosoma wagaga gigi koku lakini tuwe na vitabu vya kisasa hivi vinavyo changasha watu.

Mheshimiwa Spika, lingine na hili litakuwa la mwisho kabla ya kengele ya pili. Kuhusu *English Medium,* yako mengine mengi lakini sikujipanga kuyajibu yote labda yaulizwe, *English medium* kamishna anaporuhusu kwamba

umeenda halmashauri umeomba shule hii iwe *English medium* hasemi kwamba kachaji watu. Shule za Serikali hazichaji ni *free, free* ni elimu bila ada kuifanya *English Medium* hakukupi wewe kibali cha kuleta ada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hayo ya ada nimeuliza kidogo yanakuja kwenye Baraza la Madiwani ambapo sisi wote ni madiwani, hebu twende tukaangalie tunafanya hivyo kwa sababu gani? Kwa sababu kwakweli tunahitaji kwenda na mwongozo wa Serikali kwamba shule za Serikali zitoe elimu bila ada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa muda wako, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…….................……...Sh. 7,979,184,950

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna majina nimeletewa hapa ya Waheshimiwa Wabunge, ambao wanataka ufafanuzi kwenye mambo mbalimbali kutoka kwa

Mheshimiwa Waziri. Niwakumbushe tena kwenye kifungu hiki ambacho kina Mshahara wa Waziri ni jambo mahususi la kisera. Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Jana nilisimama na nikachangia kwenye Wizara hii na kati ya mambo mengi ambayo nilichangia nilionyesha *concern* yangu ya kutoridhishwa na mfumo uliokuwepo sasa hivi haswa lugha ya kufundishia. Nilieleza vizuri umuhimu wa lugha ya kingereza lakini pia niliainisha umri gani mwanafunzi anatakiwa kuanzishwa kufundishwa lugha ya kiswahili.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka *commitment* ya waziri je, ni wakati gani hii fursa itatolewa sawa kwa watoto wote wenye uwezo wa kulipia shule za *private* lakini wale watoto kutoka kwenye familia za kimasikini waweze kuanza darasa la kwanza wakiwa wanafundishwa lugha ya kingereza. Ameongea akasema shule ikiwa tayari ataipa kibali lakini shule hizi ni shule za kwake. Shule za Serikali ziko chini yao wao ndiyo wanatakiwa kuwa tayari je, anatoa *commitment* gani? Kwamba tutaanza kufundishwa lugha ya kingereza siyo somo, masomo yote kama zinavyofanyika kwenye shule za *private?*

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa Waziri, nadhani yeye alipata nafasi ya kukusikiliza kama unavyosema lakini kwa ngazi hii liambie Bunge hoja yako ni nini unayotaka ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri? Kama vile ujachangia, hoja yako ni nini?

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kutaka *commitment* kwa Waziri. Kwamba ni lini shule zote za msingi kwenye nchi hii zitatumia lugha ya kiswahili kama lugha ya kufundishia? *I mean* lugha ya kingereza kama lugha ya kufundishia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nifafanue kwa kifupi sana hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kimea. Kwamba hili suala sasa lipo katika mjadala wa Sera na kama nilivyosema tunaendelea kukusanya maoni mpaka tarehe 31 Mei na maoni ya wadau yatatuongoza sana katika hatua ya mwisho kabla ya kupeleka kwenye maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kwenye sera sasa hivi rasimu ya sera inaonyesha tuna hizo *two-part ways* lakini siwezi kusema hatimaye baada kwanza tukianza kufanya semina Wabunge wote na kusikiliza wadau waliyobaki tutakwenda wapi? Tunachoweza kuji–*commit* kwenye mitaala ni kwamba lugha zote zitafundishwa vizuri zaidi na tunaji–*commit* tuhakikisha kwamba watakapo maliza kwa mfano darasa la sita kama itapita inavyotakiwa mtu awezi kuwa na *command* ya lugha ambayo atakuwa amefundishiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kimea, naona ameketi kwa hivyo ameelewa ufafanuzi. Mheshimiwa Eric James Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana swali langu ni lile lile la miaka yote *recognition of prior learning*, nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Hayo maneno yana kiswahili chake? au Hayana?

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Ngoja nijaribu kutafsiri kwa Kiswahili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hapo akusaidie Mheshimiwa Almas Maige, hayo maneno kama unahitaji muda kidogo naweza kuita Mbunge mwingine ili Mheshimiwa Almas Maige

akusaidie kiswahili chake halafu nitakupa tu fursa yako Mheshimiwa Shigongo. Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Serikali inao utaratibu wa kutoa ruzuku ya kuendeshea vyuo vya kati. Vyuo hivi vinachukua wanafunzi wale ambao wameshindwa kuendelea ambao wameshiwa darasa la saba, *form four* na *form six* kimsingi ambao wameshindwa kwenda vyuo vikuu na wengi wao ni watoto wa masikini lakini kimsingi hawapatiwi mikopo kwa ajili ya vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wanaotokana na vyuo vya kati ni rahisi kuajirika na kurudisha mikopo kwa haraka. Hoja yangu ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha watoto hawa wanapatiwa mikopo na kama sijaridhika nakusudia kutoa shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ngoja msaidizi akusogezee maji maana kama utafika na kwenye kushika shilingi sijui utazungumzaje? Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo kidogo kwa Mheshimiwa Hawa Mchafu, kuhusu wanafunzi wa vyuo vya kati kama ifuatavyo; ni kweli kwamba sasa hivi Bodi ya Mikopo haijaanza kupeleka mikopo kwenye vyuo vya kati. Kwa sababu ya bajeti na kama unavyoona tunaongeza idadi ya wanafunzi wa vyuo vikuu kwenda taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mazungumzo yanayoendelea na Wizara ya Fedha kuwa na namna ambavyo tuweza tuka–*introduce* vyuo vya kati katika mikopo na pengine kwenye bajeti ijayo tutakuwa tunaweza tuka–*reflect*.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi kwa kweli kwenye *VETA* ruzuku ya Serikali ni kubwa sana. Kwa sababu ukisoma kwenye *VETA* nadhani karibu shilingi 200,000 ambayo ni ruzuku karibu ni milioni moja na kuna wanafunzi wengine wa vyuo vya kati sasa hivi kwa kweli sasa hivi wanatozwa *too nominal fees*, wanafunzi wanaosoma *diploma* nadhani *Arusha Tech* na *DIT* wanalipa laki moja lakini wanakula, wanalala bwenini na wanasoma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatambua kwa kweli umuhimu wa ku–*support* vyuo vya kati lakini nirudi tena kwenya Sera ukiangalia mfumo wetu wa Sera sasa hivi unaenda kutambua zaidi mafunzo ya amali ambayo yanatufungulia fursa ya Serikali kuongeza *support* ya wanaoenda kule. Kwa sababu tumesema tusingependa wanaochukua mkondo wa mafunzo ya amali, wahisi kwamba wananyanyapaliwa kwa maana hiyo tutajitahidi sana katika utekelezaji wa sera kuhakikisha kwamba tunawachukua wote wanaenda mbele. Naomba Mheshimiwa Hawa Mchafu asininyime Mshahara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, naona umesimama.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhishwa na ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri, hivyo naomba nitoe shilingi na Waheshimiwa Wabunge naomba mniunge mkono tuweze kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante.

**MWENYEKITI:** Hoja aijaungwa mkono na hesabu mliyosimama mko sita na yeye ni wa saba. Sasa hoja inaungwa mkono kwa watu wangapi? ama amjasoma kanuni zenu? ni watu kumi hoja aijaungwa mkono na pamoja na maneno hayo yote hakuna aliye ongezeka. Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nitafsiri kwanza neno la *recognition of prior learning* kama ulivyo elekeza ni utambuzi wa ujuzi uliyopatikana nje ya mfumo maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naweza nikaendela kwa ridhaa yako.

**MWENYEKITI:** unaweza kuendelea. Naliweka tu hilo ili tuwe tunapata picha sisi wenyewe Wabunge siyo tunapewa tu maoni kama vile tunamkabidhi mtu kazi, na sisi pia ni kazi yetu. Kama tunasema Kiswahili kimekamilika basi tukamilishe tusiingize huko maneno ya kiingereza, na kama tunasema twende kwenye Kiingereza na sisi tuanze kuhama taratibu. Mheshimiwa Shigongo karibu. Unaweza kutumia pia hayo ya Kiingereza kama ya Kiswahili yanakupa tabu. *(Makofi)*

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayanipi tabu. Naomba nisome kwenye *website* ya *TCU*. Wanasema hivi; "*The Tanzania commission of universities (TCU) has launched a new recognition of prior learning initiatives, to allow students with only primary education to be admitted to higher learning education based on work experiences, and that will start from 2013/2014 academic year.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni kwamba *TCU* iliamua kuwachukua watu wenye ujuzi waliopata nje ya mfumo wa elimu ili waweze kujipatia elimu ya ziada kwa ajili ya kuboresha taaluma zao. Sasa wako watu katika nchi yetu, vijana katika nchi yetu ambao Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi wamefanya mambo makubwa sana. Nitatoa mifano ya watu wachache. Masoud Kipanya kwa mfano amefanikiwa kuunda gari, yuko mtu mmoja kule Iringa kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mwanyika aligundua umeme na anasambaza kijiji kizima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa aina hii wanapotaka kuendeleza elimu zao kupata elimu zaidi kwenye eneo hilo wanashindwa kuwa-*admitted* kwenye vyuo vikuu kwa sababu hawana vyeti vya sekondari. Sasa *TCU* walipitisha hili jambo mwaka 2013/2014; lakini baadae lilikuja kuondolewa likafutwa. Sasa mimi ni miongoni wa watu waliopata elimu kwa mfumo huu. Na kwa nini nazungumza? Nazungumza kwa sababu wako watu wengi, ingawa mimi nilipata ningeweza kunyamaza; wako vijana wengi sana tunawanyima fursa ya kusoma kwa sababu ya huu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama ambavyo mmefanya miaka yote. Serikali itafakari jambo hili ili utaratibu huu uweze kurudi. Sasa nimesimama hapa kutafuta *commitment* kwamba Mheshimiwa Waziri…

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha sekunde 30 malizia.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commirment* ya Mheshimiwa Waziri. Je, ni lini mfumo huu wa *prior* utarejeshwa tena? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nitolee maelezo hoja ya Mheshimiwa Eric Shigongo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza *recognition of prior learning* inaweza ikahitaji bado kupitia *stage* japo unakuwa kwenye mfumo ambao siyo rasmi. Chukua mfano tu, kwamba mtu anataka Kwenda kusoma *degree* ya *physics* chuo kikuu au *mechanical engineering*. Ameunda gari huku pembeni ukienda kwenye *mechanical engineering* ukiingia darasani na *theory* na *component* ya *practical training* utafeli. Kwa hiyo inawezekana tu ukasaidiwa kuanza *step by step,* kupata vyeti vile unavyohitaji halafu baadaye ukaenda,

na hilo liko kwenye sera mpya ya sasa hivi, inaitwa unyumbufu, namna mbadala ya kuweza kupata elimu; lakini lazima upitie zile ngazi ili uwe umeandaliwa zaidi kwenda kwenye kazi ambazo ni za *theory*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye upande wa mafunzo ya amali, sasa hivi inafanyika. Si *level* ya chuo Kikuu lakini inafanyika, na inafanyika hasa kupitia kwa ushirikiano na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara yetu. Kama nilivyosema ukiwa ni fundi seremala unafanya kazi yako vizuri unaweza uka-*apply* uje ukaguliwe, wanafuatilia kazi yako unayoifanya, waniangalia, wanaipima, wanaikagua, wanafika mahali wanasema kwa kweli wewe unastahili kupata cheti hiki cha *VETA* kwa sababu siku Serikali inatangaza kazi inasema anatakiwa fundi mwenye cheti, unaweza ukaenda nacho japo hukukaa darasani. Hiyo ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namna ya Kwenda ngazi moja hadi nyingine kwa kweli ile *rig* ambayo inatakiwa wakati mwingine inaweza ikawa inafanya kazi *medium.* Kwa mfano, ukaifungua hiyo moja kwa moja, tutachukua kwa mfano *medicine* lazima ujiulize huyu mtu ni vitu gani mabavyo anatakiwa aende anavyo. Sisi tunasema tuna-*commitment* ya kufanya vile *within the constrain,* kwa kuangalia kwamba kwa kweli hatushushi ubora na wala hatuwezi kumpeleka mtu kwenda kumuadhiri akiingia darasani akafeli. Yale ambayo anaweza akafanya kwa njia mbadala na akafika sehemu hiyo tunai-*support* na iko-*supported* kwenye rasimu ya Sera ambayo sasa hivi iko hadharani kwa ajili ya kila mtu kuiona.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Eric Shigongo nadhani ameridhika amekaa. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Sikusudii kushika shilingi ya Profesa Mkenda ila ni kupata tu ufafanuzi. Ninapoongelea

kupokea teknolojia naongelea teknolojia kubwa kubwa zile duniani, mfano *robot Sophia* ambavyo anafanya shughuli zake na sisi wote tunajua na sisi tunatamani mambo kama haya Tanzania yawepo. Lakini kwa sasa hivi kwa Profesa Mkenda kulingana na *profession* yake nataka kuongelea kuna kitu kinaitwa; kwanza niseme *artificial intelligence* ni akili bandia ili usinikosoe na hilo neno; nataka kuongelea kuna kitu kinaitwa *chat-GPT* au *open artificial intelligent*. Lengo nataka kumwambia nini Mheshimiwa Mkenda, yaani atusaidie kutufafanulia, kwamba wao Wizara ambayo inasimamia teknolojia wamejipangaje na kupokea teknolojia hizi? Kwa mfano hii *chat-GPT* Profesa Mkenda inaenda kukuchonganisha wewe na walimu wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezoea kuona *google* inaweza ikakupa kila kitu, najua unashangaa hata wewe, ni vitu vipya kwenye ulimwengu wa teknolojia, ukubali uweke kitengo huko kwako tuwe tunakushauri watu wa mambo ya teknolojia. *Chat-GPT* inaenda kukuchonganisha wewe na walimu wako, kwa sababu gani? ni zaidi ya *google*. Kama mwanafunzi wa chuo kikuu anaweza akabahatika akaingia na *smart phone* kwenye mtihani wake ni zaidi ya profesa. *Chat-GPT* naweza nikamwambia naumwa nifanyeje? Ananiambia kila kitu. Na kama unavyojua, tuko kwenye ulimwengu amabo kila mtu anataka vitu vilivyo rahisi rahisi. Sasa sisi kama Serikali ili tusiendelee kupitwa, huu ni mfano tu nimetolea, tumejipangaje na mambo kama hayo? Na wewe kama Waziri ambaye umepewa dhamana kabla hamjapokea ushauri wa kuunda Wizara ya Teknolojia, huko ndani kwenye Wizara yako mmejipangaje kupokea haya mambo yawe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo ya Mheshimiwa Mbunge wa Momba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kwamba teknolojia sasa hivi inatupeleka mbali sana kiasi kwamba inawezekana mtu aka-*solve* mtihani au akaandika insha kwa kutumia *ICT Technology.* Na unaweza ukaisahisha usipokuwa makini ukadhani ni kitu ambacho ni *original* kumbe ni kitu ambacho ameenda tu ameingia kwenye *computer* ku-*forge.* Ni *movement* ya *technology* ambayo ni changamoto hata katika nchi nyingne lakini kuna taratibu sasa zimeundwa katika vyuo vingine kuhakikisha kwamba inazuia. kwa mfano mwanafunzi atakaa darasani badala ya kuchukua *homework* anafanyia palepale mnaiangalia inavyokwenda kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa ujumla wake suala la *technology;* nitarudi tena kwenye sera na mitaala. Nitoe mfano mmoja tu, sasa hivi kwenye mitaala mipya wanafunzi wetu wataanza kufundishwa kitu kinachoitwa *coding* kuanzia *primary school*. *Coding* siyo *ICT* lakini *coding* kwa kuwafanya wajifunze kufikiria kimantiki kwa namna ambayo wanaweza wakajenga *algorithm.* Kwa hiyo wakisonga mbele wakiingia *o–level* wanaweza wakaanza kusioma sasa *computer science* na wanaweza wakaaknza kuandika *programing* na kwenda mbele na kusonga mbele. Kwa sababu haya mambo mengi haya yanapogundulika ni kwasababu ya *ICT technology.* Sasa sielewi hilo suala mwingiliano kati ya Wizara moja na nyingine lakini ukweli chimbuko la sayansi na teknolojia bado liko katika shule na bado liko katika elimu na sisi katika mitaala yetu tumewekeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ikipita hii mitaala kuanzia sasa wanafunzi watakaoingia darasa la kwanza wataanza na *coding*, wakiingia *form one* wataanza nadhani somo linaitwa *computer science* kama sikosei. Tunakwenda mbele kwa ajili ya kuandaa kwamba na sisi tunaweza ku-*catch up* na *technology*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Phillipo Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama hapa kuomba Serikali itupunguzie tozo kwenye shule binafsi baada ya kuonekana kuna tozo zaidi ya 18, na hivi kuleta mzigo mkubwa sana kwa wazazi wanalipa ada na michango. Pia kuna tozo zingine ambazo ziko ndani ya uwezo wa Serikali kama ambavyo, wale watoto kama tunavyosema kila wakati ni watoto wa Watanzania wote, na nyinyi Waheshimiwa Wabunge mna watoto kule, lakini bado Serikali imefuta ada za *NECTA* kwenye shule za umma zote tangu mwaka juzi na mwaka jana wamefuta kwenye *form six,* lakini shule za *private* bado tozo hiyo ipo na ni kubwa sana tena ina penalty. Ni shilingi 50,000 kwa mwanafunzi wa kidato cha nne au kidato cha sita, na usipolipa mpaka wakati wa mtihani unalipa mara mbili yake unalipa 100,000. Wazazi wanashindwa na hivyo mpaka kukuzuia matokeo ya Baraza la Mitihani yanapotoka. Nilikuwa naomba *commitment* ya Serikali waanze kutufikiria kututolea tozo hizo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua hoja ya Mheshimiwa Mulugo kama ifuatvyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa yale ambayo yako ndani ya uwezo wa Wizara tumeyatamkia hapa sasa hivi. 100,000 ilikuwa ni kwamba kuna sehemu wanatakiwa wafanye mitihani mingi, *mock exam* na kadhalika unalipia na walisema hata wazazi hawajachagia lakini shule zinalipia. Kama nilivyosema baada ya hapa nilionmgea na Kamishna wa Elimu, kwa sababu yuko kisheria na akaniambia atatoa mwongozo kuhakikisha kwamba shule binafsi hazilazimiki kufanya hiyo mitihani. Tunaweza tukazi-*encourage* zifanye lakini zikiona ni *burden* hazilazimiki kufanya. Hiyo ni namna moja ya kwetu ya kuondoa tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine kwa kweli ni mchakato ambao sasa hivi siwezi kufanyia *commitment* ya namna yoyote kwa sababu ni mchakato wa Serikali kwa upana wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo naona umeridhika, ameketi. Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa naomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu halmashauri kujenga shule za *english medium* kwa kutumia mapato ya ndani na kuwatoza wananchi, nini kauli ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya hoja ya Mheshimiwa Taska Mbogo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zote za Serikali zinaendeshwa bila ada mpaka *form six,* na huo ndio msimamo wa Serikali, na haijalishi kama shule imepewa kibali cha kuendesha masomo yake kwa kingereza au Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Haya naona Mheshimiwa Taska Mbogo ameridhika. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mwaka 1978 tulitunga Sheria Namba 25 ya Elimu ambayo kwa mara ya kwanza Idara ya Ukaguzi wa Shule ilitambulishwa rasmi, ambapo baadaye sana 2017 tukabadilisha ikawa inaitwa Idara ya Udhibiti Ubora. Lakini mpaka leo ni zaidi ya miaka nane tangu tutunge, tulete ule Waraka wa Utumishi wa Serikali namba tatu wa mwaka 2014, ambao uliwaingiza wadhibiti ubora wakuu wa wilaya na kanda kuwa sehemu ya watakaopata posho na mishahara kwa ajili ya kazi hii katika sekta ya elimu; lakini mpaka leo imepita miaka nane hakijawahi kufanyika chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hata kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ukurasa wa 64 na 65 aliozungumza kuhusiana na wadhibiti ubora, hajasema chochote kuhusiana na maslahi ya kitendaji wa wadhibiti ubora nchini.

Sasa mimi sina kusudio la kushika shilingi lakini hata majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri aliyoyajibu huku kwenye hotuba hayapo. Sasa naomba nipate kujua utayari na maelezo ya Serikali kuhusiana na maslahi ya wadhibiti ubora nchini ambao ndio jicho la sekta yetu ya elimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kutoa ufafanuzi kwenye eneo hilo ambalo amelielezea Mheshimiwa Nusrat Hanje. Tumesema ni kweli Waraka ule namba tatu wa mwaka 2014 ulichelewa kutekelezwa. Lakini ulichelewa kutekelezwa kwa sababu muundo wa Wizara ilikuwa bado haijawaingiza

watumishi hawa wadhibiti ubora katika kada ya uongozi. Lakini nimesema kwamba mwezi Aprili tulipeleka muundo ule kwa Mheshimiwa Rais na tayari ameshausaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimuondoe hofu, katika mwaka wa fedha ujao kwa maana kuanzia Julai, zile stahiki kwa maana ya Wizara pamoja na posho zao zitakwenda sasa pamoja na ule muundo ambao uliowekwa. Kwa hiyo inawwezekana ukawa na marekebisho ndani ya bajeti ile ile kufanya *reallocation* na nini lakini kimsingi tunakwenda kuzingatia maboresho au muundo huu sasa wa Wizara na zile stahiki zao zitakwenda kuwa ndani ya bajeti au watakwenda kulipwa kama muundo unavyotaka, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……Sh.1,138,059,501
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*………..Sh. 2,210,592,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…………………Sh. 1,132,323,200
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*..............................................Sh. 627,916,000
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*................................................Sh. 513,950,000
Kifungu 1007 – *Legal Unit*……………………………Sh. 461,292,000
Kifungu 1008 – *Information, Communication, Technology and E-Learning*……..Sh. 624,256,000
Kifungu 2001 – *Basic Education Development Office*.......................................Sh. 73,925,677,004
Kifungu 2002 – *School Quality Assurance*……Sh. 42,869,261,659

Kifungu 5001 – *Teachers' Training*……………………….………Sh. 0
Kifungu 7001 – *Higher Education*…...………..Sh. 301,061,782,798
Kifungu 7002 – *Technical and Vocational Training Division*……….……………….....Sh. 54,453,962,189
Kifungu 8001 – *Higher Education*……..………Sh. 50,882,504,699

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu bilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajielekeza kwenye fungu 18, Tume ya Taifa ya *UNESCO*, ukurasa sa 79.

**Fungu 18 – Tume ya Taifa YA *UNESCO***

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…..........……………Sh. 2,733,888,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati yako inaomba ijielekeze katika Kitabu cha Nne cha Matumizi ya Maendeleo. Ukurasa wa 107, tunaanza na Kifungu 1001.

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*………………………Sh. 840,000,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………..…..........................Sh. 2,374,947,200

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu bilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……...Sh. 65,676,499,102

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……………………Sh. 354,577,800
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*…………………………………………Sh. 260,700,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 – *Basic Education Development Office*………………………………..Sh. 155,775,609,380

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu 2002 – *School Quality Assurance*………Sh. 7,763,795,00
Kifungu 5001 – *Teachers' Education*…………………………...Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 7001 – *Higher Education*…………….Sh. 810,718,794,036

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu 7002 – *Technical and Vocational Training Division*…………………………….Sh. 83,607,642,482
Kifungu 8001 – *Science, Technology and Innovation*……………………….Sh. 10,500,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba kamati ya matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa Hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa kuwa, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja imeungwa mkono na kwa utaratibu wetu sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge baada ya Wabunge wote kuafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri, nitumie sasa fursa hii kutangaza rasmi kwamba, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2023/2024, yamepitishwa rasmi na Bunge. Hivyo, nitumie pia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote walio chini ya Wizara hii kwa kupitishiwa bajeti yenu na Bunge, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Niwapongeze pia kwa sababu, mmepokea sifa nyingi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge katika utendaji wenu, pamoja na changamoto ambazo wameziainisha, ambazo wanatamani maboresho yaendelee kufanyika, lakini mmepokea pongezi nyingi, kwa hiyo, nami nawapongeza sana. *(Makofi)*

Pia, niwapongeze kwa utayari wenu na usikivu kwa mawazo wanayotoa Wabunge kupitia Kamati yetu ya Bunge ambayo nayo inafanya kazi nzuri, lakini na ninyi ni wasikivu maana humu ndani kidogo kungekuwa na mambo mambo kama mambo yangekuwa hayaendi vizuri kwenye Kamati. Kwa hiyo, nawapongeza pia, kwa usikivu wa kusikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka kwenye kamati, lakini pia na hapa Bungeni. *(Makofi)*

Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa yale mliyoyaahidi kwenye bajeti yenu, lakini na yale ambayo mmeahidi kwamba, mmeyachukua ambayo Wabunge wameyachangia kwa maana ya kuendelea kuboresha sekta yetu ya elimu ili viwango viendelee kupanda. *(Makofi)*

Niishukuru vile vile Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ambayo inajishughulisha na Wizara hii. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hii, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mnafanya ya kuisimamia Wizara hii na tunaamini mtaendelea kufanya vizuri zaidi ya hapo, ili elimu

yetu iendelee kupaa huko duniani ifanane na wengine, tuwe na sisi tukijilinganisha na wengine na sisi tuwe tunapata wanafunzi kutoka maeneo mengine kuja kujifunza hapa kwetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuishauri Serikali maana huu sio mwisho, wataendelea kupokea maoni yenu, hasa kipindi hiki ambacho Sekta ya Elimu inapitia mabadiliko makubwa. Ni muhimu sisi sote kuwa sehemu ya hayo mabadiliko, ili Serikali itakapofika sehemu sasa kwamba, hapa tumeshapokea maoni ya wadau basi na maoni yetu yawe yamesikika kule kuliko kukaa huku nyumanyuma halafu badaye Serikali imefanya maamuzi ndio tunaanza pale na hapa, tuwaambie mapema maana ni kazi yetu kuishauri Serikali.

Kama Serikali itaona jambo hilo hawawezi kulifanyia kazi muda huu, basi wataanzia hapo wanapoanzia halafu baadaye wakati wa kuisimamia mtasema hapa mmefeli, lakini Bunge wakati ule tulichangia, tulisema hivi na hivi kwa hiyo ni muhimu sana kufuatilia huu mchakato mzima kwa sababu, sisi ni wawakilishi wa wananchi na tungependa wototo wa nchi hii wapate elimu iliyo bora. Kwa hiyo, sote tushiriki katika huu mchakato wa mabadiliko. Mheshimiwa Waziri nakutakia kila la heri katika hayo yote na nikisema nakutakia kila la heri, maana yake Bunge linakutakia la heri katika hayo yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna mambo mawili; Mheshimiwa Waziri wakati ukitoa ufafanuzi hapa, lakini pia wakati imetolewa hoja, nafikiri na Mheshimiwa Taska Mbogo, kuhusu hizi shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia za halmashauri. Amesema kwamba, Halmashauri zinatumia mapato yao ya ndani kujenga hizo shule, maana yake halmashauri zinapojenga shule hizi, pamoja na kwamba ni za huduma, lakini zinajenga kama chanzo cha mapato. Kwa hivyo, ni muhimu sana Serikali pamoja na kutoa

ufafanuzi huu, kujaribu kukaa chini kuangalia namna halmashauri itakavyoweza kuendesha hizi shule ikiwa na zenyewe zitatolewa bila ada kwa sababu, ni dhahiri hakuna mzazi ambaye atataka akamwandikishe mtoto wake shule ile ya kawaida, ikiwa ipo hii inayotoa elimu kwa lugha ya Kiingereza aache hii, halafu aende kule kwingine. *(Makofi)*

Sasa ile ada ndio ambayo kidogo huwa inazisaidia Halmashauri kuendesha hizi shule. Kwa hivyo, Serikali nafikiri mtaenda huko mkae kwa namna yenu mnayofanya, kwa utaratibu wenu wa kawaida, halafu mzielekeze hizi halmashauri zifanye nini kwenye hizi shule, kwa sababu, la sivyo, tutatengeneza tatizo badala ya kulitatua kwa sababu, halmashauri zimejenga shule hizo kama kitega uchumi. Hilo lilikuwa la kwanza. *(Makofi)*

La pili, na kwa sababu tuko katika mchakato huo wa sera, jambo lingine la kutazama nadhani kwa sababu, sisi nchi yetu si kisiwa na nchi zote duniani huwa zinakuwa na bora, bora wa kwanza, bora wanaendelea mpaka watakapofika huko chini hata kama wote ni bora, lakini anakuwepo pale juu. Sisi huu mfumo nadhani vyuo vyetu kwa miaka kadhaa tumeuondoa, tukitaraji kwamba, tutafika mahali ambapo vyuo vikuu vyote vitafanana. *(Makofi)*

Kwa muktadha huo wa kufikiria vyuo vyetu vyote vitafanana, tumeweka mazingira yale ambayo yanataka mwanafunzi yeyote aingie popote. Sasa hiyo, kidogo kama nchi, tutakuwa hatupigi hatua, lazima tufanane na wenzetu ambao wametutangulia. Tukisema kwamba, tunataka kila mtu akasome chuo fulani, ili tu tufanane wote itakuwa kidogo ni ngumu na ndio maana humu ndani Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashahidi, wamesimama hapa Maprofesa wawili kuchangia Bunge lilikaa kimya kusikiliza hoja za Maprofesa wakizungumza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa tukifika mahali ambapo tunafikiri nchi yetu kila mtu atakuwa Profesa, tutakuwa hatuna uhalisia, pia tukifika mahali tukafikiri nchi yetu lazima kila mtu awe na *degree* tutakuwa hatuna uhalisia na tukifika mahali tukafikiri nchi yetu kila mtu lazima awe ni yule, umeeleza vizuri hapo kwenye hoja ya Mheshimiwa Shigongo kwamba, kila mtu ataenda chuo kikuu akae darasani afundishwe yale mambo, tutakuwa hatuna uhalisia. Wanadamu huzaliwa tofauti, yapo mambo ya kawaida kabisa yanayotutofautisha na hata ninyi Waheshimiwa Wabunge, wakati tukisoma hata shule za sekondari zilikuwa na tofauti ukienda shule hii, ukienda shule hii. *(Makofi)*

Mimi sioni kama ile mifumo ilikuwa na shida sana kuliko hiki tunachojaribu kukitengeneza. Nadhani ule utofauti hauna shida kabisa katika nchi kwa sababu, lazima huyu awepo mmoja na mwingine amsaidie, eeh, si ndio? Sasa kama wasaidizi wote mtakuwa mnalingana, sijui nani atamsaidia mwenziwe? Kwa hiyo, wale wasaidizi wanahitajika. Sasa watapatikana vipi, mifumo hii imetengenezwa kwa muda mrefu atapatikana vipi msaidizi wa huyu mmoja. Acha wanaofikiri wwe wachache, watendaji wawe wengi.

Waheshimiwa Wabunge, tukifikiri kwamba, kila mtu atakuwa mtendaji, ndio tunafika hapo kufikiri kila mtu anatakiwa awe na *degree,* kila mtu anatakiwa awe na *PhD,* maana sasahivi *PhD* nazo zimeshakuwa mtihani, kila mtu anaihitaji hata kama hana shughuli nayo. Sasa hilo nalo limetupeleka huko ambako sitaki kurejea kwenye hizo changamoto, lakini lazima kama Taifa tufike mahali tuondokane na haya mambo yanayotufanya watu waahirishe huko nje waseme, bwana tukifika huku usiniite Profesa, subiri turudi nyumbani au usiniite Daktari subiri turudi nyumbani.

Sasa hayo lazima tuondokane nayo kama Taifa kwa sababu na sisi ni sehemu ya ulimwengu hatuko nje ya huo

ulimwengu na tusijiwekee mazingira ya sisi kuchekwa kwamba, unajua huyu anatoka Tanzania kwa hiyo, hata msimsikilize hana anachojua, ama yeye mwenyewe anaogopa kufungua mdomo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo moja hapa na linatoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa na Katibu wa Bunge kwamba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hasa inayosimamia Sera, Bunge na Uratibu na Mheshimiwa Waziri yuko hapa, inawaalika Wabunge wote kuhudhuria sherehe za Ufunguzi wa Jengo la Ofisi za Ikulu, Chamwino, Dodoma. Sherehe hizo zitafanyika siku ya Jumamosi, tarehe 20 Mei, 2023, kuanzia saa 2.00 asubuhi katika viwanja vya Ikulu, Chamwino.

Kutakuwa na usafiri wa pamoja kwa Wabunge wote utakaoanzia katika viwanja vya Bunge kuanzia saa 12.00 mpaka saa 1.00 asubuhi. Kwa hiyo, saa 1.00 asubuhi mabasi yatakuwa yanaondoka hapa Bungeni kuelekea Chamwino na baadaye kuwarejesha Wabunge hapa Bungeni, ili kila mtu aweze sasa kuendelea na shughuli zake za siku hiyo.

Waheshimiwa Wabunge kadi za mialiko zitaendelea kugawiwa kwenu na baadhi yenu pengine mmeshazipata na zingine zitaendelea kugawiwa kesho mpaka siku hiyo itakapofika. Kwa hiyo, mmetangaziwa mapema ili mjiandae kwa ajili ya mwaliko huo ambao ni wa muhimu kwa kweli kwa sababu, tumekuwa tukizungumza kuhusu kuhamia Dodoma na tunajua watu wote tumehamia Dodoma, lakini sasa Ikulu, rasmi Dodoma, kwa hiyo, ni muhimu sana kuwa sehemu ya historia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.11 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 18 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*